

**TATHMINI YA UAINISHAJI WA TANZU NA VIJITANZU VYA FASIHI
SIMULIZI KATIKA VITABU VILIVYOIDHINISHWA: KAUNTI YA
MAKUENI**

CAROLYNE NZILANI MUNYAO

C50/CE/34394/2016

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA KUHITIMU SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA
KENYATTA.**

OKTOBA, 2025

IKIRARI

Tasnifu hii ya uzamili ni kazi yangu binafsi na haijatolewa katika chuo kikuu kingine
kwa mahitaji ya kuhitimu shahada yoyote.


Sahihi.....

Tarehe.....30/10/2025.....

CAROLYNE NZILANI MUNYAO

C50/CE/34394/2016

Tasnifu hii ya utafiti imewasilishwa kwa idhini ya msimamizi katika idara ya Kiswahili:

Sahihi.....

Tarehe.....30/10/2025.....

Dkt. JESSE MURITHI



TABARUKU

Kwa wazazi wangu Oliver na Regina,
Mume wangu Japheth,
na watoto wangu Austin na Arthur.

SHUKRANI

Kwanza, ninamshukuru Mungu kwa kuniwezesha kukamilisha utafiti wangu. Pia, kwa kuniongoza tangu nilipoanza masomo ya shahada ya uzamili hadi kufikia mwisho. Shukrani kwa msimamizi wangu, Daktari Jesse Murithi, kwa uelekezi wa kitaaluma. Kwa wahadhiri wa chuo Kikuu cha Kenyatta natoa shukrani za dhati kwa mafunzo niliyopata.

Kwa wahadhiri katika idara ya Kiswahili nashukuru kwa kunipa umilisi wa mawanda mbalimbali ya somo la Kiswahili. Aidha, ninawashukuru walimu wakuu, wakuu wa idara, walimu wa Kiswahili na wanafunzi kwa usaidizi wenu katika utafiti wa nyanjani.

Mwisho, shukrani za dhati kwa familia yangu kwa kunivumilia kipindi hicho na kunipa motisha kukamilisha masomo yangu. Wanafunzi wenzangu wa uzamili walionifaa katika safari hii ninawashukuru. Asanteni.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU	ii
SHUKRANI	iv
YALIYOMO	v
ORODHA YA MICHORO	viii
ORODHA YA JEDWALI	ix
ISTILAHU MUHIMU	x
ORODHA YA VIFUPISHO	xi
IKISIRI	xii
ABSTRACT	xiii
SURA YA KWANZA	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.3 Suala la Utafiti	3
1.4 Malengo ya Utafiti	4
1.5 Maswali ya Utafiti	5
1.6 Sababu za Kuchagua Mada	5
1.7 Upeo na Mipaka	6
1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada	8
1.8.1 Tafiti kuhusu Vifaa na Mbinu za Kufundishia	8
1.8.2 Kazi Zilizandikwa kuhusu Fasihi Simulizi, Uainishaji na Uwasilishaji.	-11
1.8.3 Tafiti kuhusu Fasihi Simulizi	-14
1.9 Misingi ya Kinadharia	-15
1.9.1 Nadharia ya Tanzu	-16
1.9.2 Nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili	-19
1.10 Mbinu za Utafiti	-23
1.10.1 Mahali pa Utafiti	-23
1.10.2 Muundo wa Utafiti	-23
1.10.3 Uteuzi wa Sampuli	-24
1.10.4 Mbinu za Ukusanyaji Data	-25
1.10.5 Mbinu za Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji	-25

1.10.6 Maadili ya Utafiti -----	26
1.11 Hitimisho -----	26
SURA YA PILI: TOFAUTI ZA UAINISHAJI WA TANZU NA VIJITANZU VYA FASIHI SIMULIZI-----	27
2.1 Utangulizi -----	27
2.2 Dhana ya Fasihi, Fasihi Simulizi na Uainishaji -----	28
2.3 Uainishaji wa Fasihi Simulizi kwa mujibu wa Vitabu Tofauti-----	29
2.3.1 Kiswahili Kitukuzwe -----	30
2.3.2 Chemchemi za Kiswahili -----	33
2.3.3 Johari ya Kiswahili-----	36
2.3.4 Kiswahili Fasaha -----	37
2.4 Tanzu Kuu zenye Utata wa Uainishaji -----	40
2.4.1 Mazungumzo-----	42
2.4.2 Ngomezi -----	43
2.5 Vijitanzu vya Fasihi Simulizi vyenye Utata wa Uainishaji-----	44
2.5.1 Miviga-----	45
2.5.2 Ulumbi -----	47
2.5.3 Soga -----	49
2.5.4 Ngano-----	51
2.6 Maelezo Tatanishi ya Istilahi/Msamiati na Idadi ya Tanzu-----	52
2.7 Mabadiliko ya Matoleo na Urekebisho wa Makosa -----	54
2.8 Hitimisho-----	56
SURA YA TATU: VIGezo VYA KUAINISHA TANZU NA VIJITANZU VYA FASIHI SIMULIZI-----	58
3.1 Utangulizi -----	58
3.1.1 Dhana ya Misingi na Vigezo katika Uainishaji -----	58
3.1.2 Vigezo vya Kuainisha Fasihi -----	59
3.2 Vigezo vya Kuainisha Tanzu na Vijitanzu vya Fasihi Simulizi -----	60
3.2.1 Uwasilishaji -----	62
3.2.2 Muundo/ Umbo-----	64
3.2.3 Wahusika -----	68
3.2.4 Maudhui -----	70
3.2.5 Wakati na Mahali-----	73

3.2.6 Ala/ Kifaa cha Utendaji-----	74
3.2.7 Umri-----	74
3.3 Mwingiliano wa Tanzu -----	75
3.4 Hitimisho-----	79
SURA YA NNE: SULUHISHO KWA UTATA WA UAINISHAJI WA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI-----	81
4.1 Utangulizi-----	81
4.2 Viwango Vya Umilisi Vya Wanafunzi -----	81
4.3 Mitaala ya Ufundishaji wa Fasihi Simulizi -----	84
4.4 Utahini na Ufundishaji wa Fasihi Simulizi -----	87
4.5 Vitabu vya Kufundishia-----	95
4.6 Mbinu za Ziada za Kufundishia Fasihi Simulizi -----	96
4.7 Hitimisho-----	99
SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO, MAPENDEKEZO, CHANGAMOTO NA MCHANGO WA MATOKEO YA UTAFITI -----	101
5.1 Utangulizi-----	101
5.2 Muhtasari wa Sura-----	101
5.3 Matokeo ya Utafiti-----	102
5.4 Mapendekezo ya Utafiti -----	105
5.5 Changamoto za Utafiti -----	106
5.6 Mchango wa Matokeo ya Utafiti -----	106
5.7 Hitimisho-----	107
MAREJELEO -----	108
VIAMBATISHO -----	112
Kiambatisho A: Barua ya NACOSTI-----	112
Kiambatisho B: Barua ya Idhinisho-----	113
Kiambatisho C: Hojaji kwa Wanafunzi -----	114
Kiambatisho D: Hojaji kwa Walimu -----	117

ORODHA YA MICHORO

Mchoro 4.1: Mada za fasihi simulizi -----	82
Mchoro 4.2: Sehemu za karatasi ya tatu -----	83
Mchoro 4.3: Idadi ya tanzu za fasihi simulizi-----	86
Mchoro 4.4: Kiwango cha wanafunzi -----	88
Mchoro 4.5: Walimu kupata Utata-----	90
Mchoro 4.6: Mvuto wa somo-----	92
Mchoro 4.7: Wanafunzi wahusishwe -----	94
Mchoro 4.8: Vitabu vya Kiswahili-----	96
Mchoro 4.9: Mbinu za ziada -----	97

ORODHA YA JEDWALI

Jedwali 2.1: Uainishaji; Kiswahili Kitukuzwe (uk 15) -----	30
Jedwali 2.2: Uainishaji; Chemchemi za Kiswahili -----	33
Jedwali 2.3: Uainishaji; Johari ya Kiswahili -----	36
Jedwali 2.4: Tanzu Kuu zenye Utata. -----	41
Jedwali 2.5: Chemchemi za Kiswahili vijitanzu vya maigizo -----	42
Jedwali 2.6: Miviga, Johari ya Kiswahili -----	46
Jedwali 2.7: Ulumbi, Chemchemi za Kiswahili -----	47
Jedwali 2.8: Ulumbi, Kiswahili Kitukuzwe -----	48
Jedwali 2.9: Soga, Johari -----	50
Jedwali 2.10: Soga, Chemchemi za Kiswahili -----	50
Jedwali 3.1: Mwingiliano tanzu wa Embalu na Mwakakongwa-----	78
Jedwali 4.1: Mielekeo ya fasihi simulizi-----	84
Jedwali 4.2: Utaratibu wa kufundisha fasihi simulizi-----	85
Jedwali 4.3: Matokeo ya karatasi ya 102/3 tangu 2012 – 2019-----	91
Jedwali 4.4: Mielekeo ya Fasihi Simulizi-----	93
Jedwali 4.5: Fasihi simulizi na mtandao -----	99

ISTILAH MUHIMU

Embalu : Tohara miongoni mwa Babukusu.

Mwaka kongwa : Sherehe za kuaga na kukaribisha mwaka miongoni mwa Wamakunduchi.

Mwingilianotanzu : Kuchanganyikana kwa matawi ya fasihi simulizi wakati wa utendaji.

Wamakunduchi : Ni lahaja ya Kiswahili pia huitwa Kihadimu.

ORODHA YA VIFUPISHO

EAEP	East African Educational Publishers.
(i + 1)	i ni maarifa yaliyopo sasa na 1 ni maarifa ya kiwango kinachofuatia cha Ujifunzaji.
JKF	Jomo Kenyatta Foundation.
K.I.C.D	Kenya Institute of Curriculum Development/ Taasisi ya kukuza
K.I.E	Kenya Institute of Education.
KLB	Kenya Literature Bureau
M.O.E	Ministry of Education.
MOEHRD	Ministry of Education and Human Resource Development.
MTVC	Ministerial Textbook Vetting Committee.
NACOSTI	National Commission for Science Technology and Innovation.

IKISIRI

Utafiti huu unahusu tathmini ya uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika vitabu vilivyoteuliwa kufunza fasihi simulizi ya Kiswahili kwa walimu na wanafunzi katika Shule za Upili Kenya, Kaunti ya Makueni. Utafiti ulilenga kuonyesha ukinzano wa idadi ya tanzu na vijitanzu na matatizo yanayokumba wanafunzi na walimu katika uainishaji wa fasihi simulizi. Masuala matatu yalilengwa katika utafiti huu: kubainisha tofauti katika uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika vitabu vilivyoidhinishwa, kubainisha vigezo vilivyotumiwa na kupendekeza suluhisho kwa utata unaotokana na tofauti hizi za uainishaji. Nadharia mbili zilitumiwa: ya Tanzu na ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili (Second Language Learning and Acquisition) iliyoasisiwa na Krashen (1982) ambapo haipotesia ya mchakato (Input hypothesis) zilitumiwa kufanikisha malengo ya utafiti huu. Haipotesia hii ilihusu sheria katika upokeaji wa lugha, kusonga kutoka kwa dhana rahisi hadi ngumu na uelewa wa maarifa kutoka $(i+1)$ ambapo i ni maarifa yaliyopo tayari na 1 ni maarifa yanayopatikana baadaye kupitia ujifunzaji. Nadharia ya Tanzu ilijikita kwa maswali je, tanzu zipo? Je, kuna idadi mahsusi ya tanzu? na Je, tanzu zinajisimamia au zinaingiliana? Nadharia hii ililenga uainishaji wa tanzu na vigezo vya uainishaji. Uteuzi wa kimakusudi ulitumiwa kuteua vitabu vilivyoidhinishwa na taasisi ya kukuza mitaala vya kufundishia fasihi simulizi kwa shule za upili, vitabu hivi viliwapa watafiti data ya kimsingi (maktabani) ilhali data endelevi (nyanjani) ilitokana na wanafunzi na walimu. Shule nne za upili ziliteuliwa ambapo wanafunzi ishirini wa kidato cha nne walihojiwa. Aidha, walimu wawili wa Kiswahili katika kila shule waliteuliwa na kuhojiwa. Muundo wa utafiti huu ni wa kimaelezo. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa mtindo wa kimaelezo na kuwasilishwa kwa maelezo fafanuzi na majedwali. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa vitabu tofauti vilivyoidhinishwa kufundishia fasihi simulizi kwa shule za upili vilikuwa na uainishaji unaotofautiana wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Baadhi ya vitabu vina tanzu nne, vingine tano na vingine sita. Pamoja na hayo, utafiti ulibaini kuwa uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi unategemea vigezo na misingi mbalimbali inayofuatwa na wataalamu katika kuandika matini za fasihi simulizi kama vile; muundo, maudhui, wakati, mtindo, wahusika na kadhalika. Ilibainika kuwa, ni kwa sababu hii kunatokea utata katika vitabu vilivyoidhinishwa. Kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, iwapo mada zitawasilishwa kwenye vifaa kwa njia isiyo wazi basi kutakuwa na changamoto kwa wasomaji. Aidha, kupitia hojaji, wasailiwa walikiri kuwa kuna utata katika ufundishaji na usomaji wa fasihi simulizi kutokana na hali hii. Hivyo basi, mtafiti alipendekeza kuwa, mada za fasihi simulizi zinastahili kuratibiwa upya ili ziwafae wanafunzi na walimu katika shule za upili. Utafiti huu ni wa manufaa kwa watafiti, wahakiki, waandishi wa vitabu vya fasihi simulizi, walimu na wanafunzi wa Shule za Upili na waratibu wa mitaala.

ABSTRACT

This study evaluated the classifications of oral literature genres in textbooks approved to teach Kiswahili Oral Literature for teachers and learners in secondary schools in Kenya, Makueni County. The aim of the research was to identify the different classifications of oral literature genres in the approved textbooks and the challenges faced by students and teachers from the different classifications. The research objectives were: to distinguish the difference in classification of oral literature genres as presented in the approved textbooks, to identify the basis and characteristics used in classification and to show the solutions to problems of different classifications of oral literature in approved oral literature genres. Two theories were used: Genre Theory and Krashen's Theory of Second Language Learning and Acquisition (1982). The first theory was about classification of genres and the characteristics of classification. It aimed at answering these questions: Are there genres? Is there a specified number of genres? Are genres independent or inter – dependent? The second theory utilized input hypothesis. This was about rules in language acquisition, moving from simple to complex knowledge and comprehension of input to move from (i + 1). Here, i was current level of knowledge and 1 was knowledge acquired later through learning. The theory guided the researchers in attaining the third objective. Purposive sampling was used to choose approved textbooks by the Kenya Institute of Curriculum Development (KICD), used in the teaching of Kiswahili Literature in Secondary Schools. These books gave the researchers primary data from oral literature sections while secondary data was collected from questionnaire responses from students and teachers. Four secondary schools were selected where twenty form four students from each school were identified to fill questionnaires. Two Kiswahili teachers were also picked from each school. Questionnaires aided in collection of secondary data. Qualitative research design was utilized. Data was analysed using qualitative analysis method then presented in tables and by descriptive method. The findings of this research are that, different books approved for teaching Kiswahili oral literature for secondary schools have different classification of the genres. Some have four genres; some five while others six because of different factors used by the experts and writers of these books. Some of the factors include; structure, theme, the time, style, characters among others. These differences results in understanding challenges among teachers and learners. The researcher therefore proposes that the genres of Kiswahili oral literature should be reclassified properly for the sake of the learners and teachers in secondary schools. This research will be beneficial to researchers, critics, oral literature authors, Secondary School students and teachers and curriculum developers.

SURA YA KWANZA

1.1 Utangulizi

Katika sehemu hii usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti zilishughulikiwa.

1.2 Usuli wa Mada

Kwa mujibu wa Mngaruthi (2008) fasihi simulizi ni aina ya sanaa inayowasilishwa kwa ubunifu kupitia lugha ambayo haijaandikwa. Hata hivyo imepata kuhifadhiwa kwa njia mbalimbali isipotee, baadhi ya njia hizo ni; maandishi, kanda za sauti, picha au tarakilishi. Anazidi kueleza kuwa kuainisha ni kupanga katika aina au makundi. Upangaji huu sio wa kiholela bali hufuata misingi au vigezo maalum.

Kwa mujibu wa Odeo (2006), fasihi simulizi imejidhihirisha kama sehemu mahsusi na muhimu kufuatia mapitio ya mitaala mwaka 2002 katika elimu ya shule za upili. Fasihi simulizi imepewa nafasi katika elimu na kutiliwa maanani kama sehemu ya Somo la Kiswahili.

Kulingana na Etyang (1987), kabla ya uhuru, wakoloni walijaribu kutumia fasihi yao huku wakikandamiza ile ya Waafrika. Waafrika nao baada ya uhuru, wakatia juhudi wafuate misingi yao wenyewe. Etyang amezidi kueleza, mwaka wa 1968, wahadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi walipendekeza kufundishwa kwa fasihi ambayo inalingana na mandhari ya Afrika. Mwaka wa 1974 walimu wa shule za upili walionelea kuwa silabasi ya fasihi ilihitaji kuangaziwa upya ili ioane na jamii ya Kenya na Afrika.

Katika mkutano uliofanyika katika Shule ya Upili ya Nairobi 1974, ilikubaliwa kuwa kamati iundwe ya kitaifa ili kutayarisha vifaa vya shule na kuanzisha maktaba ya vifaa vya fasihi simulizi.

Etyang aliongeza kuwa, wakati silabasi ya fasihi iliibuliwa 1980 na kutahiniwa mara ya kwanza 1982, mjadala uliibuka kuwa nchi haikuwa na walimu waliohitimu na pia hakukuwa na vitabu vya kutosha.

Kiai & Mokuu (2013), wanajadili kuwa uchaguzi wa vitabu mwaka wa 2002 ulihusisha mapitio ya mitaala tangu kuibuliwa kwa sera ya uchapishaji, ununuzi na usambazaji wakirejelea ripoti ya ushirikiano wa pamoja (Ministry of Education, 1998). Wanaonyesha kuwa vitabu vilivyosheheni kwenye soko ni vya mashirika ya uchapishaji ya Kenya Literature Bureau (KLB) na Jomo Kenyatta Foundation (JKF) - vikiwa na zaidi ya asilimia tisini ya vitabu vilivyokuwepo. Mwaka wa 1998, Chama cha Wachapishaji wa Kenya, jamii ya wafadhili na Kenya Institute of Education (KIE), ambayo sasa ni KICD zilijadiliana na kuibua sera ya vitabu vya kusoma.

Fasihi simulizi inafunzwa kwenye shule zote za upili humu nchini Kenya chini ya somo la Kiswahili; hutahiniwa katika mtihani wa Kitaifa wa Shule za Sekondari (KCSE) karatasi ya tatu. Sehemu hii ya fasihi simulizi huwa na alama ishirini na inaweza kuwa swali la lazima au isiwe.

Watafiti hawajashughulikia kwa kina athari za utata wa uainishaji wa tanzu kwa wapokezi wa fasihi simulizi. Kulikuwa na haja ya kuangazia athari za uainishaji unaotofautiana na kubadilikabadilika ili vijitanzu vya fasihi simulizi viweze kueleweka vyema kwa wanaojifunza na kusoma kazi zilizoandikwa za fasihi simulizi.

Vitabu mbalimbali vya marejeleo vimekubaliwa kufundishia fasihi na taasisi ya kukuza mitaala mwaka wa 2009 vya somo la Kiswahili na vingine ni vya kiada. Vitabu hivyo vimeainisha tanzu za fasihi simulizi kwa njia tofauti kufuatia misingi tofauti.

Vitabu vifuatavyo vimeidhinishwa kutumiwa kufundisha Kiswahili kwa shule za upili nchini Kenya; *Chemchemi za Kiswahili* kilichochapishwa na Longhorn, *Johari ya Kiswahili* kilichochapishwa na East Africa Educational Publishers (EAEP), *Kiswahili Fasaha* kilichochapishwa na Oxford, *Darubini ya Kiswahili* kilichochapishwa na Phoenix, *Hazina ya Kiswahili* kilichochapishwa na Longman, *Kiswahili Kitukuzwe* miongoni mwa vinginevyo. Vitabu hivi vina sehemu ya fasihi simulizi ambayo hufunzwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne katika shule za upili. Utafiti huu ulilenga vitabu vinne vya kidato cha nne vilivyoidhinishwa ambavyo ni; *Chemchemi za Kiswahili*, *Kiswahili Kitukuzwe*, *Kiswahili Fasaha* na *Johari ya Kiswahili*. Kazi hizi za fasihi simulizi huwa chini ya mada ya kusikiliza na kuzungumza.

1.3 Suala la Utafiti

Tafiti zimefanywa katika somo la fasihi simulizi na zingine kuhusu uwasilishaji kwenye vitabu vya kusoma. Tafiti zingine zimelenga upokezi wa wanafunzi na athari za silabasi pana. Baadhi ya tafiti zilizoangazia mambo haya ni: Etyang (1987), Namanya (2015) miongoni mwa wengine. Hakuna kati ya tafiti za awali iliyochunguza uwasilishaji wa tanzu za fasihi simulizi kwenye vitabu vilivyokubaliwa kufundishia shule za upili.

Fasihi simulizi ni muhimu katika shule za upili kwa sababu hutahiniwa katika mitihani ya kitaifa kwenye somo la Kiswahili katika karatasi ya tatu. Hivyo basi, sehemu zote za somo hili zinastahili kutiliwa maanani na kukuzwa ipasavyo.

Dhana zinazotangulizwa kwa mwanafunzi wa kidato cha kwanza zinastahili kuwa rahisi na kujengeka kwa zile ngumu kadri mwanafunzi anavyoingia kwenye ngazi za juu. Vitabu hivi vilivyoidhinishwa havizingatii haya kwani vitabu tofauti vimewasilisha uainishaji tofauti na vimeweza kupelekea ukosefu wa usawa. Tofauti hizi za uwasilishaji wa tanzu zimebainika kwenye vitabu vya kufundishia somo la Kiswahili.

Somo hili lina uainishaji wa tanzu unaofuatwa na waandishi wa vitabu mbalimbali vya kusoma. Utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo uainishaji wa fasihi simulizi unatofautiana kwenye vitabu vya kufundishia na iwapo uwasilishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu hutatiza wasomaji ambao ni wanafunzi na walimu. Hivyo basi, utafiti huu ulitathmini hilo kwa kuangazia vitabu vilivyoidhinishwa na taasisi ya kukuza mitaala.

Vitabu vilivyolengwa katika utafiti huu ni kama: Chemchemi za Kiswahili kilichoainisha tanzu kuu tano: (Hadithi, Semi, Ushairi, Maigizo na Mazungumzo) kwa mujibu wa (Wamitila, 2003a). Kiswahili Kitukuzwe nacho kimeainisha tanzu sita: (Mazungumzo, Maigizo, Hadithi, Semi, Ushairi na Ngomezi) kwa mujibu wa (Kenya Literature Bureau, 2009). Hivyo basi utafiti huu ulitathmini uainishaji ulivyo wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi kwenye vitabu vilivyokubaliwa na taasisi ya kukuza mitaala kwa wanafunzi na walimu kwenye shule za upili nchini Kenya.

1.4 Malengo ya Utafiti

1. Kuonyesha tofauti iliyopo katika uainishaji wa tanzu na vijitanzu kwenye vitabu tofauti vilivyoidhinishwa kufundisha fasihi simulizi.
2. Kubainisha vigezo ambavyo uainishaji wa tanzu na vijitanzu unafuata.
3. Kupendekeza suluhisho kwa matatizo ya uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu kwa wanafunzi na walimu.

1.5 Maswali ya Utafiti

1. Ni tofauti zipi ambazo zipo katika uainishaji wa tanzu na vijitanzu katika vitabu tofauti vilivyoidhinishwa kufundisha fasihi simulizi?
2. Je, uainishaji wa tanzu na vijitanzu unafuata vigezo gani?
3. Je, suluhisho kwa matatizo ya uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu ni zipi kwa wanafunzi na walimu?

1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Kuna sehemu katika fasihi simulizi ambazo uwasilishaji wake kwenye vitabu vya kufundisha hutofautiana. Sehemu hizo zimeweza kuibua hali ya kuchanganyikiwa kwa wanafunzi. Iwapo uainishaji wa tanzu sio wazi kwa mwanafunzi au hata mwalimu, basi huenda ikawa vigumu kusema au kujibu swali lolote kuhusu uainishaji darasani. Kutokana na hali hii, mtafiti alichunguza uainishaji tofauti wa tanzu kwenye vitabu vilivyoidhinishwa kufundisha fasihi simulizi.

Baadhi ya waandishi wamejadili katika kazi zao upungufu uliopo katika vitabu vya fasihi simulizi. Kobia (2006) katika Njogu, Momanyi & Mathooko (2006) wanaeleza udhaifu wa vitabu vilivyochapishwa na kueleza kuwa baadhi ya vitabu vimechanganya tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi. Vitabu vilivyoshughulikia fasihi simulizi hutaja tu vipera mbalimbali bila maelezo ya kina.

Vitabu vingine ni sahili na havijafanyiwa marekebisho ya matoleo. Kitabu kimoja kimetoa maelezo tofauti na kingine kuhusu kipera kimoja, hivyo basi ni muhimu kushughulikia tatizo hili.

Ili kujenga uaminifu na maarifa ya wanafunzi au hata walimu ni muhimu vifaa vyote vinavyokubaliwa kutumika shuleni hasa vya kufundishia viwe na uwazi na uwasilishaji usioleta ukinzano. Utafiti huu ulitoa mapendekezo yatakayoongoza tafiti na uandishi wa mada za uainishaji wa fasihi simulizi. Aidha, wakuza mitaala watapata mwanga kuhusu vitabu vinavyofaa kuteuliwa kufundishia Kiswahili kwa shule za upili. Isitoshe, utafiti huu umetoa mwanga kwa waratibu wa mitaala kuhusu uwasilishaji wa mada za fasihi simulizi hasa uainishaji kwenye vitabu vya wanafunzi.

Zaidi ya hayo, utafiti huu umeelekeza walimu kwa baadhi ya vyanzo vya changamoto za uainishaji wa tanzu na vijitanzu na kupendekeza njia mwafaka za kupitisha mafunzo ya uainishaji wa fasihi simulizi.

1.7 Upeo na Mipaka

Fasihi simulizi huangazia vipengele mbalimbali kama vile; uainishaji wa tanzu na vijitanzu, sifa na umuhimu wa tanzu na vijitanzu mbalimbali, mifano ya vijitanzu tofauti tofauti na kadhalika. Utafiti huu, haukushughulikia fasihi simulizi kwa ujumla ila ulijikita katika uainishaji tofautitofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika vitabu vilivyoidhinishwa kufundishia fasihi simulizi.

Vitabu vinavyoangazia fasihi simulizi ni vingi na hulenga viwango tofauti tofauti vya elimu. Utafiti huu ulilenga tu vile ambavyo vimeidhinishwa na taasisi ya kukuza mitaala kufundishia fasihi simulizi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya na wala si viwango vingine.

Vitabu vinne vilivyo dhinishwa viliteuliwa kutumika katika utafiti huu. Kutokana na utafiti wa awali, vitabu hivi vipo katika shule nne zilizoteuliwa. Vitabu hivi ni; *Chemchemi za Kiswahili, Kiswahili Fasaha, Johari ya Kiswahili na Kiswahili Kitukuzwe*. Ujumbe kuhusu tanzu na vijitanzu kwenye vitabu hivyo ulichanganuliwa ili kufikia malengo ya mtafiti.

Utafiti haukuzingatia stadi zote nne za somo la kiswahili ila ulilenga sehemu inayoangazia stadi ya kusikiliza na kuzungumza pekee kwenye vitabu vilivyoteuliwa. Sehemu hii huangazia maamkizi, ufahamu wa kusikiliza na kudadisi. Mada za fasihi simulizi huwa katika kijisehemu cha kusikiliza na kudadisi. Kwa sababu hii, utafiti huu ulilenga tu kijisehemu hicho mahsusi kwani ndicho kinajadili uwasilishaji wa fasihi simulizi na vipera mbalimbali.

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na nyanjani. Ujumbe wa vitabu kuhusu uainishaji ulijenga data ya maktabani ilhali data ya nyanjani ilitokana na wasailiwa waliojaza hojaji. Aina hizi mbili zilitumiwa kwa sababu data ya maktabani iliafikia lengo la kwanza na la pili kuhusu uainishaji tofauti na vigezo vya uainishaji. Data ya nyanjani ilitumiwa kuendeleza lengo la tatu la suluhisho kwa matatizo ya uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

Wanafunzi na walimu walichaguliwa kujaza hojaji iliyompa mtafiti data endezezi. Shule nne zilichaguliwa katika kaunti ya Makeni kwani kutokana na utafiti wa awali shule hizi nne zilikuwa na vitabu vilivyoorodheshwa kutumika kwa utafiti huu. Zaidi ya hayo, mtafiti hakuweza kutafitia wanafunzi wote shuleni na shule zote kwenye kaunti hiyo. Ilichukuliwa kuwa wanafunzi na walimu hao walikuwa kiwakilishi bora cha eneo hilo.

Wasailiwa hawa walijibu maswali ya hojaji ambayo yalielezewa katika sehemu ya viambatisho. Hojaji ilihusisha maswali wazi na funge ili mtafiti asibane habari na pia aweze kupata ujumbe mahsusi kuhusu uainishaji wa fasihi simulizi.

Katika shule hizo nne, wanafunzi ishirini wa kidato cha nne kwa kila shule walirejelewa kwani wameipokea silabasi ya fasihi simulizi tangu kidato cha kwanza. Walimu wa Kiswahili kwa kila shule pia walichaguliwa kujaza hojaji.

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Sehemu hii iligawika katika misingi mitatu tofauti; kwanza tafiti zilizofanywa kuhusu vifaa na mbinu za kufundishia, pili kuhusu vitabu vilivyoandikwa na vyenye maelezo kuhusu fasihi simulizi na uainishaji na mwisho tafiti mahsusi za fasihi simulizi.

1.8.1 Tafiti kuhusu Vifaa na Mbinu za Kufundishia

Tafiti hizi zilizofanywa zililenga matumizi ya vifaa na kuonyesha changamoto katika mchakato wa kufundisha wanafunzi na udhaifu wa mbinu hizo.

Etyang (1987) alitafiti kuhusu mbinu za kufundisha na kusoma fasihi simulizi. Alitumia sampuli yakinifu kuteua sampuli, data ilikusanywa kwa kutumia hojaji na kuchanganuliwa kwa takwimu elezi. Utafiti wake ulionyesha kuwa ujuzi wa walimu kuhusu mbinu za kufundisha ulikuwa finyu na makala yaliyochapishwa kama vile vitabu yalitegemewa sana huku mbinu zingine za ziada zikipuuzwa. Pendekezo lake lilikuwa kwa vyuo vya mafunzo viangazie upya silabasi ili wahakikishe walimu wamepokea na kuelewa mbinu za kufundisha fasihi simulizi. Utafiti wake utasaidia kuelewa jinsi fasihi simulizi inavyofundishwa na pia nafasi ya vitabu kama vifaa vya kufundishia.

Utafiti wa sasa unalenga kuendeleza utafiti wa Etyang kuhusu mbinu wanazotumia walimu kufundisha fasihi simulizi hasa matumizi ya vitabu vilivyoidhinishwa. Aidha, anakubaliana na Saunders (1974) naye anadai kuwa vifaa vyovyote vya kufundishia vinastahili kuteuliwa kutokana na ufanisi na sio bei yake. Anasisitiza kuwa vifaa vinavyoteuliwa viwe ni vile vinawasilisha ujumbe kwa njia isiyo changamano. Utafiti huu uliwezesha mtafiti kuelewa kwa kina mikakati inayowekwa ya kuchagua vitabu vya kufundisha na iwapo baadhi ya vitabu hivyo vilielekeza wasomi ipasavyo.

Lorna (2012) alitafitia namna ambavyo walimu wanapokea mbinu unganishi ya kufundisha fasihi simulizi ya somo la Kiingereza katika shule za upili ambapo alieleza changamoto zinazokumba walimu waliotumia mbinu hii. Anawanukuu Akivaga & Odaga (1985) walioeleza kuhusu jaribio la kuratibu silabasi ya fasihi simulizi tangu 1974 katika kongamano la walimu wa fasihi simulizi katika shule ya upili ya Nairobi. Aidha, aliwarejelea Kabira & Mutahi (1988) wanaosisitiza kuwa, ili kuelewa jamii ni muhimu kuangazia fasihi yake iliyoandikwa na ya kusimuliwa. Lorna anadai kuwa mwaka 1982 somo la fasihi simulizi ya Kiingereza lilihusishwa katika silabasi ya Kenya na muungano ukafanywa katika mfumo wa 8-4-4. Kuleta pamoja somo la fasihi na somo la Kiingereza kulizua utata kuhusu muda usiotosha uliotengwa. Tafiti hizi zote ni za fasihi simulizi ila utafiti huu ni wa Kiingereza na ni tofauti kwani ulijikita kuchunguza upokezi wa walimu kuhusu mbinu unganishi ya kufundisha fasihi simulizi na changamoto zilizopo. Utafiti wa Lorna ulifaa katika kuelewa changamoto zilizokumba ufundishaji na usomaji wa fasihi simulizi ya Kiswahili ilipoanzishwa na nafasi finyu ya fasihi ya Kiswahili kwenye shule za upili.

Mucai (2013) anaonyesha namna vifaa vya kielimu na matumizi yake vilivyoathiri matokeo ya mitihani ya wanafunzi kwa shule za upili. Kazi yake ilianguzia ufanisi wa wanafunzi na walimu katika kutumia vitabu vya kufundishia. Alitumia hojaji kukusanya data na nadharia ya mfumo wa mbinu katika ufanisi wa shirika. Pia alionyesha kuwa ufanisi wa shirika unapimwa na uwezo wake wa kupata vifaa au raslimali na kuzitumia katika kufikia malengo ya shirika. Akimnukuu Oni (1995) anaeleza kuwa elimu ya Shule za Upili kama yalivyo mashirika mengine, hupokea mchango kutoka kwa mazingira na kuupitisha kwa mchakato na kutoa matokeo kwa mazingira hayo. Utafiti wake ulikuwa tofauti na huu kwani alijikita katika kuwepo kwa vifaa vya kufundishia. Utafiti huu uliangazia vitabu vilivyokubaliwa na jinsi viliwasilisha dhana za uainishaji wa fasihi simulizi. Utafiti wake ulisaidia watafiti katika kuelewa ufanisi wa vitabu vya kufundisha kwa wanafunzi na walimu na athari kwa matokeo ya wanafunzi.

Nafula (2014) alitafitia changamoto za kufundisha silabasi pana ya Kiswahili katika shule za upili na alilenga kuchunguza jinsi silabasi pana ya Kiswahili inadumishwa, wakati unaotengewa somo hili na changamoto za kufundisha silabasi pana. Alitumikiza nadharia ya Krashen (1985) ya mchakato na matokeo katika upokezi wa lugha ya pili. Alitumia hojaji na mahojiano.

Utafiti wake ulionyesha kuwa walimu hupata changamoto kadhaa kama vile, wakati usiotosha kufundishia na upungufu wa maarifa katika silabasi pana. Nafula alipendekeza serikali iwaajiri walimu wengi na waratibu wa mitaala waangazie upya wakati uliotengewa somo la Kiswahili. Utafiti wake uliangazia changamoto za silabasi ya Kiswahili kwa jumla ilhali utafiti huu ulilenga uwasilishaji wa ujumbe ule ule kwa njia tofauti kwenye vitabu vilivyokubaliwa na waratibu wa mitaala.

1.8.2 Kazi Zilizandikwa kuhusu Fasihi Simulizi, Uainishaji na Uwasilishaji.

Vitabu vya waandishi tofauti wa fasihi simulizi vimeangazia dhana za uwasilishaji wa tanzu, ubora na udhaifu wa silabasi na mabadiliko ya idadi ya tanzu.

Bascom (1953) anajadili kuwa fasihi simulizi ni sehemu ya masuala ya kitamaduni na uhusishwa na utafiti wa desturi na tamaduni za watu. Fasihi simulizi uhusisha: hadithi, methali, simulizi, vitendawili, nyimbo, maleba, desturi na imani za jamii. Bascom alizidi kueleza kuwa, hizi zote ni sehemu muhimu za ethnografia na tamaduni yoyote ile. Kando na kuburudisha Fasihi simulizi ina umuhimu wa kuendeleza utamaduni, kukuza mitazamo na kuelimisha jamii. Mawazo ya Bascom ni tofauti na utafiti huu kwani alijikita katika ethnografia ya fasihi simulizi nao utafiti wa huu ulilenga kuendeleza somo la fasihi simulizi kwa kutathmini athari za uainishaji tofauti kwenye vitabu vilivyoidhinishwa.

Chandler (1997) anaeleza kuwa neno tanzu lina asili ya Kifaransa lenye maana ya aina au kiwango. Katika fasihi tanzu kuu ni: ushairi, nathari na maigizo, ambapo kila tanzu ina mgao zaidi chini yake. Utanzu wa mwananadharia mmoja waweza kuwa kijitanzu au tanzu kuu kwa mwingine. Mtindo, muundo, fomyula au maudhui yanaweza kuchukuliwa kama tanzu. Akinukuu Miller (1984) anapendekeza kuwa idadi ya tanzu katika jamii yoyote ile inategemea uchangamano na tofauti za jamii. Akinukuu Hodge, Robert & Kress (1988), anaeleza kuwa tanzu huwepo kulingana na msukumo na uamuzi wa kundi la jamii. Mawazo ya Chandler yalionyesha mwingiliano wa tanzu, hii ni tofauti na utafiti huu ambao kando na kuangalia misingi ya uainishaji tofauti ulijikita kuchunguza suluhisho kwa uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

Kwa mujibu wa Duff (2000), tanzu imekuwa kati ya dhana za kimsingi za nadharia za kifasihi tangu enzi za Aristotle. Maendeleo ya kisasa katika nadharia yameibua dhana mpya na changamano kwa misingi ya awali ya nadharia ya kiutanzu. Hii imepelekea tafsiri tofauti za tanzu na kuibuka kwa uainishaji mpya. Baadhi ya wananadharia wa kiutanzu wa karne ya ishirini ni kama: Vladamir, P., Bakhtin, M., Jauss, R. na Jacques, D. Mawazo yake Duff yalisaidia kuelewa kuhusu nadharia zenye ulinganifu na utafiti huu kuhusu uainishaji wa fasihi simulizi.

Kwa mujibu wa Kobia (2006) katika Njogu et al. (2006), fasihi simulizi katika mitaala ya elimu nchini Kenya imeangaziwa kuanzia shule ya msingi hadi vyuo vikuu. Baadhi ya malengo ya kufundisha Kiswahili kwa mujibu wa silabasi iliyotolewa na Kenya Institute of Education (2002) ni kama vile: kudadisi, kutambua, kutathmini na kustawisha aina na tanzu tofauti za lugha na fasihi kwa Kiswahili. Kuna vipera ambavyo vilikuwa vimepuuzwa katika mtaala wa elimu kama vile; ulumbi, sogu, mawaidha, mighani, ngomezi, misimu na ambavyo vilishughulikiwa baadaye katika silabasi ya mwaka 2002. Udhaifu wa vitabu vilivyochapishwa vya fasihi simulizi ni kama kuchanganya tanzu za fasihi simulizi. Kazi hii ilichangia katika kuelewa mabadiliko ambayo yamekuwepo kuhusu uwasilishaji wa tanzu za fasihi simulizi.

Kwa mujibu wa Propp (1968), utata wa uainishaji wa hadithi za kifantasia na hadithi nyinginezo ni bayana. Alieleza kuwa, tanzu huingiliana na kuhusiana kama ambavyo misingi ya fasihi huingiliana. Uainishaji sahihi unaweza kufikiwa kwa njia tatu:

Kuzingatia aina tofauti za dhana, kuwepo au kutokuwepo kwa dhana na kuhusiana kwa dhana za kipekee. Mawazo ya Propp yalisaidia mtafiti kuelewa mwingiliano wa tanzu na ugumu wa uainishaji.

Kulingana na Vansina (1985), tanzu ni dhana inayohusisha mtazamo wa umbo na matini maalum. Ujumbe unawasilishwa katika tanzu unapowekwa kwa muundo wa ndani au umbo. Zaidi ya hilo, maelezo ya tanzu yanahusiana na kanuni zilizopo na zinatambulishwa kwa tamaduni tofauti na kupewa majina. Wataalam wa sanaa simulizi wamejaribu kujenga kategoria za kifasihi ambazo zimekuwa halali kwa jamii jumla.

Hii ni muhimu hasa kwa wasomi katika tafiti linganishi. Vansina anamrejelea Finnegan (1970) aliyeanisha ujumbe katika ushairi, nathari na mbinu maalum kama lugha ya ngoma na maonyesho. Finnegan aligawa zaidi ushairi kwa makundi saba na nathari kwa makundi manne (hadithi, vitendawili, misemo na masimulizi). Mgao huu wa Finnegan haufuatwi na jamii zote; mfano: kwa watu wa Burundi, misemo na hadithi ni tanzu sawa. Vansina alieleza kuwa sio rahisi kupata uainishaji sawia kwa tamaduni zote. Kazi hii ilichangia utafiti huu kwa kuangazia dhana za jamii tofauti kuwasilisha tanzu kwa njia tofauti. Maarifa haya yalielekeza utafiti kwa kuelewa historia na kategoria za fasihi simulizi.

Wanjala (2011) anaeleza kuwa, jamii tofauti huweka vipera vya fasihi simulizi kwenye makundi mbalimbali kufuatia misingi tofauti. Kwa mfano, Wakipsingis wameainisha: methali (*Kalewenoik*), vitendawili (*tangoch*), nyimbo (*tienwogik*), mawaidha (*katigonik*), mazimwi (*chemosit*) na hadithi (*atindonik*).

Wakamba wameainisha: methali (*nthimo*), vitendawili (*ndae*), nyimbo (*mbathi*), mawaidha (*utao*) na mazimwi (*maimu*). Fasihi simulizi imeweza kuainishwa kwa njia nne kuu ambazo ni: hadithi, maigizo, semi bainifu na ushairi.

Uainishaji huu umetegemea sifa mbili kuu; kuchunguza fani katika utanzu husika na kuchunguza maudhui katika utanzu husika. Kuna vijitanzu chini ya kila utanzu ambavyo vinaainishwa kwa mujibu wa utendakazi, ujumbe, mtindo na muundo wake.

Ugumu wa kuainisha upo kwa sababu ya tofauti za kijamii, hali ya kubadilika kwa unyumbufu wa tanzu mbalimbali, mwingiliano na ukuruba mkubwa kati ya tanzu tofauti. Kutokana na maandishi haya, uainishaji wa tanzu upo na tanzu zina sifa tofauti kutegemea jamii husika. Utafiti huu ulidhamiria kutumia ujumbe wa mwandishi huyu ili kuelewa misingi mbalimbali ya uainishaji inayopelekea vitabu tofauti kuwa na uainishaji unaotofautiana wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

1.8.3 Tafiti kuhusu Fasihi Simulizi

Tafiti zifuatazo zilifanywa na kulenga fasihi simulizi. Ziliongoza utafiti kwa kuweka dhana mbalimbali wazi kuhusu ugumu wa uainishaji wa fasihi simulizi, nafasi ya somo hili na mchango wa somo.

Kwa mujibu wa Murimi, Obuchi & Kandagor (2016) dhana ya mwingiliano tanzu imeathiri uainishaji na kuleta utata wa idadi ya tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Wamebaini kuwa tatizo hili lilichangiwa na historia ya uainishaji wa ulimwengu ambayo iliegemea mtazamo wa Ki-Aristotle. Walionyesha kuwa, wataalamu waliobainisha tanzu za fasihi walikumbwa na utata wa idadi ya tanzu kutokana na sifa zenye ukuruba za tanzu hizo. Wanamnukuu Muiruri (2006) kuonyesha uainishaji wa tanzu. Utafiti huu ulimwezesha mtafiti kuelewa baadhi ya mambo yanayopelekea ugumu wa uainishaji wa tanzu.

Namanya (2015) anajadili kuhusu dhima ya misemo na nahau. Alilenga kuweka wazi sifa za fasihi na dhima na malengo ya nahau na misemo. Utafiti uliongozwa na nadharia ya uamilifu. Namanya alitumikiza mbinu ya mahojiano.

Utafiti wake unaunga mkono dhana kuwa misemo na nahau ni vijitanzu vya fasihi simulizi vyenye sifa bainifu. Utafiti wake ulisaidia kuelewa kuwa vipera vya fasihi simulizi vina sifa bainifu.

1.9 Misingi ya Kinadharia

Nadharia ni miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote (Wafula & Kimani, 2007). Hivyo basi nadharia ni maelezo yaliyopangwa kutekeleza jambo fulani.

Nadharia mbili zilitumika katika utafiti huu: Nadharia ya Tanzu na ya Ujifunzaji na Upokeaji wa lugha ya pili (Second Language Learning and Acquisition) iliyoasisiwa na Krashen (1982). Nadharia ya kwanza ilikuwa ya fasihi simulizi na ililenga uainishaji wa tanzu. Nadharia ya kwanza ilikuwa na upungufu kwani haikulenga suala la ufundishaji wa fasihi simulizi. Kwa sababu sio ya lugha, upungufu huu ulijalizwa na nadharia ya pili ya lugha ambayo ililenga ufundishaji na ilikopa kutokana na mawazo jumla ya Krashen kuhusu utayarishaji wa vifaa na njia bora za kuwasilisha matini kwa wanafunzi na walimu.

1.9.1 Nadharia ya Tanzu

Chandler (1997) anaeleza kuwa neno tanzu linatokana na neno la Kifaransa `aina` au `jamii`. Anaongeza kuwa, tangu kipindi cha urasimi kazi za kifasihi zimeainishwa katika vitengo ambavyo awali vilikuwa katika makundi matatu makuu: Ushairi, nathari na maigizo. Makundi haya yaligawika zaidi, kwa mfano, maigizo yakawa na tanzia na vichekesho.

Mwasisi wa nadharia ya Utanzu ni Boas (1940) ambaye alitumia nadharia hii katika Anthropolojia alipokuwa akichunguza lugha asilia ya Marekani. Wengine walioiendeleza nadharia hii ni kama Dell Hymes na Bakhtin.

Nadharia ya Tanzu katika fasihi simulizi imeonyesha tanzu zilivyoundwa na vigezo vilivyofuatwa katika uundaji huo. Kwa mujibu wa Ben-Amos (1976) vigezo au misingi ya kugawa tanzu za fasihi simulizi katika makundi mbalimbali ni kama;

- a. Kupeana majina mbalimbali kufungamana na ujuzi wa wenyeji - majina kama mighani, visasili, methali, vitendawili na hurafa ni dhana zenye sifa zinazojitokeza mara kwa mara.
- b. Kulingalisha na kulinganua - sifa bainifu za utanzu mmoja zinaweza kujulikana na kutenganishwa na sifa za utanzu mwingine.
- c. Kwa kuchunguza mianzo na miisho ya tanzu mbalimbali - kwa mfano, baadhi ya tanzu zina mianzo dhahiri kama 'Kitendawili... Tega' au 'Hadithi, hadithi...Hadithi njoo...'. Kutokana na sifa kama hizi tanzu za fasihi simulizi zinaweza kubainika.
- d. Mtindo - masimulizi yana mitindo tofauti yakilinganishwa na nyimbo au mashairi simulizi ya kukaririwa.
- e. Dhamira - tanzu tofauti zinaweza kutumiwa kuwasilisha dhamira tofauti.
- f. Muundo - jinsi mawazo yanavyosukwa katika tamko yanategemea kaida zinazofuatwa katika utanzu unaohusika.

- g. Itikadi za jamii - muundo wa jamii kitabaka, kijinsia na kiumri unaathiri uainisho wa baadhi ya tanzu. Hata fanani wenyewe kulingana na weledi wao wanaweza kuwa kigezo cha kuainisha tanzu.
- h. Mahali na wakati – mahali pa kutambia au kuigizia utanzu unaweza kuashiria jinsi ya kuuainisha.

Vigezo hivyo vilivyotajwa, vinaonyesha uwezo mkubwa wa kuingiliana kwa tanzu za fasihi simulizi. Kwa mfano, mtindo wa kuwasilisha utanzu mmoja umeweza kufanana na utanzu mwingine.

Bordwell (1989) anaeleza kuwa kupanga kulikohamasishwa katika kutafsiri filamu kulihusishwa na dhana ya tanzu. Dhana hii ilihusisha matatizo matatu ya uainishaji;

1. Ufafanuzi wa tanzu kama kanuni (kuitofautisha na aina zingine).
2. Mfumo unaofafanua muundo wa tanzu (kubagua moja kutokana na nyingine).
3. Ufafanuzi wa tanzu moja.

Bordwell (1989) anaongeza kuwa hakuna uainishaji wa tanzu wenye mantiki uliowezekana.

Tanzu zilichukuliwa kuwa makundi hafifu ambayo hayakuweza kufafanuliwa kwa masharti ya kutosha au misingi bainifu. Zaidi ni kuwa, utanzu kwa misingi ya mwananadharia mmoja waweza kuwa kijitanzu kwa mwingine. Mbinu, mtindo, fomula au mandhari kwa mwananadharia mmoja yaweza kuchukuliwa kama tanzu na mwingine.

Kress (1988) anaeleza tanzu kuwa aina ya maandishi ambayo yaliibua umbo lake kutokana na muundo wa matukio ya kijamii yaliyorudiwarudiwa na yaliyo na washiriki wenye sifa na malengo. Kwa mujibu wa Stam (2000) ufafanuzi wa tanzu uliweza kutatiza. Anabainisha matatizo manne makuu ya kubainisha tanzu kwa mtazamo wa filamu;

1. Ugani - ufupi au urefu wa tanzu.
2. Ukawaida - kuwepo kwa dhana zilizotambuliwa awali kuhusu vigezo na aina ya tanzu.
3. Ufafanuzi wa kimonolithiki - kuainisha kipengele kana kwamba ni cha aina moja ya tanzu.
4. Kibiolojia - mtazamo wa kuwa tanzu hubadilika kupitia viwango mahsusi vya maisha.

Stam (2000) anazidi kuelezea kuwa tanzu ziliweza kuingiliana lakini njia bora zaidi ya kutumikiza tanzu ilikuwa ni kuichunguza kama raslimali ya majadiliano na trampolini ya ubunifu. Anaongeza kuwa, mashaka kadha ya kila wakati yaligubika nadharia ya Tanzu. Mashaka haya yaliibua maswali yafuatayo:

1. Je, tanzu zipo ulimwenguni au zimejengwa na wahakiki?
2. Kuna idadi mahsusi ya tanzu au tanzu hazina kikomo?
3. Tanzu ni dhana zisizo na kikomo kiwakati au zinadumu muda mfupi?
4. Tanzu ni tamaduni moja au zinaingiliana kati ya tamaduni tofauti?
5. Tanzu zinafaa kuwa elezi au funge?

Mihimili

Kutokana na mawazo ya wataalamu waliojadiliwa, utafiti huu uliongozwa na mihimili ifuatayo iliyoafiki malengo ya utafiti:

1. Tanzu zipo ulimwenguni na ni dhana zisizo na kikomo? Hivyo basi uainishaji wa tanzu umefanyika tangu enzi za urasimi. Kwa mfano, ushairi, nathari na maigizo. Mhimili huu ulitumiwa kuchunguza uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi kwenye vitabu vilivyoidhinishwa.

Uainishaji ulilinganishwa ulivyo kwenye vitabu vilivoidhinishwa kwa kuangazia idadi na uwasilishaji wa tanzu za fasihi simulizi.

2. Mfumo ambao hufafanua muundo wa tanzu ni upi? Mhimili huu ulitumiwa kuchunguza uainishaji wa tanzu ulifuata misingi au vigezo vipi? Tanzu ziliainishwa kwa msingi tofauti kwa mitazamo ya wataalamu mbalimbali? Misingi ya waandishi tofauti ililinganishwa na vigezo vya nadharia ya Tanzu.
3. Tanzu zimejisimamia kwa maana na sifa au zimeingiliana? Tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi vimeelezewa na wataalamu mbalimbali kwa misingi inayotofautiana. Mhimili huu ulitumiwa kuchunguza iwapo tanzu zimejisimamia au ni tegemezi. Aristotle aliona utanzu kama uliotengemaa naye Bakhtin aliuona utanzu kama ulioweza kunyambuliwa.

1.9.2 Nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili

Krashen (1982) anajadili nadharia hii kwa kuangazia haipotesia tano; Haipotesia ya tofauti ya ujifunzaji na usomaji (The Acquisition – Learning distinction), Haipotesia ya mpangilio asili (Natural order hypothesis), Haipotesia ya Monita (Monitor hypothesis), Haipotesia ya mchakato (The Input hypothesis) na Haipotesia ya uchuzaji (Affective filter hypothesis). Katika kazi yake anajadili jinsi mwanafunzi wa lugha ya pili alivyojifunza, kupokea na kuelewa lugha. Anazidi kueleza kuhusu jinsi ya kutahini wanafunzi wa lugha ya pili na jinsi vifaa na vitabu vya kusoma vina dosari katika kutayarisha mwanafunzi wa lugha ya pili kikamilifu.

Katika kazi yake pia alipendekeza kwa waandishi wa makala tofauti jinsi ya kupanga kazi ili ivutie kwa msomaji. Kutokana na haipotesia tano, utafiti huu ulilenga kutumikiza haipotesia ya mchakato (Input hypothesis).

Haipotesia ya Mchakato

Haipotesia hii ilionyesha kuwa mwanadamu hupokea lugha kwa njia moja tu ya kuelewa ujumbe au maarifa. Iliangazia jinsi ya kupokea lugha kufuatia mpangilio asili, yaani tunaweza kusonga kutoka kiwango kimoja cha uelewa wa lugha hadi kingine vipi? Tutasonga kutoka (i kuenda 1) vipi? (i) ni ujuzi/maarifa ya sasa na (1) ni kiwango kinachofuatia cha maarifa. Haipotesia hii ilihusiana na upokeaji zaidi kuliko kusoma, tunapokea kwa kuelewa lugha yenye muundo.

Mchakato lazima uwe na ($i+1$) ili uwe wenye manufaa kwa mpokeaji wa lugha. Ujuzi wa silabasi unajaribu kujumuisha ($i+1$), mwalimu na mwanafunzi huhisi kuwa lengo la somo ni kufundisha au kujizoeshia kipengele mahsusi cha kisarufi. Endapo muundo huu utaeleweka basi silabasi itaendelezwa kwenye ngazi inayofuatia au kiwango cha juu cha ujifunzaji.

Iwapo mawasiliano yanafaulu, mchakato wa ujifunzaji unapoeleweka na ni wa kutosha basi ($i+1$) itajitokeza moja kwa moja. Nadharia ya upokeaji wa lugha ya pili inajibu maswali manne kuwa, iwapo marekebisho ya makosa yatafanywa kwa njia zifuatazo basi kutakuwepo na ufanisi;

1. Marekebisho ya makosa yakifanyika humsaidia mwanafunzi kubadilisha fahamu zake za kiakili kuhusu sheria na huathiri ustadi wake kwa kumjuza hali yake ya ufahamu wa wakati huo ni yenye makosa.
2. Hakuna urekebisho wa makosa katika uzungumzaji lakini kwenye kazi zilizoandikwa na kwa marudio ya kisarufi.
3. Makosa yanayohitaji kurekebishwa ni yanayotokea mara nyingi na yanastahili kupewa kipaumbele.

4. Makosa yanastahili kurekebishwa kwa kufuatia mtindo sahihi au njia ya ugunduzi.

Krashen alijadili upungufu katika vifaa vya kusoma. Alidai kuwa, ili vifaa vya kufundishia viweze kusaidia wanafunzi kuipokea lugha lazima viwe na maelezo yanayoeleweka, yanayohusiana na mada husika, yanayovutia, yanayofurahisha na yasiyo changamano. Vifaa vya kufundishia vinastahili kufuata sheria ambazo zinaweza kufunzika na kusomeka. Vifaa hivi ni muhimu kwani vinajaliza mbinu zingine zinazotumiwa darasani.

Vifaa/ vitabu vingine vina upungufu kwa njia zifuatazo;

1. Kutumia zoezi na maswali yanayojikita tu katika mada, sarufi na msamiati. Krashen anaeleza mtindo huu unamkatisha mwanafunzi tamaa kwa sababu zoezi linalenga kusoma ila sio kupokea na kuelewa kinachosomwa.
2. Waandishi wa vitabu wanastahili kukoma kujikita kwa mfululizo wa kawaida wa kuwasilisha kazi zao na waibue mpangilio mpya wa kazi hizo.

Mihimili

Japo nadharia hii ilitumiwa kwa masuala ya sarufi na lugha, ilikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu. Utafiti ulikopa kutokana na ujuzi wa kijumla wa nadharia hii kuhusu vifaa kutengenezwa kwa mpangilio ambao unaeleweka kwa ngazi tofauti za shule ya upili na uwezo wa dhana kujengeana kutoka rahisi hadi ngumu. Vigezo vifuatavyo kutokana na nadharia hii viliongoza utafiti huu:

- 1) Ili vifaa vya kusoma viweze kusaidia mwanafunzi lazima viwe na maelezo yanayoeleweka na yasiyo changamano. Mhimili huu ulichunguza iwapo vitabu tofauti vinawasilisha uainishaji ule ule kwa njia tofauti au njia sawa. Hii ilisaidia kuelewa iwapo kuna changamoto au matatizo yaliyoibuka kutokana na uainishaji tofauti kwenye vitabu vilivyoidhinishwa.
- 2) Kanuni wazi ziwepo za kufuatwa katika kutayarisha vifaa vya kufundishia ili viwe na usawa wa kuwasilisha matini na dhana mbalimbali. Hili liliondoa dhana kinzani na changamano kama vitabu tofauti kuelezea dhana ile ile kwa njia tofauti. Tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi viliweza kuwasilishwa kwa mujibu wa silabasi na kusaidia wanafunzi, walimu na waandishi kufuata mpangilio ufaao wa uainishaji wa tanzu na vijitanzu.
- 3) Wanafunzi walielewa vyema kazi iliyowasilishwa kwa mpangilio asili ($i+1$) na wenye kujengea dhana kuanzia rahisi hadi ngumu.
- 4) Mhimili huu ulichunguza iwapo uainishaji kwenye vitabu teule unafuata mpangilio dhahiri au usio wazi.
- 5) Utofauti uliojitokeza na makosa katika vitabu yalistahili kurekebishwa. Dhana za somo la fasihi simulizi ziliweza kueleweka kwa ufasaha. Mhimili huu ulichunguza iwapo vitabu hata baada ya toleo jipya kuchapishwa makosa ya awali ya uainishaji yanabaki au yanarekebishwa.

1.10 Mbinu za Utafiti

Hizi ni njia tofauti za kutumiwa ili kufikia malengo ya utafiti. Mbinu zifuatazo zilizingatiwa katika utafiti huu;

1.10.1 Mahali pa Utafiti

Huu ni utafiti wa maktabani na nyanjani. Data ya maktabani ilijenga lengo la kwanza na la pili ambayo ndiyo ya kimsingi. Data hii ilitoka kwenye vitabu vinne vya shule ya upili vilivyoidhinishwa vya Kiswahili; (*Chemchemi za Kiswahili, Kiswahili Fasaha, Johari ya Kiswahili na Kiswahili Kitukuzwe*). Data ilitokana na sehemu ya kusikiliza na kuzungumza inayoangazia uainishaji wa fasihi simulizi.

Vitabu hivi vina tofauti katika uainishaji wa tanzu. Data ya nyanjani ni ya sekondari ambayo ilijenga lengo la tatu. Nyanjani mtafiti alichunguza matatizo yanayotokana na vitabu tofauti kuwasilisha uainishaji wa tanzu kwa njia tofauti. Ujumbe huu ulitokana na wanafunzi na walimu wa shule nne za upili (Shule ya wasichana Mwaani, shule ya wavulana Makueni, shule ya wavulana Mwaani na shule ya upili Nthangu).

1.10.2 Muundo wa Utafiti

Kulingana na Kerlinger (1981) muundo ni mpangilio na mkakati wa mtazamo wa uchunguzi ili kuweza kupata majibu ya maswali ya utafiti. Muundo wa kinaelezo ulitumiwa katika utafiti huu. Muundo huu ulionyesha jinsi ya kuufanya uchunguzi kwa kufuata njia tofauti na pia kueleza matokeo ya utafiti.

Muundo huu ulitumiwa kupendekeza uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu kwenye vitabu vya kufundishia Kiswahili kwa shule za upili. Ulibainisha misingi ya uainishaji unaotofautiana kwenye vitabu hivyo kisha kutoa suluhisho kwa matatizo yanayotokana na uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu kwa wanafunzi na walimu ambao ndio wapokezi wa dhana hizi za fasihi simulizi.

1.10.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ni sehemu ya kitu au watu fulani ambao huteuliwa kutumiwa kwa minajili ya kufanya maamuzi yanayohusu kundi nzima (Kothari, 2007). Kothari (2004) anazidi kueleza kuwa sampuli wakilishi ni kati ya asilimia 10 na 15 ya jumuiya yote.

Watafiti walitumia sampuli kusudi kuchagua vitabu vinne vya Kiswahili vilivyoidhinishwa kwa shule za upili nchini Kenya. Idadi hii ilitokana na vitabu sita ambavyo huteuliwa kwa kila somo na KICD. Vitabu hivyo ni: *Chemchemi za Kiswahili, Kiswahili Kitukuzwe, Johari ya Kiswahili na Kiswahili Fasaha*. Vitabu hivyo vilichaguliwa kwani kutokana na utafiti wa awali kwenye shule nne zilizoteuliwa ndivyo vilitumiwa kufundishia Kiswahili. Vitabu hivyo vilimpa mtafiti data ya kimsingi kutokana na ujumbe unaohusu uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

Shule nne za upili zilichaguliwa katika kaunti ya Makueni kwa sababu zingeweza kumpa mtafiti data ya kutosha kutokana na ufahamu kuwa vitabu vilivyoteuliwa vipo katika shule hizi. Isitoshe, viwango vya umilisi vya wanafunzi kwenye shule hizi vinatofautiana. Wanafunzi ishirini wa kidato cha nne kwa kila shule walichaguliwa kwa usampulishaji bahatishi. Usampulishaji kusudi ulilenga kidato cha nne kwa sababu wanafunzi hawa huwa wameipokea silabasi ya Kiswahili kuanzia ngazi ya kwanza (Kidato cha Kwanza).

Walimu wawili wa somo la Kiswahili waliteuliwa ili kujaza hojaji iliyohusu uainishaji wa fasihi simulizi na ambayo inapatikana kwenye viambatisho. Wasailiwa wote kwa jumla walikuwa themanini na wanane.

1.10.4 Mbinu za Ukusanyaji Data

Data ya maktabani, ambayo ni ya kimsingi, ilipatikana kwa kusoma kuhusu uainishaji wa fasihi simulizi kwenye vitabu vya Kiswahili vilivyoidhinishwa na kunakili maelezo hayo. Mtafiti alitumia kalamu na daftari kunakili maneno na sentensi zilizoonyesha uainishaji wa fasihi simulizi.

Data ya nyanjani, ambayo ni data endelevi, ilikusanywa kwa kutumia hojaji ya maswali yaliyohusu fasihi simulizi, iliyojazwa na walimu na wanafunzi; hojaji hiyo imeambatishwa kwenye tasnifu hii. Hojaji ilihusisha maswali wazi na funge ambayo yaliwezesha wasailiwa kutoa ujumbe mahsusi na wa kijumla. Ujumbe huu ulimwezesha mtafiti kuafikia malengo ya utafiti.

1.10.5 Mbinu za Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji

Uchunguzi huu ulitumikiza mbinu ya uchanganuzi matini (content analysis approach). Kulingana na Mugenda & Mugenda (2003) kusudi kuu la uchanganuzi matini ni kusoma matini iliyopo kama katika vitabu na gazeti ili kutambua sababu zinazohusu jambo mahsusi. Uchanganuzi wa data ulifanywa kimaielezo na kwa njia ya mjadala wa matokeo ya data ya maktabani na nyanjani.

Majedwali yalitumiwa kuchanganua baadhi ya data ili kulinganisha na kulinganua aina ya vitabu katika shule teule, idadi tofauti ya tanzu kwenye vitabu hivyo na uainisho wa tanzu za fasihi simulizi.

Data iliyopatikana kuhusu uainishaji tofauti kwenye vitabu vilivyoidhinishwa iliwasilishwa kwa maelezo ya mjadala na majedwali ili kupendekeza suluhisho kwa athari za uainishaji unaotofautiana katika fasihi simulizi.

Majedwali yalionyeshwa: jinsi vitabu tofauti vimeainisha, misingi iliyotumiwa kuainisha fasihi simulizi na matokeo ya utafiti kutokana na majibu ya wanafunzi na walimu. Matokeo hayo yalikusiana na maelezo ya uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika vitabu vilivyoidhinishwa kufundishia kwa shule za upili nchini Kenya. Zaidi ya hayo, suluhisho kwa matatizo ya uainishaji liliwasilishwa.

1.10.6 Maadili ya Utafiti

Idhini ya utafiti ilitokana na kamati ya maadili ya chuo cha Kenyatta na shirika la National Commission for Science Technology and Innovation (NACOSTI). Idhini hizi ziliwapa watafiti kibali cha kuanza kufanya utafiti na kabla ya utafiti kufanywa walimu, wanafunzi na wasimamizi wa shule husika walielezwa umuhimu wa utafiti na kuhakikishiwa majina yao na ya shule zao yangebaki kuwa siri. Wasailiwa walihakikishiwa kuwa majibu waliyotoa yangeweza kusaidia katika kuendeleza somo la Kiswahili na kuchangia tafiti zaidi katika eneo hili.

1.11 Hitimisho

Sura hii imeangazia vipengele vya utafiti Kama: usuli wa mada, sababu za kuchangua mada, suala la utafiti, malengo na masuala ya utafiti. Pamoja na hayo, mbinu za utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia mbili za utafiti zimeshughulikiwa. Mihimili ya nadharia hizi ilitumiwa kuchanganua data iliyopatikana vitabuni na nyanjani. Isitoshe, maadili ya utafiti yamefafanuliwa. Sura inayofuatia inahusu tofauti za uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

SURA YA PILI: TOFAUTI ZA UAINISHAJI WA TANZU NA VIJITANZU VYA FASIHI SIMULIZI

2.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeshughulikia usuli, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

Sura hii inahusu tofauti za uainishaji na uwasilishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika vitabu vilivyoidhinishwa. Baadhi ya vitabu hivi ni Kiswahili Kitukuzwe, Johari ya Kiswahili, Kiswahili Fasaha na Chemchemi za Kiswahili. Data ilitokana na sehemu ya kusikiliza na kuzungumza katika vitabu vinne vilivyoidhinishwa vya kidato cha nne. Vitabu vyenyewe vinatumiwa kufundishia fasihi simulizi ya somo la Kiswahili, katika shule za upili nchini Kenya. Lengo kuu lilikuwa ni kuonyesha jinsi vitabu mbalimbali vinavyoainisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi kwa njia tofauti, kutumia istilahi tofauti na kuwa na idadi tofauti ya tanzu.

Nadharia ya Tanzu ilitumika kuchanganua data. Nadharia hii ilionyesha jinsi uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi unavyofanyika. Ilionyesha uainishaji wa tanzu upo ulimwenguni. Nadharia hii ilithibitisha kuwa kuna mifumo au vigezo vya kujenga tanzu za fasihi simulizi. Idadi ya tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi hutofautiana kutegemea waandishi tofauti. Waandishi na wataalam tofauti wa fasihi simulizi wameibuka na idadi tofauti ya tanzu kwani wanaegemea misingi tofauti inayojenga tanzu hizi. Uainishaji tofauti wa tanzu umeonyeshwa katika vitabu vilivyoidhinishwa kufundishia fasihi simulizi.

Nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa lugha ya pili imeonyesha matini mbalimbali zinavyowasilishwa katika vitabu vya kusoma ambavyo Krashen anarejelea kuwa vifaa (vitabu). Msisitizo ukiwa katika uwasilishaji kwenye vitabu kuwa je, matini zinatimia lugha sahili na inayoeleweka? Je, makosa yanayofanywa yanafanyiwa marekebisho? Je, vigezo sawa vinafuatwa katika uandishi wa matini za fasihi simulizi ili pasiwe na utata na dhana changamano kwa wanafunzi. Tangu na vijitanzu vya fasihi simulizi ndivyo vinarejelewa kuwa matini katika vifaa (vitabu) vilivyoidhinishwa kufundisha fasihi simulizi kwa shule za upili. Nadharia hizi mbili zililengwa ili kuafikia malengo ya utafiti huu kwa kuchanganua uwasilishaji ulivyo katika vitabu teule.

2.2 Dhana ya Fasihi, Fasihi Simulizi na Uainishaji

Fasihi ni sanaa inayoakisi hali ya mwanadamu. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2019) fasihi ni taaluma inayohusu tungo za sanaa kama vile ushairi, riwaya, tenzi na kadhalika. Nayo fasihi simulizi ni kazi ya fasihi iliyohifadhiwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo.

Mngaruthi (2008) anadai kuwa, fasihi simulizi kufikia sasa imepata kuhifadhiwa kwa njia mbalimbali ili isipotee. Baadhi ya namna ya kuhifadhi ameelezea kuwa ni: maandishi, kanda za kunasia sauti na picha au hata tarakilishi. Nao Waititu & Ipara (2015) wanaelezea kuwa fasihi simulizi imekuwepo kwa muda mrefu na ilianza wakati mwanadamu alipoanza kutumia lugha. Wataalam hawa wanazidi kueleza kuwa inaitwa fasihi kongwe au fasihi mama.

Kuainisha ni kupanga katika aina au makundi maalum, upangaji huu hutegemea vigezo au misingi maalum. Fasihi kwa jumla imepangwa katika makundi mawili kwa misingi ya uwasilishaji kwa hadhira na uhifadhi. Makundi haya ni: fasihi simulizi na fasihi andishi (Mngaruthi, 2008).

Kulingana na Mumbo & Ngamia (2005) upangaji au uainishaji hutegemea njia ya kuwasilisha au mtindo wa lugha. Wanazidi kueleza kuwa njia ya kuwasilisha ni: kusimulia, kukariri, kuimba, kuigiza au kuzungumza.

Chandler (1997) anaeleza kuwa tanzu zimegawika katika makundi. Hivyo basi kwa mujibu wa nadharia ya tanzu, tanzu zipo ulimwenguni na ni dhana zisizo na kikomo mfano ushairi, nathari na maigizo. Zaidi ya hayo, tanzu zimeelezwa na wataalam mbalimbali kwa njia zinazotofautiana.

2.3 Uainishaji wa Fasihi Simulizi kwa mujibu wa Vitabu Tofauti

Kwa mujibu wa Khamis katika Ogechi, Shitemi & Simala (2008) utanzu ni aina ya kazi ya fasihi inayozungukwa na kanuni au kaida fulani ambazo zikikiukwa huweza kuzuka ‘suitafahamu’ na mzozo mkubwa miongoni mwa waandishi, wasomaji na wahakiki.

Kwa mujibu wa Krashen (1982) katika nadharia ya ujifundishaji na upokeaji wa lugha ya pili, uandishi wa vifaa vya kufundishia unastahili kufuata mpangilio na kanuni mahsusi. Hii itasaidia kuondoa utata wa vifaa na matini kwenye vitabu vya kufundishia. Tanzu za fasihi hufuata kanuni jinsi uandishi wa vitabu na mpangilio wa matini unavyofuata sheria au silabasi.

Tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi zimewasilishwa kwa njia tofauti kwenye vitabu vya kufundishia kwa shule za upili nchini Kenya. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, uainishaji wa tanzu umefanyika tangu enzi za urasimi; mfano nathari, ushairi na maigizo.


Kwa mujibu wa Kobia katika Njogu, Momanyi & Mathooko (2006), baadhi ya vitabu vina udhaifu ambao unapelekea kutoshughulikiwa kwa kina kwa vipera mbalimbali vya fasihi simulizi. Anazidi kueleza kuwa udhaifu huu hujitokeza kwa vitabu kutaja vipera bila maelezo ya kina na vitabu vingine kukosa baadhi ya vipera.

Uainishaji katika vitabu hivyo umeonyeshwa kwa jedwali na maelezo. Fasihi simulizi hupatikana kwenye stadi ya kusikiliza na kuzungumza ambayo ni moja kati ya stadi nne za ujifunzaji katika somo la Kiswahili.

Uainishaji kwa mujibu wa vitabu tofauti umewasilishwa kwa njia zifuatazo:

2.3.1 Kiswahili Kitukuzwe

Jedwali 2.1: Uainishaji; Kiswahili Kitukuzwe



Kutokana na uainishaji huu katika Kiswahili Kitukuzwe kidato cha nne, ni wazi kuwa fasihi simulizi ina tanzu sita kuu: mazungumzo, maigizo, hadithi, ushairi, semi na ngomezi. Utata uliojitokeza ni tofauti iliyopo ya uwasilishaji wa idadi ya tanzu kwenye mchoro kama ilivyo katika Chemchemi za Kiswahili (uk 15) ni kuwa tanzu kuu kulingana na mchoro ni nne: hadithi, maigizo, ushairi na semi.

Ni wazi kuwa kwa mujibu wa kitabu hiki cha Kiswahili Kitukuzwe, ngomezi na mazungumzo sio vijitanzu chini ya tanzu zingine ila ni tanzu kuu za fasihi simulizi zinazojisimamia na zenye sifa bainifu. Licha ya hayo, maelezo ya kina kuhusu maana na uwasilishaji wa tanzu hizi mbili yamejadiliwa katika ufafanuzi wa dhana kwenye kitabu hicho.

Kwa mujibu wa mhimili wa kwanza kwenye nadharia ya Tanzu, fasihi simulizi imegawika katika tanzu na kwenye kitabu hiki imeainishwa katika aina mbalimbali. Utata unaotokea ni kuwa idadi ya tanzu ni sita hali inayokinzana na kitabu cha Wamitila (2003): Chemchemi za Kiswahili chenye tanzu nne. Kwa kuangazia mchoro huu katika Kiswahili Kitukuzwe kuna upungufu unaojitokeza wa uwasilishaji ambapo vijitanzu vya hadithi kama: mbazi, ngano za mtanziko na ngano za mazimwi hazijawasilishwa. Vijitanzu hivi vilivyokosekana katika kitabu hicho vipo katika Chemchemi za Kiswahili chini ya utanzu wa hadithi au simulizi.

Isitoshe chini ya utanzu mkuu wa maigizo kijitanzu cha michezo kimetajwa tu bila kubainishwa aina. Sio wazi iwapo hii ni michezo ya watoto au ya jukwaani. Kuna tofauti kuu kati ya vijipera hivi vya fasihi simulizi. Isitoshe, katika uk 176 mwandishi ametaja uigizaji hufungamana na shughuli za kila siku kama vile jando, unyago, michezo ya watoto, arusi, matanga na matambiko.

Kwa misingi ya nadharia ya Krashen, vifaa hivi vya kufundishia havijawasilisha dhana wazi kwa wasomaji bali kuna upungufu wa maelezo na utata wa uwasilishaji. Hii inapelekea kuwepo kwa dhana changamano kwenye vitabu inayopelekea utata katika mchakato wa ufundishaji na upokeaji wa lugha.

Idadi kinzani kwenye Kiswahili Kitukuzwe na Chemchemi za Kiswahili inaibua utata. Kwa misingi ya mhimili wa Nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili vifaa vya kusoma lazima viwe na maelezo yanayoeleweka.

Maelezo yasiwe changamano ili iwe rahisi kwa mwanafunzi kuelewa dhana za fasihi simulizi. Ni vyema kwa vitabu vilivyoidhinishwa kufundishia Kiswahili kwa shule za upili viwe na maelezo sawa. Hii itaondoa uchangamano unaojitokeza wa idadi ya tanzu kuu za fasihi simulizi. Uhora wa vitabu utaimarishwa na wasomi wataamini maelezo yaliyopo kwenye vifaa hivi.


Zaidi ya hayo, mchoro huu ulionyesha kijitanzu cha ulumbi kipo chini ya utanzu wa mazungumzo ilhali katika mchoro kwenye kitabu cha Chemchemi za Kiswahili kijitanzu hiki kipo chini ya utanzu wa maigizo (uk 15). Kwa mujibu wa Kimani katika Njogu et al. (2006) baadhi ya vitabu hutoa maelezo tofauti na vingine kuhusu kipera kimoja. Ulumbi katika Kiswahili Kitukuzwe upo chini ya mazungumzo ilhali katika Chemchemi za Kiswahili upo chini ya maigizo. Kwa mujibu wa mihimili ya nadharia ya Tanzu, utanzu unaweza kujisimamia kimaana na sifa, hivyo basi vijitanzu vya maigizo na vya mazungumzo vinaweza kubainishwa wazi kama vijitanzu vyenye sifa kamilifu.

Kwa jumla hii ni ithibati tosha kuwa ipo haja ya kushughulikiwa upya kwa uainishaji na uwasilishaji wa idadi ya tanzu kwenye vitabu vilivyoidhinishwa ili utata unaojitokeza utatuliwe.

Makosa yanayojitokeza katika vifaa vya kufundishia kwa mujibu wa nadharia ya Krashen yanastahili kurekebishwa ili vitabu vileweke na wasomaji.

2.3.2 Chemchemi za Kiswahili

Jedwali 2.2: Uainishaji; Chemchemi za Kiswahili



Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu sifa bainifu za utanzu mmoja zinaweza kubainishwa na kutofautishwa na utanzu mwingine. Hivyo basi kupata makundi mahsusi ya fasihi simulizi.

Wamitila (2003) anaeleza kuwa, tanzu kuu za fasihi simulizi ni tano: hadithi, maigizo, semi, ushairi na mazungumzo.

Ila kwa misingi ya vigezo vya uainishaji, anawasilisha katika mchoro (uk 15) tanzu za fasihi simulizi kuwa nne: hadithi, maigizo, ushairi na semi. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu ni kuwa uainishaji wa fasihi simulizi upo. Dhana hizi mbili sio wazi hasa kwa mwanafunzi kwani hazijaelezewa kwa kina. Hivyo basi mwanafunzi huenda asijue kwa uhakika tanzu za fasihi simulizi ni tano au ni nne kwa misingi ya Wamitila. Tanzu kuu hapa ni tofauti na ilivyo katika vitabu vingine kama Johari ya Kiswahili na Kiswahili Kitukuzwe ambavyo vinaonyesha tanzu sita kwenye michoro yao (uk 79) na (uk 15) mtawalia.

Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, tanzu zina uwezo wa kujisimamia kwani zina sifa bainifu. Utanzu wa mazungumzo na ngomezi ambazo katika vitabu vingine zimebainishwa kama tanzu kuu hapa katika Chemchemi za Kiswahili tanzu hizi zinaonyeshwa kuwa chini ya tanzu zingine. Mazungumzo yanaonyeshwa chini ya utanzu wa maigizo ambapo Wamitila anazidi kuonyesha mfano wa mazungumzo kuwa ni mawaidha. Nao utanzu wa ngomezi unawasilishwa kuwa kijitanzu cha maigizo katika (uk 15).

Kando na hayo, majigambo ambayo ni mfano wa aina za maghani kwenye mchoro huu yanaonyeshwa kama kijitanzu cha ushairi. Katika yaliyomo sura ya kumi na saba sehemu ya fasihi simulizi imetaja wazi maghani na aina zake.

Hivyo basi, majigambo ni aina ya maghani ya kisimulizi. Kwa muhtasari, majigambo yangeonyeshwa chini ya maghani kama ilivyo katika mawaidha yaliyoonyeshwa chini ya mazungumzo.


Kobia katika Njogu et al. (2006) anafafanua kuwa, baadhi ya vipera vya fasihi simulizi vilikuwa vimepuuzwa katika silabasi ya 1992 na kushughulikiwa baadaye katika silabasi ya 2002. Vipera hivyo ni kama: ulumbi, soga, mawaidha, ngomezi, misimu na kadhalika. Wamitila (2003) katika mchoro huu anaonyesha kuwa soga ni kijitanzu cha hadithi ilhali katika vitabu vingine sivyo.

Katika Kiswahili Kitukuzwe, Kiswahili Fasaha na Johari ya Kiswahili, soga imetajwa kuwa ni kijitanzu cha mazungumzo. Zaidi ya hayo, ulumbi na malumbano ya utani yameorodheshwa kama vijitanzu vya maigizo kwenye Chemchemi za Kiswahili ilhali katika vitabu vingine ni vijitanzu vya mazungumzo. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, sifa bainifu za utanzu mmoja zinaweza kubainishwa na kutofautishwa na za utanzu mwingine. Uchanganuzi huu umeonyesha kuwa tanzu hizi zilizokuwa zimepuuzwa kwenye silabasi 1992 zilipoanza kujumlishwa kwenye silabasi 2002 hazikuchunguzwa vyema kwa misingi ya sifa zake bainifu ndiposa ukinzano huu wa uainishaji ukatokea. Kwa misingi ya nadharia ya Krashen, makosa katika vifaa vya kufundishia yanastahili kurekebisha ili wanafunzi waelewe dhana kwa uwazi.

Ulumbi katika maelezo ya Wamitila (2003) ni kipera muhimu cha mazungumzo (uk 82) hivyo basi kipera au kijitanzu hiki kingeonyeshwa chini ya mazungumzo katika mchoro (uk 15) kama yalivyoonyeshwa mawaidha. Kwa mujibu wa nadharia ya Krashen, ili vifaa (vitabu) vya kusoma visaidie mwanafunzi lazima viwe na maelezo yanayoeleweka na yasiyo changamano. Maelezo ya mazungumzo na ngomezi yanastahili kuwa wazi na yanayoafiki silabasi ili yafae wasomaji wa kazi za fasihi.

2.3.3 Johari ya Kiswahili

Jedwali 2.3: Uainishaji; Johari ya Kiswahili



Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, tanzu zipo ulimwenguni na uainishaji umefanyika tangu enzi za urasimi; mfano ushairi, nathari na maigizo. Mumbo & Ngamia (2005) wanawasilisha uainishaji wa fasihi simulizi kwa tanzu sita kuu ila mchoro huu hauonyeshi vijitanzu vyote chini ya tanzu kuu. Kitabu hiki ni kwa kidato cha nne na kinatarajiwa kurejelea tanzu na vijitanzu vyote vya fasihi simulizi na kutoa maelezo ya kina kwa mwanafunzi anayefanya maandalizi ya mthani wa kitaifa. Katika mchoro huu tanzu kuu ni sita kama ilivyo katika kitabu cha Kiswahili Kitukuzwe kwa kidato cha nne: mazungumzo, hadithi, maigizo, ushairi, semi na ngomezi.

Udhaifu au upungufu unaojitokeza wazi ni wa vijitanzu vilivyokosekana kwenye mchoro. Upungufu unaojitokeza kwenye kitabu hiki kwa mujibu wa Kobia katika Njogu et al. (2006) ni kuwa, maelezo sio toshelevu na vipera vingine havimo kabisa.

Vijitanzu vilivyokosekana ni kama; malumbano, majingambo, vichekesho, ngonjera na vitanza ndimi. Kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, kanuni wazi zinastahili kuwepo na kufuatwa vifaa vinapotayarishwa ili viwe na usawa wa kuwasilisha matini.

Kando na hayo vijitanzu vya semi havijaorodheshwa vyote katika mchoro huu wa (Mumbo & Ngamia, 2005). Kwa mujibu wa nadharia ya tanzu ni kuwa uainishaji wa tanzu na vijitanzu upo na umekuwepo tangu enzi za Aristotle. Vijitanzu vya misemo na vitanza ndimi havipo. Japo imeelezwa awali kuwa kitabu hiki kinaoana na vingine katika uwasilishaji wa tanzu ni bayana kuwa kuna upungufu wa uwasilishaji wa vijitanzu ambavyo ni muhimu kwa mwanafunzi kuelewa wazi hasa katika kiwango hiki cha ujifunzaji.

2.3.4 Kiswahili Fasaha

Katika Kiswahili Fasaha kwa kidato cha nne, hakuna mchoro au jedwali linaloonyesha tanzu kuu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Kwa mujibu wa nadharia ya Krashen vifaa vya kufundishia vinastahili kuwasilisha maelezo kwa njia sahili ili kuwezesha wanafunzi kuelewa, mchoro ni njia mojawapo ya kurahisisha usomaji na uelewa wa mwanafunzi. Isitoshe mchoro hukumbukwa zaidi kuliko maelezo. Hivyo basi, kwa kukosa mchoro wa uainishaji kitabu hiki kina upungufu kwani uwasilishaji wa fasihi simulizi sio sahili.

Waititu & Ipara (2015) katika Kiswahili Fasaha wanaanza kwa kueleza sifa za fasihi simulizi katika (uk 1) na kuendeleza kwa kutofautisha fasihi simulizi na andishi katika (uk 10). Utanzu wa maigizo tu ndio umeelezwa wazi kuwa ni utanzu mkuu wa fasihi simulizi kwenye kitabu hiki:

“...maigizo ni moja ya tanzu za fasihi simulizi yenye umbo la tamthilia...maneno na

matendo ya binadamu hutokea kwa wingi na hupewa umuhimu mkubwa (uk 185).”

Kwa mujibu wa maelezo haya, mhimili wa nadharia ya tanzu unaafikiwa kwani inaonyesha uwezo wa kuwepo kwa tanzu na zaidi ya hayo kila utanzu kuwa na sifa bainifu. Kuongeza hayo inaakisi kuwa maigizo yamegawika katika aina:

- i. Maigizo ya matukio mbalimbali kama vita, ndoa, kilimo, tohara na kadhalika.
- ii. Kucheza ngoma za kitamaduni.
- iii. Michezo ya watoto kama vile unyumba.
- iv. Kufanya uganga kama wa ramli.
- v. Maadhimisho na matukio muhimu kama kutawazwa kwa kiongozi.

Maelezo haya ya Maigizo yaanaakisi mhimili wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili kuwa vifaa viwasilishe matini kwa njia sahili isiyokuwa na ukinzano.

Maelezo hayo ni wazi kwa wasomaji hivyo basi hapataibuka utata wowote katika ujifunzaji na upokeaji.

Hakuna sehemu inayoonyesha tanzu kuu za fasihi simulizi ni zipi. Katika stadi hii ya kusikiliza na kuzungumza waandishi hawa wanavielezea vijitanzu vya fasihi simulizi.

Mifano:

“...mafumbo ni semi ambazo maana zake za ndani zimefichika na huhitaji aliyelengwa afikiri ili aweze kutambua jambo lililofichwa (uk 57).”

“...mighani ni hadithi ambazo husimulia mambo ya watu waliotenda matendo ya kishujaa katika jamii (uk 143).”

“...nyimbo ni mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi ambazo zimetumika kutekeleza mambo mbalimbali...nyimbo labda ndicho kipera cha fasihi simulizi ambacho kina athari kubwa zaidi kwa idadi kubwa ya watu kuliko vingine. (uk 201).”

Kutokana na maelezo na mifano iliyotajwa hapo juu, mafumbo na mighani ni vijitanzu ambavyo vimeelezwa. Sifa na umuhimu wake pia umetajwa ila waandishi hawa wanaposema mafumbo ni semi na mighani ni hadithi kuna upungufu wa maelezo ya semi na hadithi ambazo zinastahili kuwa ndizo tanzu kuu.

Kando na hayo, baadhi ya vipera vya fasihi simulizi havitajwi vipo chini ya tanzu zipi. Nyimbo zimeelezwa tu bila maana yake mahsusi. Kando na hayo, hazitajwi ni kipera cha utanzu upi wa fasihi simulizi. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, uainishaji wa tanzu upo katika makundi kwani tanzu na vijitanzu vina uwezo wa kuwa na sifa bainifu. Katika kitabu hiki hakuna maelezo wazi ya uainisho wa tanzu kuu za fasihi simulizi hivyo basi inabaki ni kazi ya mwanafunzi au mwalimu kujaliza utanzu wa kijitanzu fulani kulingana na uelewa wake wa kijitanzu kilichotajwa, Mifano:

“...ngomezi ni sanaa ya ngoma. Ni sanaa ya fasihi simulizi ambayo huwasilishwa kwa midundo ya ngoma inayoakisi lugha ya binadamu (uk 117).”

“...miviga ni sherehe au ibada ambazo aghalabu hufanywa katika kipindi maalumu na kwa kufuata desturi au kawaida fulani katika jamii mbalimbali (uk 115).”

Kwa mujibu wa mifano hii ni kuwa ngomezi na miviga haielezewi bayana ipo chini ya tanzu zipi kuu au hata iwapo zenyewe ni tanzu kuu.

Kwa mujibu wa Krashen (1985) vifaa vinastahili kuwa sahili na visivyo na uchangamano. Vitabu vya wanafunzi vinafaa kuwasilisha mada au matini mbalimbali kwa uwazi. Upungufu huu wa maelezo unaweza kumpelekea mwanafunzi kujaliza maana yanayooana na dhana hizi bila kufuata misingi mahsusi. Uwasilishaji huu wa vipera vya fasihi simulizi unahitaji kuangaziwa upya ili dhana tata kama ugumu wa kuelewa fasihi simulizi ziondolewe miongoni mwa wanafunzi.

2.4 Tanzu Kuu zenye Utata wa Uainishaji

Kobia katika Njogu et al. (2006) silabasi mwaka wa 2002 inaonyesha kuwa tanzu kuu za fasihi simulizi ni sita. Kwa misingi ya nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, kanuni wazi zinastahili kuwepo katika kutayarisha vifaa vya kufundishia ili viwe na usawa wa kuwasilisha matini.


Kwa kuangazia vitabu vinne vilivyorejelewa katika utafiti huu: Johari ya Kiswahili, Kiswahili Fasaha, Chemchemi za Kiswahili na Kiswahili Kitukuzwe idadi na uainishaji wa tanzu kuu za fasihi simulizi unatofautiana. Katika Johari ya Kiswahili na Kiswahili Kitukuzwe tanzu kuu za fasihi simulizi ni sita kama ilivyo silabasi mwaka wa 2002: mazungumzo, masimulizi/hadithi, maigizo, ushairi, semi na ngomezi. Hii ni tofauti na ilivyo katika Chemchemi za Kiswahili kwani tanzu kuu ni nne: hadithi/masimulizi, maigizo, ushairi na semi.

Katika kitabu cha Chemchemi za Kiswahili, Wamitila (2003) anaonyesha kuwa tanzu mbili kuu zinazozua utata katika maelezo haya ya uainishaji zinaainishwa kuwa vijitanzu chini ya tanzu zingine na ambazo ni mazungumzo na ngomezi. Swali kuu linaloibuka hapa ni iwapo hizi zinastahili kuwa tanzu kuu au vijitanzu chini ya tanzu kuu.

Kwa misingi ya nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, ili vifaa viweze kusaidia mwanafunzi lazima viwe na maelezo yanayoeleweka na yasiyo changamano. Waititu & Ipara (2015) hawajaonyesha uainishaji wazi kwani katika kazi yao wamejikita tu katika kueleza vijitanzu vya fasihi simulizi kwa kulenga: aina, sifa na umuhimu wa vijitanzu hivyo. Hawajashughulikia tanzu kuu kwani hakuna maelezo yoyote kuhusu maana ya tanzu kuu au hata aina zinazopatikana chini ya tanzu hizo kuu.


Kwa mujibu wa kitabu cha Kiswahili Kitukuzwe na Johari ya Kiswahili kwa Kidato cha Nne (uk 15 na 79) mtawalia ni kuwa tanzu hizi mbili ni tanzu kuu chini ya fasihi simulizi kama inavyoonyeshwa katika mchoro:

Jedwali 2.4: Tanzu Kuu zenye Utata.



Kutokana na mchoro ufuatao ni wazi kuwa Wamitila (2003) anaonyesha utanzu wa mazungumzo na ngomezi kuwa ni vijitanzu vya maigizo ila sio tanzu zenye uwezo wa kujisimamia.

Jedwali 2.5: Chemchemi za Kiswahili vijitanzu vya maigizo



Tanzu hizi kuu zenye utata zinajadiliwa katika maelezo yafuatayo:

2.4.1 Mazungumzo

Kwa mujibu wa nadharia ya tanzu, sifa bainifu za utanzu mmoja zinaweza kubainishwa na kutofautishwa na utanzu mwingine. Kwa mujibu wa Mumbo & Ngamia (2005), mazungumzo yanarejelewa kama mojawapo ya vipera sita vikuu vya fasihi simulizi. Wanazidi kueleza kuwa, mazungumzo ni maongezi ya kisanii yanayozingatia tamathali za usemi na mbinu nyingine za usanii ili kuwavutia wasikilizaji. Kando na hayo, wanaorodhesha tanzu za mazungumzo kuwa: malumbano ya utani, ulumbi, soga na mawaidha.(uk 78).

Kwa mujibu wa Kenya Literature Bureau (2009) katika Kiswahili Kitukuzwe mazungumzo yameonyeshwa kama tanzu kuu katika mchoro (uk 15) ila hayajatolewa maelezo kama tanzu zingine zilivyofanyiwa katika sehemu mbalimbali za sura ishirini na mbili zilizopo katika kitabu hiki.

Kwa kufuatia maelezo ya Mumbo & Ngamia (2005) japo ukuruba unajitokeza kati ya utanzu wa mazungumzo na utanzu wa maigizo, kila mojawapo ina sifa bainifu hivyo basi kuwa na uwezo wa kujisimamia kama tanzu kuu. Hii ni kwa misingi ya nadharia ya Tanzu.

2.4.2 Ngomezi

Kulingana na Mumbo & Ngamia (2005) ngomezi ni mojawapo kati ya vipera sita vikuu vya fasihi simulizi. Wanaeleza kuwa ngomezi ni fasihi ya ngoma kwa ujumbe. Wanaongeza kuwa huwasilisha ujumbe wake kwa njia ya ngoma yenye midundo maalumu inayotambulikana na jamii.

Kenya Literature Bureau (2009) katika Kiswahili Kitukuzwe kwenye mchoro (uk 15) ngomezi inaonyeshwa kama utanzu mkuu wa fasihi simulizi ila hakuna kijitanzu chochote kinachoonyeshwa chini yake. Ngomezi inaelezewa kuwa ni jina linalotokana na neno ngoma.

“...Jamii za kiafrika hapo kale zilitumia njia tofauti kupasha habari. Miongoni mwa njia hizi ni matumizi ya ngoma. Ngomezi imehusishwa na fasihi kwa sababu ngoma hizi huashiria ujumbe fulani. Mapigo haya ni ya kazi ya sanaa (uk 163).

Kwa mujibu wa misingi ya nadharia ya Tanzu, sifa bainifu za utanzu mmoja zinaweza kubainishwa na kutofautishwa na utanzu mwingine. Kutokana na maelezo ya ngomezi yaliyotajwa awali ni kuwa, hii ni fasihi ya ngoma inayohusisha utendaji.

Njia ya kupitisha ujumbe ni mahsusi na sio kama zinavyopitishwa tanzu zingine za fasihi simulizi. Kutokana na kuwa na sifa bayana utanzu huu una uwezo wa kujisimamia kama tanzu kwani una sifa bainifu kwa kigezo cha uwasilishaji wake. Ngomezi huhusiana kwa kiwango kidogo na maigizo kwani zote huhusisha utendaji ila huu sio msingi tosha wa kuainisha ngomezi chini ya maigizo. Isitoshe, tanzu zingine za fasihi simulizi takribani zote huhusisha utendaji wa wahusika.

Ngomezi ina uwezo wa kujisimamia kama tanzu kuu kwani ina sifa bainifu zinazoitofautisha na tanzu zingine. Kobia katika Njogu et al. (2006) anaeleza kuwa kwa mujibu wa silabasi mwaka wa 2002 tanzu kuu ni sita na ngomezi ni mojawapo. Maigizo ni tofauti na ngomezi kwani huwasilishwa mbele ya hadhira kumaanisha kuwa lazima pawe na anayewasilisha na wanaowasilishiwa kama ilivyo katika vichekesho. Tofauti na maigizo, ngomezi huhitaji tu anayewasilisha ujumbe kwa ngoma kwani aghalabu hadhira au wapokezi hawapo pale. Ngoma ni njia ya kupitisha ujumbe kwa wanajamii wengine wakiwa katika boma zao. Maelezo haya ya ngomezi yameitofautisha na vipera vingine vya fasihi simulizi kwa kigezo cha lengo na jinsi inavyowasilishwa.

2.5 Vijitanzu vya Fasihi Simulizi vyenye Utata wa Uainishaji

Kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, vifaa vya kufundishia vinastahili kuwa sahili ili kueleweka kwa uwazi na wanafunzi. Kando na tanzu kuu kuwa na utata wa uwasilishaji ulioelezewa hapo juu, vijitanzu chini ya tanzu kuu pia vimeainishwa kwa njia tofauti kwenye vitabu vya kufundishia na kupelekea utata wa vipera hivyo. Sio vijitanzu vyote vya fasihi simulizi vilivyo na utata wa uainishaji.

Marekebisho ya makosa ni muhimu kwenye vifaa vya kufundishia. Hii itawezesha wasomaji kuelewa na kupenda somo la fasihi simulizi. Kwa mujibu wa Krashen (1985), ili maelezo katika vifaa yaeleweke lazima dhana ziwasilishwe kwa usahili na makosa yanayojitokeza yarekebishwe katika matoleo mengine ya vifaa hivyo. Baadhi ya vijitanzu vyenye maelezo na uwasilishaji tata kwenye vitabu vya kidato cha nne ni kama vifuatavyo: miviga, ngano, mighani, ulumbi, maghani na sogu.

2.5.1 Miviga

Kwa misingi ya nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, ili vifaa vya kusoma viweze kusaidia mwanafunzi lazima viwe na maelezo yasiyo changamano. Miviga inaelezewa kwa namna tofauti kwa mujibu wa waandishi mbalimbali. Tofauti hizi zinajitokeza, mfano katika Kiswahili Kitukuzwe na Johari ya Kiswahili, miviga ni kijitanzu cha hadithi ilhali katika Chemchemi za Kiswahili ni kijitanzu cha maigizo.


“...miviga ni kipengele kimojawapo cha maigizo (ambacho ni utanzu mmoja mkuu wa fasihi simulizi),(uk 107).”

Mumbo & Ngamia (2005) wanaeleza kuwa miviga ni sherehe au ibada ambazo huwa zinafuata utaratibu fulani wa kisanaa za maonyesho au fasihi simulizi.

Wanazidi kueleza kuwa miviga huambatana na itikadi za jamii na hutumika katika shughuli za kila siku za maisha ya watu. Katika kitabu hiki miviga ni kijitanzu cha masimulizi/hadithi kama ilivyo katika Kiswahili Kitukuzwe.

Tofauti na Mumbo & Ngamia (2005), Wamitila (2003) anaeleza kuwa sherehe za miviga huambatana na matendo au hatua fulani ambazo hujulikana kama viviga. Anaongeza kuwa baadhi ya miviga huhusishwa na sherehe za kuzaliwa, tohara, unyago, ndoa, kutambika na kadhalika.

Jedwali 2.6: Miviga, Johari ya Kiswahili



Kwa mujibu wa Kenya Literature Bureau (2009) katika Kiswahili Kitukuzwe, miviga imeelezwa kuwa ni hadithi zinazotambwa katika sherehe maalum ambazo hufanywa na jamii wakati fulani katika mwaka. Wameongeza kuwa sherehe hizi hufanywa faraghani. Isitoshe miviga huambatanishwa na matambiko ya kimila mfano arusi, matanga, majilio ya mtoto mchanga na kadhalika. Waititu & Ipara (2015) wanaeleza miviga kama sherehe au ibada ambazo aghalabu hufanywa katika kipindi maalum na kwa kufuata desturi au kaida fulani katika jamii mbalimbali. Katika kitabu hiki, miviga haijielezwa wazi ipo chini ya utanzu upi mkuu wa fasihi simulizi.

Hivyo basi, vitabu vinne vinavyorejelewa vimebaini wazi kuwa uwasilishaji wa miviga unatofautiana. Ipo haja ya usawa kwa wasomaji au wapokezi kwa mujibu wa misingi ya nadharia ya Ufundishaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili. Usawa huu utajitokeza tu kupitia marekebisho ya makosa kwa vitabu kuchapishwa upya.


Kwa mujibu wa Kobia katika Njogu et al. (2006), kitabu kimoja kina maelezo tofauti na kingine kuhusu kipera kimoja. Kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili vifaa visiwe changamano, viwasilishe dhana kwa uwazi ili wanafunzi wapate kuelewa.

2.5.2 Ulumbi


Kijitanzu hiki cha ulumbi kimeonyeshwa kuwa kipo chini ya utanzu wa mazungumzo katika kitabu cha Johari ya Kiswahili na Kiswahili Kitukuzwe ilhali katika Chemchemi za Kiswahili kipo chini ya utanzu wa maigizo. Zaidi ya hayo, katika kitabu cha Kiswahili Fasaha kijitanzu hiki hakijaelezewa kipo chini ya utanzu upi.

Kwa mujibu wa misingi ya Krashen (1982), vifaa vya kufundishia vinastahili kuwasilisha maelezo yake kwa uwazi bila uchangamano wowote. Vitabu hivi vinaenda kinyume na misingi hii kwani kijitanzu cha ulumbi kinawasilishwa kwa njia tofauti. Tofauti hii imejitokeza kwenye michoro ifuatayo:

Jedwali 2.7: Ulumbi, Chemchemi za Kiswahili



Jedwali 2.8: Ulumbi, Kiswahili Kitukuzwe



Kwa mujibu wa Kenya Literature Bureau (2009) katika Kiswahili Kitukuzwe ulumbi ni unenaji wa kifasihi ambapo msemaji huzungumza kwa ufasaha mkubwa na kutia madoido katika maongezi yake. Inaelezewa zaidi kuwa ushawishi mkubwa katika ulumbi ni uwasilishaji wake unaoambatana na viziada lugha kama ishara, kiimbo, shadda, miondoko na utendaji.

Naye Wamitila (2003) anaeleza kuwa, ulumbi ni uwezo maalumu na wa kipekee wa kimazungumzo. Anaongeza kuwa ulumbi ni kipera muhimu cha mazungumzo. Waititu & Ipara (2015) wanaeleza kuwa ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha au kuzungumza kwa ufundi wa kipekee.

Kwa misingi ya nadharia ya Tanzu, tanzu zina uwezo wa kujisimamia hivyo basi uwezo wa kuainishwa kwa uwazi katika tanzu kuu mbalimbali. Maelezo ya maana ya ulumbi yanahusiana katika vitabu hivi vinne ila tofauti inajitokeza katika uwasilishaji. Ukinzano wazi unajitokeza kati ya ulumbi kuwa ni kijitanzu cha mazungumzo au cha maigizo.

Utata huu (makosa haya) unastahili kurekebisha kama alivyoelezea Krashen (1985), katika nadharia ya Ufundishaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili. Ulumbi kutokana na maelezo yake ni aina ya mazungumzo.

2.5.3 Soga


Kobia katika Njogu et al. (2006) silabasi mwaka wa 1992 haikuhusisha vipera kama; ulumbi, soga, mawaidha na kadhalika. Katika mwaka wa 2002 soga zilikusishwa kama kipera cha mazungumzo. Kwa mujibu wa kitabu cha Kiswahili Kitukuzwe, Johari ya Kiswahili na Kiswahili Fasaha, soga imeonyeshwa kuwa ni kijitanzu cha mazungumzo ilhali katika Chemchemi za Kiswahili soga ni hadithi au simulizi.

Kando na hayo, katika Kiswahili Fasaha kijitanzu hiki kimeelezwa kuwa ni aina ya mazungumzo katika fasihi simulizi ambayo hutumika kupitisha wakati. Maelezo haya ya Waititu & Ipara (2015) yanatofautiana na mawazo ya Wamitila (2003) anayeeleza kuwa soga sio tu gumzo au mazungumzo ya kupitisha wakati, bali hutumiwa kuelezea hadithi ndogo ndogo zenye utani, ucheshi na zinazowasilisha funzo fulani muhimu katika jamii.

Kuna utata wa maelezo kuhusu soga unaojitokeza wazi. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, tanzu zipo ulimwenguni na zinajisimamia kwa sifa bainifu. Hivyo basi soga ina uwezo wa kujisimamia kama kijitanzu cha mazungumzo ila si maigizo.


Kenya Literature Bureau (2009) katika Kiswahili Kitukuzwe imeelezwa kuwa soga ni mazungumzo ya kupitisha wakati ambapo mkondo wa mazungumzo haya huwa ni masimulizi yaliyojikita kwenye chuku kiasi cha kukosa uhalisia. Michoro ifuatayo inaakisi hayo:

Jedwali 2.9: Soga, Johari



Katika mchoro huu kijitanzu cha soga kinaonyeshwa kipo chini ya utanzu wa mazungumzo. Utanzu huu wa mazungumzo kwa mujibu wa Mumbo & Ngamia (2005) ni utanzu mkuu wa fasihi simulizi. Hii ni tofauti na kitabu kinachofuatia cha Chemchemi za Kiswahili kinachoonyesha soga kama kijitanzu cha hadithi. Ulinganisho huu umeonyesha wazi kuwa utata upo wa uainishaji wa vijitanzu vya fasihi simulizi kwa mujibu wa waandishi tofauti. Kwa misingi ya nadharia ya utanzu, tanzu zina sifa bainifu na hivyo basi kuwa na uwezo wa kujisimamia.

Jedwali 2.10: Soga, Chemchemi za Kiswahili



Katika Chemchemi za Kiswahili, mchoro umeonyesha kijitanzu cha soga kuwa kipo chini ya utanzu mkuu wa hadithi au simulizi. Hii ni tofauti na ilivyo katika vitabu vingine vilivyoonyesha kuwa soga ni kijitanzu cha mazungumzo. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, kila kipera kina uwezo wa kujisimamia na sifa bainifu. soga ni kipera chenye sifa bainifu.

Utata huu unastahili kuondolewa na waandishi kwa kuweka vigezo vya kufuata misingi sawa katika kuainisha vijitanzu vya fasihi simulizi. Hii itaondoa tofauti za uwasilishaji wa uainishaji wa tanzu zinazojitokeza kwenye vitabu vilivyooidhinishwa kufundishia fasihi simulizi kwa shule za upili nchini Kenya.

2.5.4 Ngano

Kwa mujibu wa Waititu & Ipara (2005), ngano ni kipera cha hadithi au masimulizi. Waandishi hawa wanabainisha kuwa ngano ni kipera ila sio utanzu mkuu wa fasihi simulizi. Wanazidi kueleza kuwa ngano hugawika katika makundi kutegemea wahusika na kinachozungumziwa. Ngano hizi ni:

- i. Hurafa
- ii. Visasili
- iii. Hekaya
- iv. Ngano za mazimwi
- v. Ngano za mtanziko

Kutokana na maelezo hayo, sio wazi tofauti iliyopo ya maana kati ya kipera na utanzu. Neno ngano limetumiwa kuonyesha kisawe cha hadithi au masimulizi. Utata unaoibuka ni katika matumizi ya istilahi ngano, hadithi na masimulizi. Kwa mujibu wa nadharia ya Ufundishaji na Upokeaji wa lugha ya Pili tofauti zinazojitokeza kwenye vitabu na makosa yanastahili kufanyiwa marekebisho ili kuwe na usawa wa matini zinazowasilishwa kwa wanafunzi.

Aidha, maelezo ambayo yamewasilishwa kwenye kitabu hiki ni finyu sana hasa katika sehemu za fasihi simulizi. Maelezo haya yanamwacha msomaji na maswali zaidi kuliko majibu.

2.6 Maelezo Tatanishi ya Istilahi/Msamiati na Idadi ya Tanzu

Kwa mujibu wa Kobia katika Njogu et al. (2006), udhaifu wa vitabu vya fasihi simulizi vilivyochapishwa ni maelezo hafifu na wakati mwingine kukanganya kuhusu vipera mbalimbali vya fasihi simulizi. Waandishi wa vitabu vinne vilivyorejelewa katika utafiti huu wametumia istilahi kwa maana tofauti na hivyo zinaweza kuibua utata kwa wasomaji. Kwanza, Mumbo & Ngamia (2005) wanarejelea tanzu kuu za fasihi simulizi kuwa ni vipera vya fasihi simulizi ambapo wanaeleza kuwa vipera vya fasihi simulizi ni sita: mazungumzo, ushairi, semi, masimulizi, hadithi, maigizo na ngomezi. Kando na hayo, vijitanzu vinavyopatikana chini ya tanzu kuu ambavyo waandishi hawa wawili walirejelea kuwa ni vipera pia vimetajwa kuwa vipera. Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa Mumbo na Ngamia walirejelea tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi kuwa vipera. Ni wazi kuwa hakuna tofauti bainifu au maana bayana ya tanzu na vipera.

Kwa misingi ya nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, vifaa (vitabu) viwasilishe dhana zisizo changamano. Neno kipera ni changamano katika muktadha huu kwani sio wazi iwapo ni utanzu au ni kijitanzu cha fasihi simulizi.

Kwa mujibu wa Kenya Literature Bureau (2009) katika Kiswahili Kitukuzwe kwa kidato cha nne, hakuna matumizi ya istilahi tanzu au vipera kwa kina. Katika maelezo yote ya tanzu kuu hakuna sehemu iliyotaja moja kwa moja kuwa hiki ni kijitanzu cha utanzu fulani ila inaelezwa tu moja kwa moja maana ya utanzu au kijitanzu, mfano;

“...maigizo ni sanaa ya maonyesho ya kuiga matendo ya watu au viumbe wengine ili kuburudisha au kutoa ujumbe fulani katika jamii (uk 141).”

Kutokana na vitabu hivi viwili vilivyotajwa (Johari ya Kiswahili na Kiswahili Kitukuzwe) imeonyesha wazi kuwa dhana ya tanzu, vipera na vijitanzu haijawekwa wazi hivyo basi kuna utata wa maana na matumizi.

Kyung (2004) anaeleza kuwa kuna dhana za kiasili za masimulizi ya Kiswahili ambayo yana maana inayoingiliana. Mfano: `ngano`, `hadithi`, `kisa`, `hekaya` na `masimulizi`. Anaongeza kuwa neno ngano limetumiwa kurejelea masimulizi ya fasihi simulizi. Kuna utata wa matumizi ya istilahi ngano, hadithi na masimulizi kwa mujibu wa mwandishi huyu.

Kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, matini kwenye vifaa vya kufundishia inastahili kuelezewa kwa njia iliyo wazi bila utata wowote. Iwapo utata wa dhana utakuwepo basi marekebisho ya vifaa hivyo yanastahili kufanywa ili kuondoa makosa hayo.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) katika Chemchemi za Kiswahili, istilahi hadithi inaelezwa kuwa na maana sawa na ngano (uk 15) ilhali katika kitabu kiki hiki katika mchoro ulioko ukurasa huo huo masimulizi ni kisawe cha hadithi. Hivyo basi ina maana kuwa maneno haya matatu yana maana sawa kwa mujibu wa maelezo ya mwandishi huyu.

Katika kitabu hiki, ngano ni tanzu kuu ilhali katika vitabu vingine ni kijitanzu chini ya tanzu kuu kama vile katika Kiswahili Kitukuzwe na Johari ya Kiswahili. Kuna mchanganyiko wa matumizi na maana ya ngano katika vitabu vitatu vilivyorejelewa Vijitanzu vya fasihi simulizi vinarejelewa kwa jina vipera katika Chemchemi za Kiswahili. Utanzu wa semi una vipera kadha kama: methali, misimu na kadhalika (uk 37).

Idadi ya tanzu inaelezewa kwa njia isiyo wazi katika Chemchemi za Kiswahili ambapo fasihi simulizi inaelezewa kuwa na tanzu tano kuu: hadithi/ngano, maigizo, semi, ushairi na mazungumzo.

Zaidi ya hayo, kwa kufuatia msingi wa kuainisha tanzu zinakuwa ni nne ambazo pia zipo katika mchoro (uk 15): hadithi, semi, maigizo na ushairi.

Kwa mujibu wa misingi ya nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, vifaa viwe na usawa na maelezo wazi yasiyo changamano ili kueleweka na wasomaji.

Istilahi vipera, tanzu na vijitanzu inaibua utata wa aina kuu za fasihi simulizi na uainisho chini ya aina hizi kuu. Usawa huu unaweza tu kuwepo kupitia marekebisho ya makosa kwa kuchapisha matoleo mapya na kuzingatia istilahi mwafaka.

2.7 Mabadiliko ya Matoleo na Urekebisho wa Makosa

Kwa mujibu wa Krashen (1982) makosa katika vifaa vya kufundishia yanastahili kurekebishwa ili dhana zinazopokezwa kwa mwanafunzi ziwe wazi. Vifaa vinastahili kuvutia na kuwa na maelezo sahili. Vitabu vya kufundishia Kiswahili vimerejelewa kuwa vifaa katika muktadha huu na ambavyo vimekuwa na matoleo tofauti yanayochukuliwa kuwa yanafanywa ili kuboresha matini katika vitabu hivi. Kwa mfano, kitabu cha Kiswahili Kitukuzwe kimekuwa na matoleo kuanzia toleo la kwanza (1989) hadi sasa toleo la nne limetolewa mara tatu: mara ya kwanza (2009) na mara mbili baadaye (2011).

Hii ni ithibati kuwa vitabu vinafanyiwa marekebisho na kuboreshwa zaidi ili kuweza kuambatana na mahitaji ya silabasi mpya na mtaala. Ijapokuwa baadhi ya vitabu havizingatii sehemu zote na zinabaki zilivyokuwa awali, utafiti huu ulilenga zaidi kuangazia mada za uainishaji wa fasihi simulizi na kuchunguza iwapo yapo marekebisho yoyote ya makosa. Kitabu cha Kiswahili Fasaha ndicho kilitumiwa kuangazia marekebisho ya makosa au uboreshaji wa dhana za fasihi simulizi.

Kiswahili Fasaha kwa kidato cha nne kina matoleo mawili (2005) na (2015) mtawalia. Kwa kuangazia yaliyomo, mabadiliko yalifanywa kwa kutenga matini katika sura ishirini na sita ambazo awali (2005) hazikuwepo na wakati huo yaliyomo yalirejelewa kama faharasa. Isitoshe, wakati huo matini za kitabu hiki ziligawika katika sehemu kumi na nane tu.

Zaidi ya hayo, stadi nne kuu: kusikiliza na kuzungumza, sarufi na matumizi ya lugha, kusoma na kuandika zinazorejelewa katika silabasi kwa shule za upili za kujifunzia hazikuwepo kwenye kitabu cha Kiswahili Fasaha (2005). Hivyo basi ingekuwa vigumu kujua sehemu zinazoeleza kuhusu uainishaji wa fasihi simulizi na maelezo ya tanzu na vijitanzu vyake.

Kutokana na vitabu tofauti vilivyoidhinishwa kufundisha fasihi simulizi kwa shule za upili nchini Kenya, fasihi simulizi ni sehemu muhimu ya somo la Kiswahili. Sehemu hii huchangia matokeo ya mwanafunzi katika mitihani. Vitabu vyote vinastahili kuwa na matini wazi zisizo na utata ili wanafunzi waelewe wanaposoma. Iwapo vitabu vya kufundishia havitaratibiwa upya na kufanyiwa marekebisho basi dhana tata zitabakia kuwepo. Dhana hizi tata zitaibua changamoto kwa wanafunzi wanapojibu maswali ya idadi ya tanzu, uainishaji wa vijitanzu, maana ya istilahi mbalimbali na vigezo vya kuainisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

Marekebisho haya yakifanyika vifaa hivi vya kufundishia vitakuwa vina dhana sawa na zile zinazowasilishwa na silabasi iliyokubalika nchini. Hivyo basi walimu nao pia watakuwa na umilisi ufaao wa dhana za kuwasilishia wanafunzi.

Fasihi simulizi ni pana. Fasihi simulizi hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Jamii tofauti huwasilisha idadi tofauti ya tanzu kwani waandishi wake wanafuata misingi tofauti.

Idadi hizi tofauti na istilahi kinzani zinakubalika kwani jamii hizi ni tofauti na zina desturi, mila na tamaduni zake tofauti. Katika silabasi ya kufundisha nchini, dhana zote kwenye vitabu zinastahili kuwa sawa ili kuafiki msingi wa nadharia ya Krashen kuwa vifaa viwasilishe matini kwa njia sahili na wazi isiyoibua utata.

Nadharia ya tanzu pia imeakisi kuwa tanzu zipo ulimwenguni na kuwa zina sifa bainifu na uwezo wa kujisimamia kwani zinaundwa kwa vigezo au mifumo mahsusi.

Vitabu vilivoidhinishwa kufundishia kwenye shule zina uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Tatizo kuu linaloibuka ni la uwasilishaji wa idadi tofauti, kuingiliana kwa tanzu na ukinzano wa istilahi zinazotumiwa. Iwapo utata huu utatatuliwa na sheria kufuatwa za misingi itakayotumiwa kuainisha fasihi simulizi tatizo hili litaondolewa. Misingi inayofuatwa ya kuchapisha, kuandika au ata kufundisha fasihi simulizi ioane au ifanane na maelekezo ya silabasi yalivyo.

2.8 Hitimisho

Sura ya pili imechunguza uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Uchunguzi huu umelenga vitabu vifuatavyo vya kufundisha vilivoidhinishwa kwa shule za upili nchini Kenya:

- i. Kiswahili Kitukuzwe

- ii. Chemchemi za Kiswahili
- iii. Johari ya Kiswahili
- iv. Kiswahili Fasaha

Kutokana na vitabu hivi teule, uainishaji umedhihirika kuwa unaotofautiana kwa misingi ya mihimili ya nadharia ya Tazungu na nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili.

Sura hii pia imeshughulikia tanzu kuu na vijitanzu vya fasihi simulizi vyenye utata, maelezo tatanishi ya istilahi na idadi ya tanzu na mabadiliko ya matoleo na marekebisho ya makosa. Sura inayofuata inahusu vigezo vya uainishaji au misingi inayofuatwa katika uainishaji wa fasihi simulizi.

SURA YA TATU: VIGEZO VYA KUAINISHA TANZU NA VIJITANZU VYA FASIHI SIMULIZI

3.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia, imeshughulikia tofauti zilizopo katika uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika vitabu. Vitabu vilivyorejelewa ni vinne vilivyoidhinishwa kufundisha Kiswahili kwa shule za upili nchini Kenya. Kwa misingi ya nadharia ya Tanzu, uainishaji wa tanzu upo na unafuatia misingi na vigezo mahsusi.

Sura hii inachunguza misingi au vigezo vya uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Data hii ilitokana na vitabu vya Kiswahili na tafiti za fasihi. Sehemu hii pia inaangazia mbinu za ziada za kufundisha fasihi simulizi. Nadharia ya Tanzu itatumika kwa kuangazia mhimili wa mfumo (misingi au vigezo) unaofafanua muundo wa tanzu. Mhimili ya nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili itaangaziwa katika kueleza vigezo mbalimbali vinavyopelekea uainishaji wa fasihi simulizi.

3.1.1 Dhana ya Misingi na Vigezo katika Uainishaji

Chandler (1997) anaeleza kuwa, tangu kipindi cha urasimi, kazi za kifasihi ziliainishwa katika makundi ambayo awali yalikuwa ushairi, nathari na maigizo. Misingi au vigezo ni jinsi aina au makundi huundwa. Hii inarejelea mambo yanayozingatiwa katika kutengeneza makundi mbalimbali. Kulingana na kamusi ya TUKI (2019) msingi pia ni chanzo, asili, sababu, kiini au mwanzo wa kitu fulani. Kamusi hii inaeleza kigezo kuwa kanuni au sifa inayokubalika kama msingi wa kupimia au kutolea uamuzi wa jambo. Vigezo vya uainishaji vimeelezewa na waandishi na wataalam mbalimbali na vinajadiliwa kwa kuangazia vigezo vya kuainisha fasihi, tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

3.1.2 Vigezo vya Kuainisha Fasihi

Kwa mujibu wa nadharia ya Tazunguzi, tanzu zinaweza kugawika katika makundi. Fasihi imegawika katika aina mbili kuu (fasihi andishi na fasihi simulizi) kwa kigezo cha uwasilishaji. Matei (2011) anaeleza kuwa, fasihi imegawanywa kulingana na jinsi inavyowasilishwa na kuhifadhiwa. Aliongeza kuwa, fasihi simulizi hubuniwa na kuhifadhiwa akilini kisha kuwasilishwa kwa masimulizi, mazungumzo ya kisanaa, kuimba, kughani, kuigiza na kukariri kwa hadhira. Nayo fasihi andishi huhifadhiwa katika maandishi na kusambazwa kupitia kwa maandishi.

Ben-Amos (1976) anaeleza mtindo wa kuwasilisha ni mojawapo ya vigezo vya kugawa tanzu za fasihi simulizi. Masimulizi kwa mfano yana mtindo tofauti yakilinganishwa na nyimbo au mashairi simulizi ya kukaririwa. Mtindo wa kuwasilisha ni mojawapo ya vigezo muhimu vya kuainisha fasihi simulizi.

Wamitila (2003) Fasihi hutofautiana kwa njia moja kuu ambayo ni uwasilishaji. Kutokana na uwasilishaji kuna fasihi andishi inayowasilishwa kwa maandishi na fasihi simulizi inayowasilishwa kwa mdomo au kupokezana kwa masimulizi (uk 4). Kutokana na maelezo ya Wamitila fasihi imegawika kwa makundi mawili kwa kigezo cha uwasilishaji. Naye M'ngaruthi (2008) anajadili kuwa vigezo vikuu vinavyozingatiwa katika uainishaji wa fasihi ni uwasilishaji kwa hadhira na uhifadhi.

Kigezo cha jinsi dhana inavyowasilishwa ni muhimu sana katika kuelewa fasihi na vipengele vyake vyote. Kulingana TUKI (2019) uwasilishaji ni hali ya kutoa maoni au mawazo kwa watu wengine. Vitabu tofauti vya kufundishia somo la Kiswahili kwa shule za upili vimewasilisha fasihi na vipengele vyake kwa misingi tofauti ambayo hutofautiana kutoka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine.

Tofauti hizi za vigezo vya uwasilishaji wa dhana ndizo huenda zinapelekea kuwepo kwa tofauti ya idadi ya tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

Uwasilishaji wa vifaa kwa misingi ya nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa lugha ya pili unastahili kuwa sahili na usio changamano ili vifaa vieleweke na msomaji. Uainishaji wa fasihi simulizi uwe wazi bila ukinzano wa misingi au vigezo vya kuainisha kwenye vifaa (vitabu) vya wanafunzi.

3.2 Vigezo vya Kuainisha Tanzu na Vijitanzu vya Fasihi Simulizi

Fasihi simulizi huainishwa kwa misingi inayotofautiana. Tofauti hizi zinatokana na wataalam mbalimbali kufuata vigezo vinavyotofautiana kuainisha tanzu hizi. Odeo (2006) kila utanzu wa fasihi simulizi unatambulika kwa mujibu wa upekee wa fani, miundo na mtindo. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu kila utanzu na kijitanzu kina sifa bainifu zilizo tofauti na tanzu zingine. Hivyo basi kuvipa vitanzu vya fasihi simulizi uwezo wa kuwa katika makundi tofauti na kuwa na misingi maalum ya kuainishwa.

Kuwepo kwa misingi tofauti ya kubainisha tanzu za fasihi simulizi ni ithibati kuwa tanzu zina sifa bainifu. Ben-Amos (1976) anaeleza misingi ya kugawa tanzu za fasihi simulizi katika makundi. Misingi hii ni: kulinganisha na kulinganua, sifa bainifu za utanzu, kuchunguza mtindo wa uwasilishaji, muundo wa utanzu miongoni mwa vigezo vinginevyo.

Kwa mujibu wa Magambo (2019) kuna aina sita za nyimbo kutegemea misimbo tofauti katika tamasha za muziki. Anaeleza kuwa makundi haya ni kutokana na vigezo vya:

- i. Umri
- ii. Maudhui
- iii. Maeneo
- iv. Jinsia
- v. Idadi

vi. Mbinu ya uwasilishaji

Odeo (2006) anaeleza kuwa matumizi ya nadharia tofauti huleta utata wa uainishaji. Anaongeza kuwa, japo vitabu vya shule vina maelezo, uwezo wa walimu wa kuainisha kazi za fasihi umelemazwa na msingi dhaifu wa kinadharia.

Misingi hii ya uainishaji ni kama: Uwasilishaji, wahusika, lugha, muundo na maudhui. Baadhi ya misingi hii imejadiliwa kwa kurejelea wataalam mbalimbali.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003a) zipo aina mbalimbali za ngano kutegemea: maudhui yake, muundo wake, wahusika wake na kadhalika. Kutokana na misingi hii ameeleza aina kuu za ngano kuwa: ngano za mashujaa au mighani, ngano za wanyama au hurafa, ngano za usuli au chanzo, visasili, ngano za mazimwi na ngano za mtanziko. Kando na hayo anaeleza kuwa ngano huwa na sifa kama: mianzo maalum, urudiaji, matumizi ya nyimbo, mtuo wa kidrama, matumizi ya tanakali za sauti, matumizi ya ishara, mbinu za ufaraguzi, matumizi ya maswali na miishio maalum. Anaongeza kuwa katika uchambuzi wa ngano za fasihi simulizi mambo yafuatayo yanapaswa kuchunguzwa: wahusika ni nani? muundo au msuko, taharuki, maudhui na adili au mafunzo ya ngano.

Kwa msingi wa maelezo ya Wamitila, tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi vina uwezo wa kugawika kwa makundi kufuatia misingi mbalimbali mahsusi.

Misingi hii ni kama mianzo maalum, urudiaji, miishio maalum na kadhalika. Haya ni sawa na misingi ya Ben-Amos (1976) anayedai kuwa vigezo kama mianzo na miishio ya tanzu inatumiwa kuainisha tanzu.

Maelezo haya ni ithibati tosha kuwa tanzu zipo ulimwenguni na uainishaji katika makundi unafanyika tangu enzi za urasimi kwa mujibu wa Chandler (1997). Hivyo basi misingi hii inayoelezwa na waandishi tofauti ipo.

Tatizo linalojitokeza katika baadhi ya vigezo vya uainishaji ni kuwa hakuna uwezo wa kupima baadhi ya misingi inayoelezwa. Baadhi ya misingi isiyo wazi ni kama ufupi na urefu wa tanzu. Mwandishi hawezi kutumia kigezo hiki kwani hakina mashiko na hakipimiki. Misingi/ vigezo vya uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi ni kama ifuatayo:

3.2.1 Uwasilishaji

Kwa mujibu wa Mng'aruthi (2008), uainishaji unazingatia sifa kama vile uwasilishaji. Uwasilishaji waweza kuwa kiutambaji, kishairi, kimafumbo, kimaigizo au kimazungumzo. Kutokana na sifa hizi kuna vipera vitano vikuu vya fasihi simulizi. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, hii ni ithibati kuwa fasihi ina uwezo wa kugawika kwa tanzu na kuwa tanzu zipo ulimwenguni.

Vipera hivi kwa mujibu wa Mng'aruthi (2008) ni:

- i. Hadithi (kiutambaji)
- ii. Ushairi (kishairi)
- iii. Semi (kimafumbo)
- iv. Maigizo (kimaigizo)
- v. Mazungumzo (kimazungumzo)

Kutokana na misingi hii ya uainishaji utanzu wa ngomezi haujaangaziwa popote. Kwa misingi ya nadharia ya ujifunzaji na upokeaji wa lugha ya pili, makosa yanayohitaji kurekebishwa ni yanayotokea mara nyingi na yanastahili kupewa kipaumbele.

Si uainishaji huu pekee uliokosa utanzu wa ngomezi bali pia kitabu cha Wamitila (2003) kimeainisha tanzu kuu nne pekee. Kitabu hiki hakijahusisha ngomezi popote. Utanzu wa ngomezi huwasilishwa kwa mapigo ya ngoma.

Kwa mujibu wa silabasi (2002), tanzu za fasihi simulizi ni sita ikiwepo ngomezi. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya tanzu, kuna mifumo bainifu inayofuatwa katika uainishaji wa tanzu. Uainishaji huu umeegemea kigezo cha namna au jinsi ya kuwasilisha tanzu za fasihi simulizi. Wamitila (2003) anaeleza uainishaji hutegemea vipengele kama vile njia ya kuwasilisha. Anarejelea uwasilishaji kwa:

- i. Kusimuliwa
- ii. Kuigizwa
- iii. Kuzungumzwa

Msingi huu sio kamilifu kwani baadhi ya tanzu kama vile ngomezi na ushairi haziwasilishwi kwa njia zilizotajwa. Njia tatu zinazotajwa zinarejelea hadithi, maigizo na semi pekee. Kwa mujibu wa misingi ya nadharia ya Krashen (1982) vifaa vinastahili kuwasilisha matini kwa njia rahisi isiyoibua utata kwa msomaji.

Wamitila (2003) anawasilisha tanzu nne kuu kufuatia misingi mitatu aliyoeleza ya uainishaji wa fasihi simulizi tofauti na ilivyo kwenye silabasi ya Kiswahili iliyo na tanzu sita. Matini za kufundishia fasihi simulizi yafaa zioane na silabasi ili pasiwe na utata wa maelezo na uwasilishaji wa dhana mbalimbali.

Maghani kwa mujibu wa Wamitila (k.h.j) ni ushairi. Ushairi huu anautofautisha kwa msingi wa uwasilishaji wake. Kuna aina mbili kuu za maghani: maghani ya kawaida na maghani simulizi. Maghani ya kawaida hukaririwa au kutolewa kwa kalima ilhali maghani simulizi husimuliwa kwa kurejelea kisa au hadithi na yanaweza kuambatishwa na muziki wa ala. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, tanzu zina sifa bainifu na uwezo wa kujisimamia bila kuingiliana. Hivyo basi maghani yaelezwe kama kipera cha ushairi na sio maigizo.

Kwa mujibu wa Murimi, J., Obuchi, S., Kandagor, M. (2016) jinsi ya utendaji ni msingi wa kuainisha tanzu na vipera vya fasihi simulizi. Utanzu wa hadithi ulipata jina hili kutokana na kuwasilishwa kwa njia ya kusimuliwa. Maghani yalipata jina lake kutokana na kuwa yaliwasilishwa kwa njia ya kughaniwa.

Kwa misingi ya nadharia ya utanzu kuna mifumo au vigezo vinavyofuatwa katika kuainisha tanzu. Vigezo hivi hutofautiana kwa misingi ya wataalam tofauti kugemea nadharia tofauti wanapoainisha tanzu. Vigezo hivi mbalimbali hupelekea tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi zinazowasilishwa kwenye vitabu tofauti.

Kwa kufuatia msingi huu wa uwasilishaji tatizo linaibuka la vijitanzu tofauti kuwasilishwa kwa njia sawa na vipo katika migao tofauti ya tanzu. Kwa mfano, mawaidha yatawasilishwa kimazungumzo na mafumbo kwa njia hiyo hiyo japokuwa hivi ni vipera vya mazungumzo na semi mtawalia. Dhana ya uwezo wa tanzu kuingiliana inajitokeza (Stam, 2000). Uwasilishaji ule ule wa tanzu moja unafanywa kwa tanzu ingine tofauti. Kuingiliana huku kwa tanzu kunaibua utata katika mikakati ya ufundishaji na usomaji.

3.2.2 Muundo/ Umbo

Kwa mujibu wa Mngaruthi (2008) uainishaji wa vipera vya fasihi simulizi unaweza kufanywa kwa kuongozwa na kigezo cha urefu na ufupi wa tanzu.

Kwa kigezo hiki fasihi imegawika katika vikundi vitatu vikuu:

- i. Tanzu ndefu
- ii. Tanzu fupi
- iii. Ushairi

Tanzu ndefu hujumlisha aina zote za masimulizi au hadithi. Aliongeza kuwa nazo tanzu fupi ni kazi za fasihi simulizi ambazo ni fupi zikilinganishwa na zinazopatikana katika tanzu ndefu mfano kundi la semi na mazungumzo. Stam (2000) anaeleza kuwa tatizo moja la ufafanuzi wa tanzu ni kufuata kigezo cha urefu na ufupi wa tanzu.

Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, tunaibua swali je, tanzu zinajisimamia au zinaingiliana? Kufuatia maelezo haya ya umbo dhana ya mwingiliano wa tanzu linajitokeza kwani uwezo wa kupima urefu na ufupi wa tanzu utatofautiana kutoka kwa mtaalam mmoja hadi mwingine.

Mngaruthi (2008) anaeleza kuwa, semi zimegawika katika: Methali, misemo, misimi, vitanza ndimi, mafumbo na lakabu. Mazungumzo yamegawika katika vichekesho, malumbano ya utani, sogu na ulumbi.

Nao ushairi unaelezwa kuwa unajumlisha kazi zote zilizowasilishwa kwa mtindo wa kishairi kama vile kukaririwa, kuimbwa au kughaniwa. Mifano ya ushairi ni mashairi, nyimbo na maghani.

Maelezo haya yana udhaifu kwa mujibu wa Mngaruthi (2008) ambaye anasisitiza kuwa urefu na ufupi wa utanzu haujawekewa mipaka na huweza kutegemea maoni ya mtu binafsi. Anazidi kueleza udhaifu kwa kutaja mifano kama: Kuna hadithi zenye urefu sawa na sogu na ambayo inaelezwa kama tanzu fupi. Kando na hayo, kipera cha maigizo kimepuuzwa na hakijaangaziwa popote.

Kulingana naye maigizo hujumuisha ngonjera, sanaa za maonyesho, sarakasi, majigambo, vichekesho, ngomezi, malumbano ya utani, sogu, mawaidha na maigizo ya watoto.

Kwa misingi ya nadharia ya tanzu, tanzu hujisimamia kwa maana na sifa bainifu. Hivyo basi makundi sio haya matatu tu yaliyoorodheshwa. Kigezo hiki cha uainishaji kinaonyesha udhaifu mkubwa kwani baadhi ya tanzu kama ngomezi zimepuuzwa kama tanzu kuu. Zaidi ni kuwa hakuna maelezo toshelevu kuhusu tanzu zilizoachwa. Kuongezea ni kuwa, urefu na ufupi wa tanzu sio bainifu.

Baadhi ya tanzu zinaingiliana kwa misingi ya kigezo hiki. Isitoshe, tanzu zilizorejelewa kuwa ni ndefu zimeelezwa kwa njia finyu sana bila ufafanuzi wa kina. Hii inapinga mhimili wa nadharia ya Tanzu kuwa tanzu zipo ulimwenguni na zina sifa bainifu na uwezo wa kujisimamia kimaana.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003b) msingi mkuu wa kuainisha au kupanga makundi ya fasihi simulizi ni mtindo wake. Anaeleza kuwa tanzu zinatokana na sifa za kimtindo kama ufupi wa kimuundo kwa kiwango kikubwa. Kigezo hiki kulingana naye kinaibua utanzu wa semi.

Maelezo haya yana udhaifu, kwani ufupi wa kimuundo haupo kwa semi pekee. Urefu wa mafumbo unaweza kuwa sawa na urefu wa sogu na hivi ni vipera vya tanzu mbili tofauti. Hivyo basi, sio sahihi kugegemea kigezo cha ufupi au urefu wa tanzu na vijitanzu. Kwa mujibu wa Stam (2000) ufafanuzi wa tanzu unaweza kutatiza. Anazidi kubainisha baadhi ya matatizo ya ufafanuzi wa tanzu kwa mtazamo wa filamu kama ugani ambao anaueleza kama urefu au ufupi wa tanzu. Anaongeza kuwa, japo tanzu zina uwezo wa kuingiliana ni vyema zaidi iwapo kila utanzu utachunguzwa na kufafanuliwa kivyake.

Kwa misingi wa nadharia ya Tanzu, tanzu zipo ulimwenguni na zinaweza kujisimamia ila sio kwa kuangazia vigezo visivyopimika kama urefu na ufupi wa tanzu. Kigezo cha umbo la ufupi na urefu wa tanzu kitaibua ukinzano na utata wa dhana kwenye vitabu ambao kwa msingi wa nadharia ya Krashen vifaa vya kufundishia havistahili kuwasilishwa kwa njia changamano. Uwasilishaji unastahili kufanywa kwa uwazi bila makosa ya uwasilishaji wa dhana tofauti.

Muiruri (2006) anadai kuwa tanzu na vipera tofauti huwa na (muundo) namna ya pekee ya kuanza:

Utanzu wa Hadithi/ Masimulizi

Msimulizi: Hadithi! Hadithi!

Hadhira: Hadithi njoo!

Utanzu wa semi – Vitendawili

Mtegaji: Kitendawili!

Hadhira: Tega!

Anaongeza vilevile kuwa, uainishaji wa tanzu upo kwa msingi wa umbo la viishio maalum:

- i. Hadithi/ masimulizi yaweza kuishia kwa ``...wakaishi raha mustarehe``.
- ii. Kitendawili kinaweza kuishia kwa mtegaji kusema ``...nilienda Moyale watu wa huko wakaniambia...``.

Tanzu na vijitanzu tofauti vya fasihi simulizi huwa na umbo mahsusini ambalo huzibainisha na kuzipa uwezo wa kujisimamia. Nadharia ya Utanzu inaonyesha wazi kuwa vipera vya fasihi simulizi vina sifa bainifu. Sifa hizi bainifu zinaweza kujitokeza kwa umbo au muundo.

Ben-Amos (1976) anaeleza kuwa, tanzu tofauti za fasihi simulizi huwa na mianzo na miishio bainifu. Hadithi katika mifano iliyotajwa ina miishio inayoitofautisha na vitendawili na kuifanya kuwa na uwezo wa kujisimamia kama tanzu bainifu.

3.2.3 Wahusika

Kyung (2004) anadai kuwa kigezo cha wahusika wakuu kinaweza kutumiwa katika masimulizi au hadithi za Kiswahili. Anaeleza kuwa baadhi ya hadithi zilihusu binadamu ilhali zingine zilihusu wanyama. Anaongeza kuwa ni vigumu kubaini aina ya hadithi kwa kigezo hiki cha wahusika. Anamnukuu Mbughuni (1987) anayedai kuwa hadithi zilizohusu wanyama zilitofautiana na hadithi za binadamu. Anaongeza kuwa kuna tofauti bainifu kati ya hadithi hizi, hivyo basi zichukuliwe kuwa hadithi mbili tofauti. Anaonyesha kuwa ngano za wanyama ni tofauti na za binadamu. Ngano za wanyama ni fupi na zenye utani ikilinganishwa na za binadamu.

Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, tanzu zina sifa bainifu kama ilivyoelezewa. Kuna tofauti kati ya ngano za wanyama na za binadamu. Hii ilidhihirisha kuwa kuna mifumo iliyofuatwa kuunda tanzu au vijitanzu vya fasihi simulizi.

Murimi, J., Obuchi, S., Kandagor, M., (2016) wanadai kuwa wahusika au watendaji ni msingi wa kuainisha fasihi simulizi. Wanaeleza kuwa kila utanzu huhusishwa na watendaji wa hali, jinsia na umri fulani. Mfano: Nyimbo za watoto, watendaji wake ni watoto. Nyimbo za kitamaduni zinaweza kuainishwa kwa misingi ya kijinsia. Wakimnukuu Wamitila (2003b) wanarejelea mfano wa jamii ya Waswahili ambapo Chakacha huhezwa na wanawake na vijana huku vugo ikichezwa na wanawake waliokomaa.

Waliongeza kuwa masimulizi ya aina ya hurafa yalipata jina lake kutokana na wahusika wake kuwa wanyama. Nayo maghani yana wahusika ambao ni mashujaa. Zaidi ya hayo wanarejelea malumbano ya utani kuwa wahusika wake wanatarajiwa kuwa wenye utani.

Kwa mujibu wa nadharia ya Tazunguzi mifumo tofauti hutumiwa katika kutenga tanzu za fasihi simulizi katika makundi mahsusi. Mifumo hii tofauti huonyesha vigezo au misingi ya uainishaji. Kigezo cha aina ya wahusika husaidia katika kuelewa aina ya kijitanzu cha fasihi simulizi.

Matei (2011) anadai kuwa kuna aina tofauti ya wahusika, fanani na hadhira. Kuna wahusika binadamu, wanyama, mazimwi na viumbe visivyo na uhai. Wahusika wanyama walio na sifa za binadamu hutumiwa kimapumbo kukashifu tabia hasi katika jamii. Wahusika binadamu waweza kuwa wa kihistoria walioishi au wa kubuni. Wahusika mazimwi huwa na maumbile ya kiajabu. Wahusika vitu husikika vikizungumza kama binadamu. Mfano: mawe, vibuyu, vyungu na hutenda kama binadamu. Wahusika mizimu ni roho za waliokufa na huonekana zikitembea na kufanya kama binadamu. Wahusika miungu huaminika kuwa na uwezo mkubwa dhidi ya binadamu.

Wahusika ni kigezo kikuu katika kuainisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Kwa mfano, hurafa na hekaya hutofautishwa kwa vigezo tofauti kama vile wahusika waliohusishwa kwenye hadithi. Kwa mujibu wa nadharia ya tanzu, mifumo tofauti hutumiwa kugawa makundi ya fasihi simulizi.

3.2.4 Maudhui

Kwa mujibu wa TUKI (2019), maudhui ni mambo muhimu yanayoelezwa kama vile katika hadithi, riwaya, hotuba au makala. Wamitila (2003b) anaeleza kuwa visasili na ngano za usuli ni vipera tofauti vya hadithi kwa mujibu wa maudhui au aina ya chanzo kinachoelezwa. Visasili husimulia mianzo au asili ya vitu/ watu kwa mtazamo wa kihistoria. Mfano, asili ya lugha, jua, kifo au kabila. Ngano za usuli husimulia na kuelezea chanzo cha tabia, hali au tukio fulani. Mfano: Kwa nini sungura ana masikio marefu au kwa nini kuku huchakura.

Kwa mujibu wa Matei (2011), visasili ni hadithi za kale zilizoonyesha asili/ chanzo cha jamii, kifo, milima na mito. Ngano za usuli huelezea sababu za kuwepo kwa hali, tabia ama mahusiano fulani. Mfano: Kwa nini fisi hula mizoga au kwa nini mwewe hula vifaranga wa kuku.

Kwa mujibu wa maelezo haya, ngano za usuli na visasili ni vijitanzu vya hadithi ambavyo vina sifa bainifu. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, tanzu zina uwezo wa kujisimamia kutokana na sifa zake bainifu. Hivyo basi kwa kigezo cha maudhui ya chanzo cha tabia kuna tofauti kati ya kijitanzu cha kisasili na ngano za usuli.

Magambo, E., Simiyu, F., Amukowa, (2019) wanadai kuwa, uainishaji wa nyimbo unaweza kufanywa kimaudhui. Mfano: **nyimbo za kazi**. Hizi zinahusu utendaji.

Mfano:

*``tuyafyeke haya magugu, tuyafyeke,
kwa miundi tuyafyeke, tuyafyeke,
kwa pamoja tuyafyeke,
kwa nguvu tuyafyekee...``*

Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, tanzu zina vigezo au mifumo mahsusi. Nyimbo ni kijitanzu cha fasihi simulizi ambacho kinaweza kuainishwa kwa misingi mbalimbali. Mfano, wimbo huu wa kazi unahimiza watu washirikiane pamoja wafanye kazi. Kigezo cha maudhui au ujumbe mkuu kinajitokeza katika msingi huu wa uainishaji.

Magambo (k.h.j) anazidi kueleza baadhi ya nyimbo zinaibua **maudhui ya mapenzi**.

Mfano:

``zilizopendwa``.

``Nakulia ooh Susana,

...nakulia wewe Susana

...nakulia, nakulia, nakulia ooh Susana,``

Kwenye tamasha hizo, nyimbo za kumsifu Mungu zilidhihirisha **maudhui ya dini**.

Hapa nyimbo za kikristo na za kiislamu pia zilitofautishwa kwa maleba na vifaa vilivyotumika.

Mfano:

``Ninaona! Ninaona!

Bwana Yesu ameketi kitini mawinguni,

Ninaona! Ninaona!``

Katika tamasha za muziki kulikuwa na nyimbo za **maudhui ya sifa**. Hizi ziliimbwa kumiminia watu sifa au makundi kwa mchango wao katika jamii. Mfano:

*``Hapa shuleni kielimu mengi tunayapokea,
Ila pasipo mwalimu katu tusingeyaweza,
Ila pasipo mwalimu katu tusingeyaweza...``*

Kwa mujibu wa Magambo (2019), maudhui ya upashaji tohara yalijitokeza katika nyimbo za nyiso ambazo zilisheni katika tamasha. Akimnukuu Wanjala (2007), anadai kuwa **nyimbo za tohara** huwa fupi na huwa na umbo maalum na mkarara.

Mfano:

*``Ulisema,
Tohara, sherehe ya tohara eeh!
Sherehe yangu ya tohara ni nzuri
Ndio sherehe ya tohara ni yetu``*

Wimbo huu wa tohara unaibua maudhui yanayotofautiana na maudhui katika nyimbo zingine. Wimbo umeonyesha mtu jasiri anayefurahia utamaduni huu wa upashaji tohara katika jamii yake.

Kwa mujibu wa Murimi, J., Obuchi, S., Kandagor, M., (2016) tunaweza kupata yaliyomo katika kazi husika ya fasihi simulizi yakitumika kuiainisha. Mfano:

Utanzu wa nyimbo

- i. *Nyimbo za hodiya* huonyesha maudhui ya kazi.
- ii. *Nyiso* huonyesha maudhui ya kitamaduni ya upashaji tohara.

Utanzu wa Semi

Methali hurejelea ujumbe mahsusi.

- i. ‘Liandikwalo halifutiki’ hurejelea maudhui ya majaliwa.
- ii. ‘Asiyesikia la mkuu huvunjika guu’ hurejelea maudhui ya maadili na makanyo.

Mifano iliyoielezwa inabainisha wazi kuwa kigezo cha maudhui kina utata. Kwa sababu tanzu tofauti zinaweza kuwa na maudhui sawa. Hivyo basi kigezo hiki cha maudhui ni hafifu kutumiwa kama msingi wa kuainisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi kwa sababu ya mwingiliano wa maudhui katika vijitanzu mbalimbali. Kwa misingi ya nadharia ya utanzu, kuna mwingiliano wa tanzu tukirejelea kigezo hiki.

3.2.5 Wakati na Mahali

Murimi, J., Obuchi, S., Kandagor, M., (2016) wanaeleza kuwa msingi wa wakati huhusishwa na kipindi maalum. Mfano kipera cha nyimbo, kuna zilizorejelewa wakati wa kupashwa tohara. Kuna nyimbo za wakati wa vita, zingine za wakati wa kazi. Kipera cha soga hutumiwa wakati wa mapumziko.

Nyimbo zina uwezo wa kuainishwa kwa msingi wa wakati zinapotumiwa, kwa sababu baadhi ya nyimbo huchukua wakati mahususi kuwasilishwa. Mfano, kipera cha soga hakiwezi kuwasilishwa asubuhi kabla ya kufanya kazi. Murimi na wengine (k.h.j) wanaeleza kuwa fasihi simulizi iliweza kuainishwa kwa msingi wa mahali inapotendeka. Mfano, nyimbo za jandoni zitaitwa hodiya. Nyimbo za matangani zitaitwa mbolezi na nyimbo za harusini ni za harusi.

Kwa mujibu wa kigezo hiki utendaji wa fasihi simulizi unaangaziwa kiwakati na mahali pa kuwasilishia. Huu ni mfumo wa kuainisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Mfumo huu ni kati ya vigezo vinavyoelezewa na Ben-Amos (1976) kuwa vya kugawa tanzu. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu, kila utanzu wa fasihi simulizi una sifa bainifu zinazoutambulisha. Kigezo hiki kinaonyesha uwezekano wa kugawa tanzu na vijitanzu kwa msingi wa wakati na mahali pa kuwasilishia.

3.2.6 Ala/ Kifaa cha Utendaji

Murimi, J., Obuchi, S., Kandagor, M., (2016) wanaeleza kuwa kifaa kinachotumika kuwasilisha utanzu au kipera fulani hutumika kukipa jina. Mfano, ngoma ya Isukuti ya jamii ya Abaluhya inapata jina kutokana na ngoma za kienyeji. Ngoma hii huchezwa kwa mtindo maalum.

Waliongeza kuwa utanzu wa vugo katika jamii ya Waswahili hujikita katika maandamano kutoka kwa bwana harusi hadi kwa bibi harusi kwa kusudi la kuwasilisha mahari. Wakimnukuu Bazmaleh (2006), vugo huchezwa na wanawake wakiwa wameshika pembe na kigongo kidogo cha kupigia pembe.

Vifaa vya kuwasilishia tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi huweza kusaidia katika ugawaji wa makundi. Utanzu wa ngomezi hurejelea matumizi ya kifaa cha ngoma kinachotumiwa kupitisha ujumbe kwa mapigo yake maalum. Hivyo basi huu waweza kuwa msingi wa kuainisha tanzu na vipera vya fasihi katika makundi.

3.2.7 Umri

Magambo (2019) anadai kuwa tamasha za muziki zimezua uainishaji wa nyimbo ambao waweza kusaidia kufundisha fasihi simulizi shuleni. Nyimbo za watoto ziliimbwa na watoto wa chekechea na shule za msingi katika tamasha za muziki. Akimnukuu Wamitila (2003b), anadai kuwa nyimbo za watoto huimbwa wakati wa michezo ya watoto. Anaongeza kuwa tamasha za muziki huainisha nyimbo za watoto zaidi kwa kigezo cha maleba na mahali wimbo ulirejelea au kuzungumzia. Mfano:

*``Asubuhi na mapema,
Nikienda kule London,
...wakati tunapocheza
Tunacheza na kamba
Tunacheza na mpira...``*

3.3 Mwingiliano wa Tanzu

Kenguru (2013) anaeleza kuwa tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi ni ndogo sana. Aina hizi mbili za fasihi zinakamilishana kimaudhui, kimuundo na fani zingine kwa kiasi kikubwa. Anaongeza kuwa licha ya tofauti zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi, zote zinategemeana kwa mafunzo katika jamii. Mchango wa fasihi simulizi kwa fasihi andishi ni mkubwa sana.

Stam (2000) anaeleza kuwa kuna uwezekano mkubwa wa tanzu kuingiliana. Tanzu za fasihi simulizi zinahusiana kwa kiwango kikubwa na za andishi. Dhana hii inaibua hali ya utegemezi kwani aina hizi mbili za fasihi zinakamilishana. Mfano, vijitanzu vya semi na ushairi katika fasihi simulizi hutumikizwa kwa kiwango kikubwa katika matini za fasihi andishi.

Murimi na wengine (2016) wanaeleza kuwa dhana ya mwingiliano tanzu inaondoa mipaka ya kazi husika na kuiweka wazi. Wakimnukuu Mulokozi (1989) walidai kuwa hakuna utanzu wowote ule unaojitosheleza ila tanzu huingiliana na matumizi ya tanzu zingine ili kufaulisha uwasilishaji wa ujumbe.

Wanaeleza kuwa mwingiliano tanzu husababishwa na:

- i. Mchakato wa mwingiliano matini, unaowezesha kazi husika kukopa, kuiga au kurejelea tanzu zingine bila kuzingatia mipaka ya kiutanzu.
- ii. Tanzu mbalimbali katika kazi moja ya fasihi huingiliana na kuumbana.

- iii. Mwingiliano tanzu hubainishwa na wataalam wa fasihi simulizi kama mtindo wa kawaida katika kumbo za fasihi.

Okemwa (2017) anaeleza kuwa kazi moja ya kifasihi ina sifa za tanzu nyingine ndani yake. Hivyo basi alionyesha kuingiliana kwa matini katika kazi za fasihi. Anaangazia visasili na mchango wake katika uandishi wa fasihi simulizi.

Wanjala (2015) anaeleza kuwa fasihi simulizi inaingiliana na fasihi andishi ili kuweza kukamilika na kutekeleza wajibu wake barabara. Anaongeza kuwa kuna mwingiliano tanzu kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi na kuwa mwingiliano huu unavunja mipaka ya kiutanzu. Anaongeza kuwa neno mwingilianomatini limetumiwa kwa maana ya njia mojawapo inayotumiwa kujenga mwingilianotanzu. Tanzu zinachanganyikana kifani na kimaudhui.

Wanjala (k.h.j) kuna mwingiliano matini kati ya mighani na maghani yaliyotolewa katika mfumo wa mivigha ya *embalu* miongoni mwa Babukusu. Uvunjaji wa mipaka unajitokeza wakati matini simulizi hupangwa katika mistari inayopokezana, kuingiliana na kukamilishana bila kuzingatia mipaka ya kimatini.


Anaongeza kuwa fanani katika majigambo ya khulonga anatumia msemu ``yola nakhufwara engubo ya mango`` kumaanisha tazama nakuvisha nguo ya mango. Jina la mhusika katika utanzu wa ngano linaingizwa katika utanzu wa majigambo ili kuukamilisha.

Mifano hii inadhihirisha kuwa kila utanzu hukopa na kunukuu au kurejelea tanzu zingine ili kukamilika. Hivyo basi hakuna utanzu wa kifasihi ambao ni asilia. Maelezo haya yanapinga misingi ya nadharia ya Tanzu na kuionyesha kuwa ni hafifu na isiyoweza kubainika wazi kisifa.

Aidha, alimnukuu Vansina (1985) anadai kuwa utanzu mmoja unaweza kujibadilisha na kuwa aina mbili tofauti za tanzu katika utendaji. Hili linawezesha utanzu mpya kuibuka. Wanjala (k.h.j) anadai kuwa fanani anaweza kuanza kuimba wimbo ambao unabadilika na kuwa ngano au malumbano ya utani kadri anavyoendelea kughani.

Anaongeza kuwa nyimbo nyingi za mwaka kongwa zilizoimbwa wakati wa kuchomwa kwa kibanda zilijibadilisha na kuwa malumbano ya utani, tarihi, kisasili, ngonjera, maghani na majigambo kwa wakati mmoja.

Jedwali 3.1: Mwingiliano tanzu wa Embalu na Mwakakongwa



Kielelezo hicho kinaonyesha tanzu mbalimbali kuingiliana kupitia mifanyiko tofauti tofauti ya kiutanzu. Tanzu kama malumbano ya utani, majigambo, maghani na nyimbo hubeba tanzu zingine kama methali, misemo, misimu, tarihi, visasili, ngonjera, majazi na mighani. Kutokana na maelezo jumla ya Wanjala (k.h.j) tanzu mbalimbali huingiliana katika utendaji wake.

Bordwell (1989) anadai kuwa hakuna uainishaji wa tanzu unaowezekana. Tanzu zichukuliwe kuwa makundi hafifu ambayo hayawezi kufafanuliwa kwa misingi bainifu. Utanzu wa mwananadharia mmoja waweza kuwa kijitanzu kwa mwananadharia mwingine.

Uainishaji kwa makundi ulikuwepo tangu enzi za Aristotle, hivyo basi kwa misingi ya nadharia ya Tanzu ni kuwa uainishaji upo na unafuata mifumo au misingi tofauti. Dhana ya uwezekano wa kuingiliana kwa tanzu sio kikwazo cha kuondoa uainishaji kwa makundi ya tanzu na vipera. Misingi sawa ifuatwe kwa kutumikiza nadharia mahsusili ili pawe na usawa wa idadi na vigezo au misingi ya kuweka makundi hayo.

3.4 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia misingi mbalimbali ya kuainisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi inayoegemewa na maandishi tofauti. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu imebainika wazi kuwa tanzu zina sifa bainifu hivyo basi kuwa na uwezo wa kujisimamia. Misingi hii ni kama vile; Uwasilishaji, wahusika, wakati na kadhalika.

Sura hii pia imeonyesha uwezekano wa kuingiliana kwa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika utendaji wake. Kwa mfano, vijitanzu vya semi na ushairi vinaweza kutumika katika hadithi. Mfano methali katika wimbo zinaweza kuhusishwa katika hadithi za hurafa.

Uwezekano wa mwingiliano tanzu haufutulii mbali uainishaji wa tanzu. Mwingiliano huu ni wa kiutendaji tu. Hivyo basi tanzu zipo ulimwenguni na hazina kikomo. Kila utanzu una uwezo wa kijisimamia kwa sifa bainifu.

Sura inayofuata imeangazia suluhisho kwa utata unaotokea kutokana na uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

SURA YA NNE: SULUHISHO KWA UTATA WA UAINISHAJI WA TANZU ZA FASIHI SIMULIZI

4.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeshughulikia misingi ya uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Baadhi ya misingi hiyo ni: muundo, wahusika, maudhui, mahali, wakati na kadhalika. Kwa mujibu wa nadharia ya Tanzu imebainika kuwa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi zimejengeka kwenye misingi ya sifa bainifu. Kila utanzu una uwezo wa kujisimamia.


Sura hii imechunguza, suluhisho kwa utata wa uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi. Majibu ya wasailiwa kutokana na maswali ya hojaji yamewaongoza watafiti kubaini athari za uainishaji tofauti kwa wanafunzi na walimu. Kando na hayo, kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, suluhisho kwa utata huu zimebainishwa kwa kupendekeza njia mwafaka za utayarishaji wa vifaa na mpangilio wa matini.

4.2 Viwango Vya Umilisi Vya Wanafunzi

Karani (2016) anaeleza kuwa ufunzaji na utahini wa mashairi ya Kiswahili huathiri pakubwa umilisi wa wanafunzi. Aliongeza kuwa wanafunzi wengi walidai kuwa mashairi hayaeleweki. Alieleza kuwa baadhi ya mashairi yalipita viwango vya umilisi vya wanafunzi hivyo basi kuathiri matokeo yao. Anazidi kueleza kuwa takwimu za miaka kumi iliyopita, zilionyesha kuwa Baraza la Mitihani ya Kitaifa (Kenya national Examiation Council) liliegemea zaidi kutahini mashairi ya kimapokeo ikilinganishwa na mashairi huru.

Kutokana na majibu ya wanafunzi ilibainika kuwa fasihi simulizi ni mojawapo kati ya sehemu za karatasi ya tatu zenye ugumu. Wanafunzi hawa walieleza kuwa sehemu hizi huwa na ugumu kutokana na matini kubwa ambazo huhusishwa hasa vitabu teule. Waliongeza kuwa vitabu hivi huwa na wahusika wengi. Mchoro ufuatao unaonyesha sehemu hizi za karatasi ya tatu.

Sehemu za Karatasi ya Tatu zenye Ugumu



Mchoro 4.2: Sehemu za karatasi ya tatu

Walimu pia walikiri kuwa waliegemea utahini wa mashairi ya kimapokeo huku wakipuuza mashairi huru. Mashairi huru hayachaguliwi na wanafunzi wengi katika mtihani wa kitaifa kutokana na uhaba wa maarifa kuyahusu.

Munyao (2016) anaeleza kuhusu uchambuzi wa mashairi. Anadhihirisha kuwa iwapo mwanafunzi ataelekezwa vyema katika uelewa wa vipengele vyote vya kimsingi kuhusu ushairi ataweza kuchagua swali hili katika mtihani. Hivyo basi, mada za fasihi simulizi zinastahili kuangaziwa upya ili mwanafunzi awe na umilisi wa kutosha wa sehemu zote zinazotahiniwa.

Walimu walieleza kuwa wanafunzi wengi wana mielekeo hasi kwa somo la fasihi simulizi. Walieleza kuwa wanafunzi wengi hudai kuwa fasihi simulizi haina uhalisia.

Waliongeza kuwa inaonekana kongwe ikilinganishwa na usasa na matumizi ya mtandao katika elimu. Jedwali ifuatayo inaonyesha mielekeo hiyo.

Jedwali 4.1: Mielekeo ya fasihi simulizi

Mielekeo ya Fasihi Simulizi	Idadi ya Walimu	Asilimia
Chanya	3	38%
Hasi	5	62%

4.3 Mitaala ya Ufundishaji wa Fasihi Simulizi

Kwa mujibu wa nadharia ya Krashen (1982) ili vifaa vya kusoma vimsaidie mwanafunzi lazima viwe na maelezo yasiyo changamano. Vitabu tofauti vya Kiswahili kwa shule za upili vinawasilisha idadi tofauti ya tanzu za fasihi simulizi. Huu ni utata ambao umeweza kumtatiza mwanafunzi anayejiandaa kwa mtihani wa kitaifa. Ili kuondoa utata huu, suala la mtaala wa fasihi simulizi linafaa kuangaziwa upya ili mada zipangwe kwa utaratibu kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Si vyema kwa mwanafunzi wa kidato cha kwanza kuwasilishiwa tanzu zote tano za fasihi simulizi katika kiwango hiki. Utangulizi uhusishe tu historia ya fasihi simulizi na utanzu mmoja pekee. Katika kiwango hiki mwanafunzi asomeshwe tu vijitanzu vya hadithi. Kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, mada au dhana zitakuwa zimepangwa kuanzia rahisi hadi zile ngumu kwa viwango vinavyofuatia.

Walimu walieleza kuwa jinsi mada za fasihi simulizi zinawasilishiwa wanafunzi huathiri matokeo yao. Walipendekeza kuwa katika kidato cha kwanza utangulizi wa fasihi simulizi ufanywe kwa kina. Kisha tanzu kuu za fasihi simulizi kutangulizwa tu bila maelezo ya vijitanzu kama ilivyo katika jedwali.


Jedwali 4.2: Utaratibu wa kufundisha fasihi simulizi

Utaratibu Bora wa Kufundisha Fasihi Simulizi	Idadi ya Walimu	Asilimia
Kutanguliza	2	25
Kutanguliza na kutaja tanzu kuu pekee	4	50
Kutanguliza, kutaja tanzu kuu na kufundisha utanzu mmoja	1	12.5
Kutanguliza, kutaja tanzu kuu na kufundisha tanzu zote	1	12.5

Nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili inapendekeza kanuni wazi ziwepo za kufuatwa katika kutayarisha vifaa vya kufundishia ili viwe na usawa wa kuwasilisha matini. Hivyo basi vitabu vyote vilivyoidhinishwa vya kufundishia Kiswahili kwa shule za upili viwe na uainishaji kwa tanzu tano na kufuata misingi au vigezo sawa vya uainishaji ili pasiibuke utata kwa wanafunzi.

Kutokana na maelezo ya walimu, tanzu kuu za fasihi simulizi zinatofautiana kwenye vitabu. Walipendekeza pawe na misingi sawa ya kuainisha tanzu. Waliongeza kuwa waandishi wa vitabu waongozwe na silabasi. Mchoro ufuatao unaonyesha kutokana na wasailiwa kuwa idadi inayofundishwa ya tanzu inatofautiana.

Idadi ya Tanzu za Fasihi Simulizi



Mchoro 4.3: Idadi ya tanzu za fasihi simulizi

Ngugi (2008) anaeleza kuwa wataalamu wa taaluma ya ukuzaji mitaala kama vile Hooper (1971), Shiundu na Omulando (1992), Oluoch (2002) na Okech na Asiach (1992) wanakubaliana kuwa mtaala ni yaliyoangaziwa na taasisi za elimu ili kufuatwa na walimu katika ufunzaji wao. Wanataja hatua saba za ukuzaji mitaala kama vile:

- a) Uamuzi wa kisera
- b) Kutathmini mahitaji
- c) Kuunda mtalaa
- d) Kuandaa zana za kufudishia
- e) Majaribio
- f) Utekelezaji
- g) Tathmini

Ngugi (k.h.j) hatua hizo ni muhimu na iwapo mojawapo haitashughulikiwa kitaaluma huenda athari ikatokea katika utekelezaji wa mtalaa. Jukumu muhimu baada ya kuandaa mtalaa ni kuandaa zana za kufundishia ambapo maswali haya yatahughulikiwa:

- a) Ni zana zipi zinahitaji kuongezewa?
- b) Zitatayarishwa na nani au vipi?
- c) Zana mpya zitagharimu pesa ngapi?

Ngugi (k.h.j) anadai kuwa walimu hutumia miongozo na silabasi kwa njia isiyokuwa ya kitaaluma. Anadai kwamba hatua za uandalizi wa mitalaa hazikuhusisha walimu. Anaongeza kuwa iwapo washikadau wote hawatahusishwa kutoka hatua ya kwanza matatizo yanaweza kutokea.

Ni dhahiri kuwa utekelezaji wa silabasi ya fasihi simulizi una upungufu mkubwa. Hii ni kutokana na uainishaji tofauti wa tanzu kwenye vitabu vya Kiswahili. Tofauti hizi zinapelekea athari kuu kwa wanafunzi ambao hutahiniwa kuhusiana na vipengele tofauti vya fasihi simulizi. Hivyo basi suala hili linahitaji kuangaziwa upya ili kutatua utata uliopo.


4.4 Utahini na Ufundishaji wa Fasihi Simulizi

M`ngaruthi (2008) anaeleza kuwa lengo kuu la kumtahini mwanafunzi ni kujaribu kutathmini uwezo wake wa kuyashika, kuyahifadhi akilini na kuyatumia maarifa anayopata katika somo husika. Somo la fasihi simulizi ni muhimu kwa mwanafunzi katika shule ya upili. Mada za fasihi simulizi hutahiniwa katika mtihani wa kitaifa kwenye karatasi ya tatu. Swali la fasihi simulizi linaweza kuwa la lazima au lisiwe. Karatasi ya tatu ina maswali ya kuteua lakini la kwanza huwa la lazima kwa kila mwanafunzi.

Kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, mwanafunzi anastahili kuwasilishiwa mada zisizo changamano. Mada za fasihi simulizi zikiwasilishwa kuanzia dhana rahisi au za kimsingi na kujengea kwa ngazi au kiwango cha juu atakuwa na umilisi wa mada hizo kikamilifu. Mwanafunzi akitahiniwa katika kidato cha kwanza kutokana na kijisehemu kidogo cha utangulizi wa fasihi simulizi atajenga maarifa yake.

Walimu wengi walikiri kuwa karatasi ya tatu ya mtihani kwa wanafunzi wa kidato cha nne ni kiwango cha wanafunzi. Japo walibaini sababu kadhaa za wanafunzi wengi kutofanya vyema katika karatasi hii, mchoro ufuatao unaonyesha maswali yanafaa wanafunzi wa kidato cha nne.

Maswali ya Karatasi ya Tatu ni Kiwango cha Wanafunzi



Mchoro 4.4: Kiwango cha wanafunzi

Mgaruthi (k.h.j) anaorodhesha baadhi ya mada za kushughulikiwa ili kufaulu vyema katika mtihani unaohusisha fasihi simulizi:

- a) Maana ya fasihi simulizi
- b) Uhusiano na tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.
- c) Vipera na vijipera vya fasihi.
- d) Chimbuko au historia ya vipera hivyo.
- e) Uhusiano wa vipera na jamii (vipera hujitokeza vipi au hutumikizwa vipi katika jamii).
- f) Masuala ibuka na yanavyojitokeza katika vipera mbalimbali.
- g) Ukusanyaji na uhifadhi wa data na kadhalika.


Kutokana na maoni ya walimu ni vyema kuwepo na muhtasari wa mada zote muhimu za fasihi simulizi kama alivyoorodhesha Mgaruthi (k.h.j). Mwongozo kama huo utamfaa mwalimu na mwanafunzi katika matayarisho ya mitihani ya kitaifa.

Ben-Amos (1976) anaeleza vigezo mbalimbali vinavyofuatwa katika kugawa tanzu za fasihi simulizi katika makundi mbalimbali. Vigezo hivi ni kama kulinganisha na kulinganua tanzu. Kutokana na maoni ya walimu, awali mitihani imetahiniwa ikihusisha maswali ya ulinganisho wa tanzu za fasihi.

Kulingana na nadharia ya tanzu, wanafunzi waelezewe bayana kuwa tanzu zipo na zina sifa bainifu zinazozitofautisha na tanzu zingine. Maswali kama haya ya tanzu huwepo na yatazidi kuhusishwa katika mitihani ya kitaifa.

Walimu walieleza kuwa wanapata changamoto katika kufundisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Hii ni kutokana na vitabu tofauti kuwasilisha idadi tofauti ya tanzu kuu za fasihi simulizi. Tatizo hili la mgao bora wa tanzu linaathiri walimu wengi kama ilivyoonyeshwa hapo chini.

Walimu Kupata Utata Kufundisha Mgao wa Fasihi Simulizi



Mchoro 4.5: Walimu kupata Utata

Kwa mujibu wa ripoti ya Kenya National Examination Council (2019) Matokeo ya karatasi ya tatu mwaka 2019 yalishuka kwani alama ya juu iliyotunzwa ni 72/80. Ripoti hii inaonyesha kuwa wanafunzi asilimia 3.73 % walipata sufuri katika kila swali. Hii kutokana na walimu wa somo la Kiswahili inadhihirisha kuwa wanafunzi hawajamudu uelewa wa sehemu zote za karatasi ya tatu. Matokeo ya wanafunzi yamekuwa yakiyumbayumba katika mtihani wa kitaifa.

Mucai (2013) anaeleza kuwa matokeo ya mtihani ya wanafunzi wa shule za upili yamekuwa yakiathiriwa na vifaa vinavyotumiwa. Ifuatayo ni jedwali kuonyesha matokeo ya karatasi ya tatu tangu 2012.

Jedwali 4.3: Matokeo ya karatasi ya 102/3 tangu 2012 – 2019

Mwaka	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Alama Wastani	<i>32.14</i>	<i>34.82</i>	<i>42.93</i>	<i>38.80</i>	<i>25.67</i>	<i>25.15</i>	<i>22.20</i>	<i>21.08</i>
Alama Tenganishi	<i>15.15</i>	<i>14.92</i>	<i>15.81</i>	<i>15.38</i>	<i>12.87</i>	<i>13.42</i>	<i>11.92</i>	<i>12.64</i>


Muhtasari huu wa matokeo unadhihirisha kuwa utendaji wa watahiniwa unaendelea kudorora. Ripoti hii ilibaini kuwa watahiniwa wengi hawakumudu swali la fasihi simulizi, hasa kuainisha wimbo na kujadili mbinu mwafaka za kufanyia nyimbo utafiti.

Walimu walieleza kuwa katika karatasi ya tatu ni rahisi kwa mwanafunzi kujibu swali la fasihi simulizi na ushairi kuliko maswali ya vitabu teule. Hii ni kwa sababu mara nyingi mtahiniwa uhitajika kukumbuka muktadha wa majina ya wahusika kwenye vitabu teule ambayo huwa changamoto kubwa. Kando na hili masuala ya fasihi simulizi hayabadiliki ni yale yale kuanzia kidato cha kwanza tofauti na vitabu teule vilivyo na sehemu nyingi za uchambuzi na umulisi.

Baadhi ya wanafunzi walikiri kuwa fasihi simulizi ni rahisi ikilinganishwa na uchambuzi wa vitabu. Hata hivyo changamoto hujitokeza hasa kidato cha tatu na nne. Hii ni kwa sababu walimu wengi hujikita katika uchambuzi wa vitabu na kusahau mada muhimu za fasihi simulizi.

Wanafunzi walieleza kuwa fasihi inavutia isipokuwa somo la fasihi simulizi. Kama ilivyo katika mchoro, walieleza kuwa walipenda kuchambua vitabu vya fasihi ila sio kusoma uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi.

Somo la Fasihi Simulizi Linavutia



Mchoro 4.6: Mvuto wa somo

Walimu walieleza kwamba iwapo wanafunzi watazimudu vyema mada za fasihi simulizi na ushairi basi wana uwezo wa kupata alama wastani katika karatasi ya tatu. Hata hivyo walibaini kuwa wanafunzi wengi hawapendi mada hizi kutokana na ukawaida unaotumika kuzifundisha. Hizi ni mada zinazostahili kuhusisha ubunifu na kumchangamsha mwanafunzi kutokana na utendaji na uigizaji.

Nafula (2014) anadai kuwa, fasihi simulizi haijapata nafasi inayostahili katika kufundishia shule za upili nchini Kenya. Walimu walidai kuwa kuna changamoto ya muda unaotengewa somo la Kiswahili. Waliongeza kuwa, Kiswahili huwa ni kama masomo mawili yaliyounganishwa pamoja. Kando na hayo, muda huu hauwaruhusu kupitia kwa kikamilifu mada za sarufi, ufahamu, ufupisho, isimujamii, insha, uchambuzi wa vitabu vitatu teule, fasihi simulizi na ushairi.

Kwa mujibu wa Krashen (1982), ili ufundishaji uwe na mvuto, mbinu mbalimbali zihusishwe ili maarifa yapitishwe kwa msomaji kwa njia isiyo changamano. Walimu walipendekeza kuwepo kwa utendaji wa wanafunzi hasa katika karatasi ya tatu.

Mada za karatasi ya tatu zionyeshe kwenye filamu, video kuhusu tamaduni za kale na wanafunzi washiriki maonyesho ya fasihi simulizi. Kando na hayo walimu walipendekeza kuwepo mashindano ya mada za fasihi kwa jumla baina ya wanafunzi.

Ilibainika kuwa iwapo mambo hayo yatahusishwa katika kufundisha somo la Kiswahili wanafunzi watakuwa na mielekeo chanya kuhusu somo hili. Baadhi ya wanafunzi wanaofeli katika karatasi hii sio kutokana na ugumu wa mada bali ni mielekeo hasi. Walimu walibaini kuwa wanafunzi wengi hawapendi somo la fasihi simulizi.

Jedwali 4.4: Mielekeo ya Fasihi Simulizi


Mielekeo ya Fasihi Simulizi	Idadi ya Walimu	Asilimia
Chanya	3	38%
Hasi	5	62%

Baadhi ya wanafunzi waliripoti kuwa fasihi simulizi ni kongwe sana. Inafundisha masuala yaliyopitwa na wakati. Mfano miviga ya kupasha tohara au kutoa kafara. Waliongeza kuwa hakuna uhalisia wa baadhi ya mada za fasihi simulizi kwani hazina uhai katika karne ya 21 ambapo kila mtu anajihusisha na teknolojia ya kisasa.

Krashen (k.h.j) anapendekeza waandishi wa vitabu wasiwasilishe kazi zao kwa njia ya kawaida. Aliongeza kuwa, waibue mpangilio mpya wa kutumika kupitisha maarifa.

Walimu walipendekeza kuwa ili mada hizi za fasihi simulizi zisionekane kongwe sana zihusishwe katika teknolojia kwa kiwango kikubwa. Walipendekeza utendaji wa wanafunzi wenyewe katika masuala ya fasihi urekodiwe kisha rekodi hizi zihifadhiwe na kuonyeshwa mitandaoni kama ilivyoonyeshwa kwenye mchoro.

Wanafunzi Wahusishwe katika Utendaji wa Fasihi Simulizi



Mchor 4.7: Wanafunzi wahusishwe

Walimu walibaini kuwa mfumo wa kutahini karatasi ya tatu umebadilika. Swali lolote sasa linaweza kuwa la lazima tofauti na awali. Mfano, mwaka 2013 swali la lazima lilikuwa fasihi simulizi;

- a) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya vitanza ndimi (al 2)
- b) Fafanua majukumu sita ya vitanza ndimi katika jamii (al 6)
- c) Eleza mbinu sita unazoweza kutumia kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi (al 12)

Iwapo mwanafunzi hajapata maarifa kuhusu kijitanzu cha vitanza ndimi hana uwezo wa kujibu swali hili la lazima. Hivyo basi ataishia kufanya mtihani kwa alama $x/60$.

Maswali mengi ya karatasi ya tatu huhusiana na iwapo mwanafunzi atakosea a) basi huenda b) na ch) pia atakosea. Walimu walionyesha umuhimu wa kuzishughulikia mada za fasihi simulizi kwa kikamilifu ili kumwezesha mwanafunzi kuyamudu maswali ya karatasi ya tatu.


Iyaya na wengine (2016) wanaeleza kwamba sehemu zinazowatatiza wanafunzi katika ushairi ni istilahi na misamiati migumu. Kando na hayo, mbinu za lugha, mtindo na kuandika ushairi kwa lugha nathari pia huchangia utata wa umilisi wa wanafunzi. Zaidi ya hayo, waligundua katika utafiti wao kuwa ukosefu wa nyenzo za kutosha katika kufundishia somo la ushairi huathiri ufundishaji wa somo hili.

4.5 Vitabu vya Kufundishia

Mwikali na wengine (2024) wanaeleza kuwa vitabu vya kufundishia kwa shule za upili vinachangia matokeo ya wanafunzi kwa kiwango kikubwa katika kaunti ya Makueni. Wanasisitiza kuwa matumizi ya vifaa vya kufundishia yana mchango mkubwa katika elimu. Wanaongeza kuwa hakuna uhaba wa vitabu vya kufundishia katika Kaunti ya Makueni. Wanahitimisha kuwa sio ukosefu wa vifaa au vitabu unaopelekea kudorora kwa matokeo ya wanafunzi. Hii ilidhihirisha kuwa kuna sababu zingine zinazochangia matokeo mabaya katika mitihani.

Kutokana na utafiti nyanjani, walimu na wanafunzi walikiri kuwa vitabu vya kufundishia viko kwa kila mwanafunzi kwa uwiao wa 1:1. Vitabu vya Kiswahili vilivyoidhinishwa vipo katika shule teule zilizotafitiwa. Walidai kuwa japo vitabu hivi vipo vina dosari kubwa. Baadhi ya vitabu waliripoti kuwa vinawasilisha dhana ile ile kwa njia tofauti. Hii inapelekea kukosa uaminifu kwa yanayowasilishwa kwenye vitabu vyenyewe. Mchoro ufuatao unaonyesha vitabu vinavyopatikana shuleni.

Vitabu vya Somo la Kiswahili



Mchoro 4.8: Vitabu vya Kiswahili

Wasailiwa hawa walidai kuwa vitabu hivi vina matumizi ya istilahi zinazokinzana. Mfano, neno vipera, tanzu, vijitanzu na vijipera haijawaasilishwa kwa njia wazi. Waliongeza kuwa uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi umewasilishwa kwa idadi tofauti. Utata huu hata hivyo hauelezwi sababu zake katika vitabu hivi.

Kwa mujibu wa Ruthiri (2012), baadhi ya vitabu vinavyopendekezwa na K.I.E kwa wanafunzi ni vigumu sana au rahisi sana kwa wanafunzi wanaolengwa. Katika utafiti huu, walimu walipendekeza dhana za utangulizi wa fasihi simulizi pekee zihusishwe katika vitabu vya kidato cha kwanza. Walimu walidai kuwa wanafunzi wanapofundisha tanzu zote kwa pamoja watakuwa na changamoto ya kuzimudu.


4.6 Mbinu za Ziada za Kufundishia Fasihi Simulizi

Mwaniki na wengine (2022) wanapendekeza kuwa lazima walimu wahusishe mitindo mbalimbali ya kufundisha katika shule za upili.

Hii itachangia katika kuimarisha matokeo ya wanafunzi. Wanaongeza kuwa mitindo tofauti ya kufundisha huchangia mielekeo chanya ya wanafunzi kuhusu masomo mbalimbali.

Kando na vitabu, walimu wahusishe mbinu tofauti za kupitisha maarifa. Mbinu hizi mbadala ni kama vile; chati, vitu halisi, redio, kompyuta na kadhalika. Walimu na wanafunzi walipendekeza mbinu za ziada za kufundisha fasihi simulizi shuleni. Walikiri kuwa iwapo fasihi simulizi itafanywa kuwa na uhai huenda mielekeo ya wanafunzi ikabadilika. Mapendekezo yao ni kama ilivyoonyeshwa katika mchoro.

Mbinu za Ziada za Kufundisha Fasihi Simulizi



Mchoro 4.9: Mbinu za ziada

Walimu waliohojiwa walipendekeza mbinu zifuatazo kuimarisha umilisi wa wanafunzi;

- a) Maigizo ya wanafunzi.
- b) Programu za mitandaoni kama Swahilithub.
- c) Utumiaji wa hadithi miongoni mwa wanafunzi.
- d) Maonyesho ya vipindi vya runinga kuhusu fasihi simulizi.
- e) Ziara za wanafunzi nyanjani kutafiti kuhusu fasihi simulizi.

Kwa mujibu wa Mose (2012), wanafunzi walipendekeza vipindi vya redio vitumiwe kufundishia shuleni. Anataja baadhi ya mada ambazo zingewasilishwa kwa mfumo huu; ushairi, sarufi, fasihi, isimujamii na ufahamu.

Gatwiri (2015) anaeleza kuwa kumekuwa na maendeleo makubwa ya Kiswahili katika mtandao. Programu zimezinduliwa kuhakikisha kukua Kwa Kiswahili. Anaeleza kuwa swahilithub ndio tovuti kuu zaidi ya Kiswahili kote ulimwenguni. Tovuti hii inasheheni; habari, picha, video, hazina ya lulu za kale za Kiswahili, insha, hadithi, tasnifu za Kiswahili na kadhalika.

Walimu waliohojiwa walieleza kuwa programu hizi za mtandao zitawafaa wanafunzi sana. Hasa wanafunzi wenye mielekeo hasi kuhusu mada za fasihi simulizi kwani mada hizi huwasilishwa kwa mtindo wa kuvutia na kuburudisha. Mapendekezo ya walimu ni kama ilivyo katika jedwali.

Jedwali 4.5: Fasihi simulizi na mtandao

Fasihi Simulizi Kuhusisha Mtandao	Idadi ya walimu	Asilimia
Ndio	6	75
La	2	25

Akaka (2013) anaeleza kuwa fasihi simulizi hufunzwa katika lugha ya Kiswahili na mpaka sasa haijabainika iwapo mwalimu anafaa kufundisha fasihi simulizi ya waswahili au ya jamii mbalimbali nchini.

Anaongezea kuwa vitabu vya kufundishia havitoi maelezo ya kina. Kando na hayo, wanafunzi wa sasa hawajakuzwa na kulelewa katika mazingira ya kiutamaduni yatakayowawezesha kuelewa fasihi simulizi ya jamii zao.

Jambo hili anadai hutatiza ufundishaji wa tanzu za fasihi simulizi. Anapendekeza vifaa vya kuboresha ufundishaji kama;

- a) Vinasa sauti.
- b) Maandalizi ya sherehe zinazoonyesha matumizi ya vipera vya fasihi simulizi.
- c) Kuhudhuria shughuli za kitamaduni.
- d) Kuzuru sehemu za nchi ambako mambo ya kiutamaduni yangali yanazingatiwa.
- e) Matumizi ya picha na sinema za kimasomo kuhusu fasihi simulizi.

4.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia suluhisho kwa utata wa uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Imeangazia changamoto zinazokumba wanafunzi na walimu katika shule za upili nchini Kenya kuhusiana na fasihi simulizi.

Kwa misingi ya nadharia ya Krashen (1982), vifaa vya kufundishia vimekuwa na makosa ambayo yanahitaji kurekebishwa ili pawe na usawa wa dhana zinazopitishwa kwa wanafunzi. Isitoshe mada kwenye vitabu hivi hazijapangwa kwa utaratibu wa kuanzia dhana sahili hadi ngumu. Hivyo basi kuna haja ya mtaala kuangaziwa upya ili makosa hayo yarekebishwe.

Sura inayofuatia inatoa muhtasari wa matokeo, mapendekezo, changamoto za utafiti na mchango wa matokeo ya utafiti.

**SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO, MAPENDEKEZO,
CHANGAMOTO NA MCHANGO WA MATOKEO YA UTAFITI**

5.1 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilishughulikia suluhisho kwa baadhi ya changamoto zinazotokana na uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Sura hiyo ilijikita katika mihimili ya nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili kuhusu ubora wa vifaa vya kufundishia.

Sura hii imeeleza muhtasari wa matokeo, mapendekezo ya utafiti, changamoto za utafiti na mchango wa matokeo ya utafiti huu.

5.2 Muhtasari wa Sura

Sura tano zilitumiwa kwenye utafiti huu. Sura ya kwanza ilihusisha usuli wa mada, suala la utafiti, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka ya utafiti. Pia ilianguzia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti na nadharia.

Sura ya pili ilidhamiria kujibu swali la kwanza la utafiti. Ilianguzia uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi kwenye vitabu vilivyoidhinishwa. Ilibainika kuwa vitabu tofauti vilivyoidhinishwa kufundishia fasihi simulizi kwa shule za upili zilikuwa na uainishaji unaotofautiana wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Baadhi ya vitabu vina tanzu nne, vingine tano na vingine sita. Sura hii ilianguziwa kwa kurejelea misingi ya nadharia ya Utanzu na ya Ufundishaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili.

Sura ya tatu, ilijibu swali la pili la utafiti, kwa kuonyesha vigezo au misingi inayofuatwa katika uainishaji wa tanzu na vijitanzu. Ilibainika kuwa wataalamu na waandishi mbalimbali wa vitabu vya Kiswahili wanatumia vigezo tofauti kuainisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Matumizi haya ya misingi tofauti yamepelekea uainishaji unaotofautiana hivyo kuibua utata wa ni matini ipi bora kutumiwa katika kuelekeza mwanafunzi wa somo la fasihi.

Sura ya nne ilijibu swali la tatu kuhusu suluhisho kwa utata wa uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi. Baadhi ya suluhu kwa utata huo zilitokana na mchango wa walimu na wanafunzi wa shule za upili katika Kaunti ya Makeni. Baadhi ya suluhisho ni kuratibu vitabu ili viwe na matini sawa kuhusu uainishaji wa fasihi simulizi na kuhusisha mbinu za ziada katika kufundishia fasihi simulizi. Data hii ilitokana na maoni ya wanafunzi na walimu kuhusu uainishaji wa fasihi simulizi.

Sura ya tano imetoa muhtasari wa sura, matokeo ya utafiti, mapendekezo, changamoto za utafiti na mchango wa matokeo ya utafiti.

5.3 Matokeo ya Utafiti

Somo la fasihi simulizi ni muhimu katika shule za upili kwani ni sehemu muhimu katika silabasi. Ili kufikia malengo ya Somo la Kiswahili na kujenga maarifa ya mwanafunzi anayejiandaa kwa mtihani hasa karatasi ya tatu inayohusisha fasihi simulizi, misingi madhubuti lazima iwepo kuhusu mada za fasihi simulizi.

Utafiti huu ulijikita kuchunguza uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika vitabu vilivyoidhinishwa kufundishia fasihi simulizi kwa shule za Upili nchini Kenya. Utafiti huu umefanywa kwa misingi ya nadharia mbili.

Kwanza, nadharia ya Utanzu, iliyothibitisha kuwa tanzu zipo ulimwenguni, kila utanzu una sifa bainifu na tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi vina uwezo wa kujisimamia.

Pili, nadharia ya Ujifunzaji na upokeaji wa Lugha ya Pili ya Krashen, ilitibitisha kuwa vifaa vya kufundishia ni kigezo muhimu katika ufundishaji. Hivyo basi, mada katika vitabu zinastahili kuwa wazi bila utata wowote. Kando na hayo, mada ziwasilishwe kwa ngazi kuanzia mada rahisi katika kidato cha kwanza na kujengea zile ngumu kwa viwango vya juu. Zaidi ya hayo, makosa yanayojitokeza ya uwasilishaji yanastahili kurekebisha ili vitabu viwe vya manufaa kwa wanafunzi na walimu.

Kwa mujibu wa nadharia ya tanzu, utafiti huu ulionyesha kuwa uainishaji wa tanzu upo. Pia ilidhihirika kuwa, kila utanzu una sifa bainifu zinazoweza kusaidia kutofautisha na tanzu zingine. Kutokana na data ya maktabani, vitabu vilivyoidhinishwa kufundishia Kiswahili kwa shule za upili vilionyesha kuwa uainishaji upo. Hata hivyo vitabu hivyo vinaibua utata kutokana na uainishaji unaotofautiana wa fasihi simulizi.

Hivyo basi, vitabu vilivyoidhinishwa vilidhihirisha idadi tofauti ya tanzu kuu za fasihi simulizi. Kiswahili Kitukuzwe (uk 15) kina tanzu kuu sita, Johari ya Kiswahili (uk 79) ina tanzu kuu sita na Chemchemi za Kiswahili (uk 15) ina tanzu kuu nne ilhali Kiswahili Fasaha hakijabainisha wazi tofauti kati ya tanzu na vipera. Zaidi ya hayo, Kiswahili Fasaha hakijaonyesha uainishaji wazi wa tanzu hizi.

Aidha, vitabu vilivyorejelea tanzu kuu kuwa sita zinataja; hadithi, maigizo, semi, mazungumzo, ngomezi na ushairi simulizi. Kitabu kilicho na tanzu nne kinarejelea; hadithi, maigizo, semi na ushairi. Kutokana na matokeo hayo ni wazi kuwa kuna utata unaozuka kutokana na tofauti ya idadi na matumizi ya istilahi kama vile kipera na kitanzu.

Isitoshe kwenye vitabu hivi imebainika kuwa baadhi ya vijitanzu havitajwi kamwe. Mfano, Johari ya Kiswahili (2005) inataja jando na unyago pekee kama vijitanzu vya maigizo ilhali Kiswahili Kitukuzwe (2019) kina; majigambo, michezo, unyago, jando, vichekesho na ngonjera.

Maelezo haya yanabainisha changamoto anazokumbana nazo mwanafunzi akisoma kuhusu tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

Pamoja na hayo, lengo la pili lilibainisha kuwa uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi unaegemea misingi tofauti. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya tanzu, kuna mifumo inayofafanua muundo wa tanzu. Mifumo hii ni vigezo mbalimbali vinavyofuatwa na wataalamu katika kuandika matini za fasihi simulizi. Zaidi ya hayo, utafiti huu ulibaini kuwa uainishaji tofauti unatokana na wataalamu kuegemea misingi tofauti ya kuainisha. Misingi hii ya kuainisha ni kama vile; muundo, maudhui, wakati, mtindo, wahasika na kadhalika.

Kando na hayo, lengo hili la pili liliibua sababu za utata unaojitokeza katika vitabu vilivyoidhinishwa. Ilibainika kuwa sababu ya idadi kinzani ya tanzu za fasihi simulizi ni misingi yake. Kwa mujibu wa nadharia ya Ujifunzaji na Upokeaji wa Lugha ya Pili, iwapo mada zitawasilishwa kwenye vifaa kwa njia isiyo wazi basi kutakuwa na changamoto kwa wasomaji. Isitoshe, nadharia hii ilibaini kuwa matini zinazowasilishwa kwenye vitabu zinastahili kuwa rahisi. Matini kwa kidato cha kwanza ziwe rahisi kisha zijengee kwa mada changamano katika ngazi za juu. Hivyo basi, mada za fasihi simulizi zitangulizwe kwa utaratibu unaofaa ili mwanafunzi awe na umilisi wa mada hizo.

Kutokana na lengo la tatu, ilibainika kuwa mada za fasihi simulizi zinastahili kuratibiwa upya ili ziwafae wanafunzi. Matokeo yaliyotokana na hojaji za wasailiwa yalidhihirisha kuwa kuna utata katika ufundishaji na usomaji wa uainishaji wa fasihi simulizi. Zaidi ya hayo, vitabu vilivyoidhinishwa vimebainika kuwa na makosa kwenye mada hizi za fasihi simulizi. Makosa haya yanastahili kurekebisha ili somo hili liwe la manufaa kwa wasomaji.

Aidha, wasailiwa walieleza kuwa baadhi ya matini za fasihi simulizi zina maelezo finyu sana ambayo yanamfanya mwanafunzi kukosa umilisi katika karatasi ya tatu. Pia, kutokana na maelezo ya wasailiwa baadhi ya mada za fasihi simulizi ni ngumu kwa sababu zinafundishwa kwa mtindo wa kawaida wa kutumia vitabu darasani. Mbinu mbadala za kufanya somo livutie zilipendekezwa.

Mwisho, utafiti huu ulidhihirisha ya kuwa uainishaji tofauti wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi huathiri upokezi na matokeo ya wanafunzi. Pia, ulionyesha kuwa uainishaji tofauti hutokana na vigezo tofauti vya kuainisha vinavyotumiwa na waandishi wa vitabu. Wasomaji walikiri kuchanganyikiwa kutokana na uainishaji huu.

Baadhi ya mada za karatasi ya tatu zimejikita kwenye tanzu za fasihi simulizi. Hivyo basi, ni muhimu kutilia maanani sehemu zote za somo ili kukuza umilisi wa wanafunzi na kupata matokeo yanayofaa.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi katika vitabu vilivyoidhinishwa kwa kuangazia shule teule katika Kaunti ya Makueni nchini Kenya. Kutokana na matokeo ya utafiti huu watafiti au wasomi wanaweza kujikita katika kutafitia kuhusu mbinu za ziada za kufundishia fasihi simulizi.

Pia tafiti zaidi zinaweza kufanywa katika somo hili kwa kuchunguza nafasi ya fasihi simulizi katika maendeleo ya kitekolojia.

5.5 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto kadhaa. Kwanza, changamoto ya safari ndefu na gharama kubwa ya kwenda maktabani kufanya utafiti. Hata hivyo, mtafiti aliweza kupata nafasi kazini wakati wa likizo. Pili, gharama ya kupiga chapa na kutolesha nakala. Mtafiti alipata msaada wa kifedha.

Tatu, katika kipindi cha kuufanya utafiti huu, mtafiti alikuwa kazini. Changamoto ya kumudu malengo kazini na kufikia malengo ya utafiti ziliibuka. Licha ya hayo, kwa ukakamavu utafiti uliweza kukamilika kupitia muda wa likizo na ruhusa mara chache kazini. Isitoshe, haikuwa rahisi kuchagua shule nne katika kaunti nzima. Mtafiti alibaini kwa usaidizi wa walimu kubaini shule za viwango tofauti vya umilisi. Kando na hayo yote, mwishowe utafiti nyanjani ulikamilika na uchanganuzi wa data kufanywa.

5.6 Mchango wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu unaweza kusaidia waandishi wa vitabu ili kuelewa zaidi kuhusu uainishaji tofauti. Waandishi wanapotumia misingi tofauti kuainisha tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi waeleze bayana misingi inayopelekea uainishaji wao. Hili litapunguza viwango vya wanafunzi kuchanganganyikiwa

Waandishi wa vitabu vya wanafunzi wafuate silabasi. Silabasi iwe na maelezo ya kutosha kuongoza waandishi hao. Misingi au vigezo sawa vihimizwe ili pawe na usawa wa matini ya wanafunzi. Dhana zinazowasilishwa kwenye vitabu zijengeane kutoka kiwango kimoja hadi kingine.

Waratibu wa mitaala pia wawe makini wanapochagua vitabu ili kuviidhinisha. Visiwe na utata kuhusu dhana zilezile. Iwapo makosa yatakuwepo yarekebishwe kabla vitabu hivyo kuchapishwa. Matini kwenye nakala hizi ziwe sahili kwa kutanguliza dhana kwa ngazi za viwango vya umilisi vya wanafunzi.

5.7 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia matokeo ya utafiti. Imedhihirisha kuwa uanishaji wa idadi ya tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi unatofautiana kwenye vitabu vilivyoidhinishwa kufundishia Kiswahili kwa shule za upili nchini Kenya.

MAREJELEO

- Akaka.I. (2013). Changamoto zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule zaUpili Nchini Kenya. *Kioo Cha Lugha, 11*, 52–56.
- Akivaga, S. K., & Odaga, A. (1985). *Oral Literature: A School Certificate Course*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Bascom, W. (1953). Folklore and Anthropology. *Journal of American Folklore, 66*(262), 282–290. <https://doi.org/10.2307/536722>
- Bazmaleh, A. S. (2006). *Winner of Special Category, Human Rights Award*. Webb Memorial Library.
- Ben-Amos, D. (1976). *Folklore Genres*. Austin: University of Texas, Austin Press.
- Bordwell, D. (1989). *Making meaning: Inference and Rhetoric in the Interpretation of Cinema*. Cambridge: Harvard University Press.
- Chandler, D. (1997). An Introduction to Genre Theory. Retrieved April 29, 2021, from http://www.aber.ac.uk/media/Documents/intgenre/chandler_genre_theory.pdf
- Duff, D. (2000). *Modern Genre Theory*. University of Michigan: Longman.
- Etyang, E. K. (1987). *Strategies and Media for Teaching and Learning Oral Literature in Kenya*. M.ED Thesis, Kenyatta University.
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Cambridge: United Kingdom Open Book Publishers.
- Gatwiri, J. . (2015). *Tathmini ya Hadithi za Watoto Katika Mtandao*. Kenyatta University.
- Hodge, Robert, & Kress. (1988). *Social Semiotics*. Cambridge: Polity.
- Iyaya.R, K. . & L. . (2016). Uchanganuzi wa Mambo yanayoathiri Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili Nchini Kenya. *Mara Research Journal of Kiswahili, 1*(1), 18–36.
- Kabira, M. W., & Mutahi, K. (1988). *Gikuyu Oral Literature*. Nairobi: Heinemann Educational Publishers.
- Karani.J. (2016). *Upokezi wa Wanafunzi wa Shule za Upili kuhusu Mashairi ya Kiswahili katika Jimbo la Nakuru*.
- Kenguru, P. M. (2013). *Athari za Fasihi Simulizi Katika Riwaya ya Utubora Mkulima*. University of Nairobi.
- Kenya Institute of Education. (2002). *Secondary Syllabus Volume I*. Nairobi: KIE Curriculum Development and Research Centre.
- Kenya Literature Bureau. (2009). *Kiswahili Kitukuzwe: Kitabu Cha Wanafunzi Kidato Cha Nne*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kenya National Examination Council. (2019). *Fasihi ya Kiswahili 102/3*.

- Kerlinger, F. N. (1981). *Foundations of Behavioural Research* (Second). New York: Holt, Rinehart and Winston Inc.
- Kiai, W. A., & Mokuu, G. M. (2013). Textbook Selection Experiences among Secondary School Teachers of English in Kenya. *International Journal of Education and Research. IJER*, 1(12), 2–6.
- Kobia, J. (2006). Uchapishaji wa Fasihi Simulizi Nchini Kenya: Matatizo, Changamoto na Mustakabali wake. In K. Njogu, C. Momanyi, & M. Mathooko (Eds.), *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Twaweza Communications.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.
- Kothari, C. R. (2007). *Research Methodology: Methods and Techniques*. Mumbai, India: New age International Publishers.
- Krashen, S. (1982). *Principles and Practice in Second Language Acquisition*. Oxford: Pergamon Press.
- Krashen, S. (1985). *The Input Hypothesis. Issues and Implications*. London: Longman Group UK Ltd.
- Kress, G. (1988). *Communication and Culture: An Introduction*. Kensington: New South Wales University Press.
- Kuloba, P. . (2015). *Mwingiliano Matini Katika Cheche za Moto na Kidagaa Kimemwozea*. Kenyatta University.
- Kyung, P. J. (2004). *The Oral - Written Interface in the Swahili Fictional Prose*. university of Nairobi.
- Lorna, W. (2012). Teachers Attitude Towards the Integrated Method of Teaching Oral Literature in Secondary Schools in Uasin - Gishu County, Kenya. *Journal of Emerging Trends in Educational Research and Policy Studies (JETERAPS)*, 3(4), 487–494.
- Mngaruthi, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni: Kitabu cha Walimu na Wanafunzi (Shule na Vyu)*. Nairobi, Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.
- Magambo, E., Simiyu, F., Amukowa, D. (2019). Mchango wa Tamasha za Muziki katika Ufundishaji wa Uainishaji wa Nyimbo katika Shule za Upili Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, 4(1).
- Magambo, E. (2019). *Mchango wa Tamasha za Muziki katika Ufundishaji wa Uainishaji wa nyimbo katika Shule za Upili Nchini Kenya*. Kibabii University.
- Matei, A. (2011). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Nairobi, Kenya: Oxford University Press.
- Mbughuni, P. M. (1987). *From Oral to Written: The Politicization of Kiswahili Literature*. University of Indiana.
- Miller, C. R. (1984). Genre as Social Action. *Quarterly Journal of Speech.*, 70(2), 151–167. <https://doi.org/10.1080/00335638409383686>

- Ministry of Education. (1998). *National Policy on Textbooks Publishing, Procurement and Supply for Primary schools*. Nairobi.
- Mose. P. (2012). *Mielekeo na Uelewa wa Walimu na Wanafunzi wa Sekondari kuhusu Vipindi vya Redio vya Taasisi ya Elimu Nchini Kenya: Utafiti wa Nairobi*. Kenyatta University.
- Mucai, E. W. (2013). *Availability and Utilization of Educational Resources in Influencing Students Performance in Secondary Schools in Mbeere South, Embu County, Kenya*. M.ED Thesis, Kenyatta University.
- Mugenda, O., & Mugenda, A. (2003). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.
- Muiruri, P. K. (2006). *Maandalizi Mufti ya KCSE Fasihi Simulizi: Maswali na Majibu*. Nairobi: Palco Enterprises Ltd.
- Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasuhi Simulizi. Mulika Na. 21*.
- Mumbo, C. K., & Ngamia, F. O. (2005). *Johari ya Kiswahili Kidato cha Nne*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Munyao.M.K. (2016). *Uhuru wa Kishairi katika Utunzi wa Mashairi: Uchanganuzi wa Sikate Tamaa na Miale ya Uzalendo*. Kenyatta University.
- Murimi, J., Obuchi, S., Kandagor, M. (2016). Mwingilianotanzu katika uainishaji wa tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiswahili. *Journal of Educational Research (IJRD)*., 1(2).
- Mwaniki.W, Ogola.M, & N. . (2022). Influence of Instructional Resources on Quality of Education in Public Secondary Schools in Murang`a County, Kenya. *African Journal of Education & Practice*, 8(4), 21–32.
- Mwikali.A, K. . &Ogeta. . (2024). Utilization of Textbooks and its Influence on Students` Academic Performance in Public Secondary Schools in Makeni County, Kenya. *Journal of Education*, 4(2), 21–34.
- Nafula, M. (2014). *Challenges of Teaching The Expanded Kiswahili Syllabus in Secondary Schools: A study of Selected Secondary Schools in Trans Nzoia County, Kenya*. Master Thesis, Moi University.
- Namanya, E. (2015). *Dhima ya Misemo na Nahau katika Jamii ya Wakiga Wilayani Kabale Kusini Magharibi mwa Uganda*. Master Thesis, Pwani University.
- Ngugi.B. (2008). *Tathmini ya Mtaala wa Isimu Jamii wa Shule za Upili Nchini Kenya*. Kenyatta University.
- Njogu, K., Momanyi, C., & Mathooko, M. (Eds.). (2006). *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi.
- Odeo, I. (2006). Matatizo ya Kufundisha Fasihi Simulizi Katika Shule za Upili. In M. Njogu.K., Momanyi, C., Mathooko (Ed.), *Fasihi Simulizi ya Kiswahili* (pp. 30–31). Nairobi, Kenya: Twaweza Communications.

- Odeo, I. O. (2006). Matatizo ya Kufundisha Fasihi Simulizi katika Shule za Upili. In K. Njogu, C. Momanyi, & M. Mathooko (Eds.), *Fasihi Simulizi ya Kiswahili* (pp. 29–40). Nairobi: Twaweza Communications.
- Ogechi, N., Shitemi, L., & Simala, L. (2008). *Nadharia Katika Taaluma Ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press.
- Okemwa. M. (2017). *Mchango wa Fasihi Simulizi katika Fasihi Andishi: Mfano wa Visasili katika Mafuta (1984) na Walenisi (1995)*. Kenyatta University.
- Oni, J. (1995). *Educational Resources: An Introduction*. Abeokuta: Gbemi Sodipo Press Limited.
- Propp, V. (1968). *Morphology of the Folktale*. Texas: University of Texas, Austin Press.
- Ruthiri. M. (2012). *Tathmini ya Ufaafu wa Vitabu vya Kusoma kwa Madarasa ya 5 na 6 katika Shule za Msingi: Mifano ya waandishi wanne*. Kenyatta University.
- Saunders, D. J. (1974). Visual Communication Handbook. In *Teaching and Learning Using Simple Visual Materials*. London: United society for Christian Literature, Luther-Worth Press.
- Stam, R. (2000). *Film Theory*. Oxford: Blackwell.
- TUKI. (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (4th ed.). Nairobi, Kenya: Oxford University Press East Africa Ltd.
- Vansina, J. (1985). *Oral Traditions as History*. Nairobi, Kenya: Heinemann Educational Publishers.
- Vansina, Jan. (1985). *Oral Tradition as History*. Wisconsin: The University of Wisconsin Press.
- Wafula, R. M., & Kimani, N. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Waititu, F., & Ipara, I. (2005). *Kiswahili Fasaha Kidato cha Nne*. Nairobi, Kenya: Oxford University Press East Africa Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003a). *Chemchemi za Kiswahili Kidato cha Nne*. Nairobi, Kenya: Longhorn Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003b). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Focus Publications Ltd.
- Wanjala, S. (2007). *Nyiso za Wabukusu: Maudhui na Lugha*. Kenyatta University.
- Wanjala, S. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi: Kwa Shule, Vyuvo na Ndaki*. Mwanza, Tanzania: Serengeti Bookshop.
- Wanjala, S. (2015). *Mwingilianotanzu Katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: Mfano wa Embalu wa Mwakakongwa*. Kenyatta University.

VIAMBATISHO

Kiambatisho A: Barua ya NACOSTI



REPUBLIC OF KENYA

Ref No: 903606

RESEARCH LICENSE

Date of Issue: 25/April/2024


**NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION**




This is to Certify that Ms. Carolyn Nzilani Munyao of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Makeni on the topic: TATHIMINI YA UAINISHAJI WA TANZU NA VIJITANZU VYA FASIFI SIMULIZI KATIKA VITABU VILIVYOIDHINISHWA: KAUNTI MAKUENI, for the period ending : 25/April/2025.

License No: NACOSTI/P/24/34942

Applicant Identification Number: 903606

Director General
Walthero
**NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE, TECHNOLOGY &
INNOVATION**

Verification QR Code



**NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document,
Scan the QR Code using QR scanner application.**

See overleaf for conditions

Kiambatisho B: Barua ya Idhinisho



KENYATTA UNIVERSITY GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Executive Dean, Graduate School
TO: Carolyne Nzilani Munyao
C/o Kiswahili & African Languages Dept.

DATE: 27th March, 2024
REF: C50/CE/34394/2016

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL


This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 13th March, 2024 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, "Tathmini ya Uainishaji wa Tanzi na Vijitanzu vya Fasihi Simulizi katika Vitabu Vilivyoidhinishwa: Kaunti ya Makeni, Kenya."

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed supervision tracking and progress report forms per semester. The forms are available at the university's website under Graduate School webpage downloads.

Also, please ensure that you publish article(s) from your project before submitting it to Graduate School for examination as per the Commission for University Education and Kenyatta University guidelines.

Thank you.


ELIJAH MUTUA
FOR: EXECUTIVE DEAN, GRADUATE SCHOOL

c.c. Chairman, Kiswahili and African Languages Department

Supervisors:

1. Dr. Jesse Murithi
C/o Department of Kiswahili & African Languages
Kenyatta University

EM/mo

Kiambatisho C: Hojaji kwa Wanafunzi

MASWALI KUHUSU TATHMINI YA UAINISHAJI WA TANZU NA VIJITANZU VYA FASIHI SIMULIZI KATIKA VITABU VILIVYOIDHINISHWA KUFUNDISHA KISWAHILI KWA SHULE ZA UPILI NCHINI KENYA.

Wewe ni miongoni mwa wanafunzi walioteuliwa ili kutoa habari na ujumbe ambao utakuwa wa manufaa katika utafiti huu, ili tuweze kuelewa mielekeo ya wanafunzi kuhusu uainishaji wa tazu za fasihi simulizi.

Maelezo yote utakayotoa yatahifadhiwa na kuwekwa siri. Unaombwa kujibu maswali yafuatayo kwa kutia mkwaju kwenye vijisanduku vya aidha ndio au la na kujibu nafasi zingine zilizoachwa wazi.

Maswali,

1. a) Taja idadi ya tazu kuu za fasihi simulizi?

b) Orodhesha tazu hizo kuu.
2. Je, ni vitabu vipi vya kusoma mnavyotumia darasani vya somo la Kiswahili?
3. a) Katika somo la fasihi simulizi mlielezewa misingi ya uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi?

Ndio

La

b) Iwapo jibu lako ni ndio taja baadhi ya misingi ya kuainisha tanzu za fasihi simulizi.

4. Orodhesha baadhi ya mada za karatasi ya tatu ambazo zina utata au ni ngumu kuelewa.

5. a) Vitabu mnavyotumia darasani vya Kiswahili vinaainisha fasihi simulizi?

Ndio

La

b) Je, unaona utata wowote kutokana na vitabu hivyo kuhusu uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi.

Ndio

La

c) Eleza utata huo kwa kifupi.

6. Orodhesha baadhi ya mada katika fasihi simulizi ambazo hazijaelezewa kikamilifu.

7. a) Walimu wako wa Kiswahili wanapofundisha wanaeleza tanzu zinazotofautiana au wote hutaja idadi sawa ya tanzu za fasihi simulizi?

b) Iwapo wanaeleza tanzu zinazotofautiana, je wanaeleza sababu zao za kutaja

idadi tofauti?

Ndio La

c) Iwapo jibu lako ni ndio, baadhi ya sababu wanazoeleza walimu kwa kueleza idadi tofauti ya tanzu ni zipi?

8. Pendekeza baadhi ya mbinu za ziada zinazoweza kutumiwa katika kufundisha ili kufanya somo la fasihi simulizi kuvutia zaidi.

Kwa maoni yako kuna faa kuwoko na mabadiliko au marekebisha ya uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi kweye vitau vya Kiswahili?

Ndio La

9. Je, mada za fasihi simulizi kwenye vitabu mnavyotumia darasani zinaafiki viwango vifuatavyo?

a) Binafsi unafurahia mada hizo?

Ndio La

b) Unazielewa mada hizo vyema?

Ndio La

c) Unaweza kusoma mada za fasihi simulizi kwa madhumuni tofauti mbali na kujitayarishia mtihani?

Ndio La

SHUKRANI SANA KWA WAKATI WAKO NA KWA KUSHIRIKI KATIKA KUJAZA HOJAJI HII.

Kiambatisho D: Hojaji kwa Walimu

MASWALI KUHUSU TATHMINI YA UAINISHAJI WA TANZU NA VIJITANZU VYA FASIHI SIMULIZI KATIKA VITABU VILIVYOIDHINISHWA KUFUNDISHA FASIHI SIMULIZI KWA SHULE ZA UPIILI NCHINI KENYA.

Wewe ni miongoni mwa walimu walioteuliwa ili kutoa maoni yako na habari au ujumbe ambao tunatarajia utakuwa wa manufaa katika utafiti huu.

Unaombwa kutoa majibu kwa kweli na taarifa yoyote ya ziada inayoweza kufanikisha utafiti huu. Taarifa zote zitawekwa faraghani na kubakia kuwa siri. Nakuhakikishia majibu utakayotoa ni ya utafiti huu pekee.

Unaombwa kujibu maswali kwa kutia alama ya mkwaju au kujaza jibu mwafaka katika sehemu zilizoachwa wazi.

Maswali,

1. Je, katika chuo kikuu au ndaki ulisoma kozi yoyote inayohusu fasihi simulizi?

Ndio

La

2. a) Mnatumia vitabu vipi vya somo la Kiswahili vilivyoidhinishwa?

Viorodheshe

- b) Mada kwenye vitabu hivi zinaelezwa kwa kikamilifu au zina upungufu?

3. a) Je, umeweza kupata utata wowote unapofundisha uainishaji wa tanzu kuu za fasihi simulizi?

Ndio

La

b) Iwapo umebaini utata katika idadi ya tanzu zilizoainishwa, eleza kwa kifupi utata huo.

c) Kwa maoni yako ni mgao upi bora zaidi kwa mwanafunzi au ulio sahihi kutumiwa?

d) Kwa nini umependekeza mgao huu, je, umeegemea misingi ipi kuuchagua?

4. a) Je, unadhani uainishaji tofauti unawaathiri wanafunzi?

Ndio

La

b) Iwapo jibu lako ni ndiyo, wanafunzi hao huathirika vipi?

5. Toa mifano miwili ya maswali ambayo yanahusu uainishaji wa tanzu na vijitanzu vya fasihi simulizi

6. Je, maswali yanayotahiniwa katika karatasi ya tatu ni ya kiwango cha wanafunzi wa kidato cha nne?

7. a) Je, unadhani taasisi ya kuratibu mitaala imetekeleza jukumu lake ipasavyo katika kuidhinisha vitabu vya kufundishia fasihi simulizi?

Ndio

La

b) Iwapo jibu lako ni la, ni ithibati gani inaonyesha hawajafaulu, eleza.

c) Unadhani walimu wengine wa Kiswahili nchini Kenya wanapata utata huu wa kufundisha uainishaji wa tanzu za fasihi simulizi?

Ndio

La

8. a) Kwa maoni yako, taja baadhi ya sababu zinazopelekea wanafunzi kutofanya vyema katika sehemu ya fasihi simulizi katika karatasi ya tatu.

9. Pendekeza suluhisho kwa utata unaojitokeza katika mada za fasihi simulizi, hasa kuhusu uainishaji.

10. Mielekeo ya wanafuzi wako kuhusu somo la fasihi simulizi ni ipi?

Chanya

Hasi

11. Utaratibu bora zaidi wa kufundisha fasihi simulizi ni upi?

a) Kutanguliza

b) Kutanguliza na kutaja tanzu kuu pekee

c) Kutanguliza, kutaja tanzu kuu na kufundisha utanzu mmoja

d) Kutanguliza, kutaja tanzu kuu na kufundisha tanzu zote

12. Orodhesha mbinu za ziada za kufundisha fasihi simulizi zinazoweza kulisimua wanafunzi.

SHUKRANI SANA KWA WAKATI WAKO NA KWA KUSHIRIKI KATIKA KUJAZA HOJAJI HII.